Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 13 Aprili,2010**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa na Wabunge)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

*(Saa 3.03 Mitambo ya Sauti iliacha kufanya kazi na Bunge Kuahirishwa kwa muda)*

*(Saa 5.00 Asubuhi Bunge lilirudia katika Ukumbi wa Pius Msekwa kutokana na kutotengamaa kwa haraka Mitambo ya Sauti ya Ukumbi Mpya wa Bunge)*

**SPIKA:** Tafadhali tukae, Katibu kwa Orodha ya shughuli za leo.

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, samahani tulianza na tulisema isomwe taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kumbe ni hii taarifa yangu. Kwanza niseme tu tatizo la ufundi kule linashughulikiwa na tunadhani kesho tunaweza kuwa tumepata ufumbuzi, kikubwa ni ile ramani ya *electronic* inayotawala kufungua vile vipaza sauti.

Taarifa yangu ni kama ifuatavyo. Katika mkutano wa kumi na nne wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada minane ya sheria kama ifuatavyo:-

*The Nursing and Midwifery Bill* 2009, *The Written Laws Miscellaneous Amendment* namba tatu, *The Electronic and Postal Communication Bill 2008, The National Security Council Bill 2008, The Architects and Quantity Surveyors Registration Bill 2008, The Supplementary Appropriation for the Year 2009/2010 Bill, 2010,The Election Expenses Bill* 2009 na *The Election Laws Miscellaneous Amendments Bill 2009.*

Baada ya kupitishwa na Bunge na baadaye kupitia katika hatua zake zote za uchapishaji, miswada hiyo ilipelekwa kwa mujibu wa Katiba kwa Mheshimiwa Rais na

leo ninafurahi kuwaarifu kwamba Mheshimiwa Rais amekwisha toa kibali chake kwa Miswada sita ifuatayo: -

*The Nursing and Midwifery Act 2009* itakuwa ni sheria namba moja ya mwaka 2010, *The Written Laws Miscellaneous Amendments* itakuwa namba tatu ya mwaka 2009, namba mbili ya mwaka 2010, Sijui kwa nini wameandika namba tatu. Basi kwa maana ya sheria ni namba mbili ya mwaka 2010.

*The Architects and Quantity Surveyors Registration Act 2009* ambayo yenyewe sasa itakuwa ni namba nne ya mwaka 2010,*The Supplementary Appropriation Bill* ambayo sasa ni sheria namba tano ya mwaka 2010, *The Election Expenses Act 2009* inakuwa ni sheria namba sita ya mwaka 2010 na *National Security Council Act 2009* ni sheria sasa namba nane ya mwaka 2010. Kingine tu nawapa taarifa kwamba katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa, Mheshimiwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali atatoa taarifa yake kwa mujibu wa Kanuni ya 37(1) ya Kanuni zetu, toleo la Kanuni ya mwaka 2007.

Kwa hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha taarifa yake ya mwaka 2008 na tumempangia tarehe 20 Aprili, 2010 kwa shughuli hiyo. Ahsanteni sana. Katibu, kwa shughuli inayoendelea.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Uratibu na Sera.

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Kumi na nane wa Bunge uliopita. Naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Uhakiki wa Majina katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA (K.n.y. MHE. NURU AWADHI BAFADHILI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wanaojiorodhesha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura hupewa shahada maalum na hutakiwa kufanya uhakiki wa majina yao siku chache kabla ya uchaguzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wananchi kuhakiki majina angalau mwezi mmoja kabla ya uchaguzi ili kurekebisha kasoro zinazojitokeza mara kwa mara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge Viti Maluum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria za uchaguzi wananchi waliojiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura hupewa shahada maalum inayojulikana kama (Kadi ya Mpiga kura) na hutakiwa kufanya uhakiki wa taarifa zao zilizoko katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kipindi cha kuweka wazi Daftari la Wapiga kura katika maeneo husika kama itakavyokuwa imepangwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Uhakiki wa taarifa za Mpiga Kura kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi uko wa aina mbili, ambapo uhakiki wa kwanza ufanywa kila mara baada ya uandikishaji au uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga kura kwa kuweka wazi Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Uhakiki huu hufanyika katika vituo vyote vya kila kata kwa muda usiozidi siku saba au muda ambao Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakaoona unafaa. Hii huwezesha wananchi waliojiandikisha au kubadili taarifa zao kupata fursa ya kuhakiki taarifa zao. Iwapo wataona kasoro zimejitokeza kama vile kukosewa jina, jina la mtu aliyeandikishwa kutokuwepo kwenye Daftari, kuwepo jina la mtu asiyestahili kuwepo kwenye Daftari na kasoro nyingine, kasoro hizo huwasilishwa Tume kwa ajili ya kurekebishwa na hatimaye Tume kutoa Daftari lililorekebishwa na kuwa sahihi kwa ajili ya siku ya kupiga kura. Uhakiki wa pili ndio ule unaofanyika siku nane kabla ya Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi.

Lengo la uhakiki huu ni kumwezesha mpiga kura aliyejiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kujua Kituo kipi amepangiwa kupiga kura ili kuepuka usumbufu au kubabaika siku ya kupiga kura. Kwa kuwa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura hufanyijka mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na mwingine, ni dhahiri kuwa wananchi hupata fursa mara mbili ya kuhakiki taarifa zao. Fursa hiyo hutolewa mapema sana kabla ya siku ya uchaguzi na hutumika kurekebisha kasoro mbali mbali.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umuhimu wa uhakiki wa Daftari kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kuhakikisha kwamba kasoro mbalimbali zinaondoka, lakini kwanza naomba niulize swali langu hili. Je, pamoja na uhakiki huo wa mara mbili wa

Daftari la Wapiga Kura , kwanini siku ya Kupiga Kura bado mtu anaenda kituoni anakuta jina lake halipo au kuna jina la mtu mwingine, picha ni ya mtu mwingine. Ni sababu gani inayosababisha hivyo?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwa sababu mtu anapojiandikisha ndipo anapotakiwa kupiga kura, kwanini kuwe na tatizo la kumkuta mtu kapangiwa kituo kingine wakati kile ndio kituo chake ambacho amejiandikisha na hakuna tatizo lolote lililomfanya ahamishiwe kituo kile, ni sababu ipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda nimjibu Mheshimiwa Riziki maswali yake mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hutokea makosa ya kibinaadamu mara kwa mara na pengine makosa ya chapa, lakini ikumbukwe pale ambapo tunapiga kura zetu, sio pale ambapo tumejiandikisha kwa sababu inatakiwa watu wachache iwezekanavyo, watu mia mbili mpaka mia tatu wanatakiwa wawe na kituo cha Kupigia Kura. Kwa hiyo, kituo kimoja cha kuandikishia kinaweza kikawa na maeneo a,b,c hata d kutegemeana na wingi wa watu waliojiandikisha katika kituo hicho ili upigaji kura uweze kukamilika katika muda wa masaa yasiozidi kumi. Hivyo, wananchi itabidi wawe waangalifu kujua wako katika kituo gani cha kupigia kura, katika eneo lile ambalo wamejiandikisha.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mshashu, ukumbi huu kwa kweli dah! Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa haya matatizo yanatokea kipindi cha uchaguzi na kwa kuwa kipindi cha Uchaguzi wanatoa majina kwamba kuhakiki na kweli wanahakiki lakini unakuta majina mengi ya watu waliokufa, majina yanajitokeza. Je, Tume ya Uchaguzi imejipangaje katika uchaguzi mkuu ili wale waliokufa majina yafutwe mapema?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majina ya watu waliofariki huwa yanatolewa taarifa na hasa watendaji wa Kata na pia maafisa tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Wilaya na Hati zile kama ziko zinachukuliwa na kupelekwa Dar es Salaam ili ziweze kuchomwa. Kwa hiyo, inawezekana watu kufariki siku chache kabla ya Uchaguzi Mkuu au Uchaguzi Mdogo hivyo inawezekana majina yale yakijitokeza au baada ya daftari kuhakikiwa. Kwa hiyo, tunalotaka kusema ni kwamba tutajitahidi iwezekanavyo watendaji katika ngazi ya chini tutawaagiza iwezekanavyo ili kupeleka kadi za waliofariki na kuondoa majina yao kwenye Daftari kabla ya Uchaguzi wowote ule, Uchaguzi Mkuu au Uchaguzi Mdogo.

Na. 2

**Wabunge Viti Maalum kupewa Fedha za Mfuko wa**

**Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)**

**MHE. ELIETA N. SWITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inatambua Wabunge wa Viti Maalum kuwa ni sawa na Wabunge wengine wa Majimbo katika utendaji kazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wabunge wa Viti Maalum, fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleleo ya Jimbo *(CDCF)?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ameturudisha tena salama hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Elieta N. Switi, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mwezi Julai, 2009 Bunge lako Tukufu lilipitisha muswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Kuchochoea Maendeleo ya Jimbo (*The Constituencies Development Catalyst Fund).*

Tarehe 21 Agosti, 2009 Mheshimiwa Rais aliidhinisha Muswada huo na kuwa sheria yaani *The Constituencies Development Catalyst Fund Act No. 16 of 2009.*

Madhumuni ya Sheria hiyo ni kuchochea na kuhamasisha Maendeleo katika Majimbo ya Uchaguzi kwa kugharamia utekelezaji wa miradi ambayo imeibuliwa na wananchi katika maeneo yao lakini haikupata fedha katika Bajeti za Halmashauri ambapo Majimbo hayo yamo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria hii, Jimbo lina maana ya Jimbo lililoanzishwa chini ya Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

*"Constituency" means an Electoral Constituency Established by Electoral Commission pursuant to Article 75 of the Constitution".*

Hivyo, Ibara hii ya 75 inazungumzia majimbo ya Uchaguzi yaliyoanzishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya kupata kibali cha Rais.

Kwa msingi huu Wabunge wanaotajwa katika Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ni Wabunge wanowakilisha Majimbo ya Uchaguzi yaliyoanzishwa chini ya Ibara ya 75 na Wabunge hao wawe wamechaguliwa kwa mujibu wa Ibara ya 77 ya Katiba na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria ya Uchaguzi Namba 1 ya mwaka 1985.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elieta N. Switi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali inawatambua Wabunge wa Viti Maalum kuwa ni sawa na Wabunge wengine wa Majimbo katika masuala ya utendaji kazi. Hata hivyo kutokana na madhumuni ya mfuko huu kulenga maendeleo ya Majimbo ya Uchaguzi, Sheria iliyopo sasa haiwajumuishi Wabunge ambao hawawakilishi Majimbo ya Uchaguzi yaliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 75 ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa maelezo haya na kwa kuzingatia masharti ya Sheria iliyopo sasa, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuwapatia Wabunge wa Viti Maalum fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo *(CDCF)* kwa kuwa kufanya hivyo itakuwa tunavunja Sheria iliyoanzisha Mfuko huu.

**MHE. ELIETA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri na nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Serikali yetu imesaini sheria za kimataifa kama *SIDO* na kuridhia Itifaki za *SADC* kama *SADC Gender Protocol* ambazo zote zinakataza ubaguzi na unyanyasaji wa namna yoyote wa kijinsia na kwa kuwa mfuko huu umeshakubalika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza hizi sheria na Itifaki ambazo zimekwisha sainiwa?

(b) Kwa kuwa Serikali inatekeleza ilani yake ya Chama cha Mapinduzi kuwanyima wanawake fedha za mfuko wa maendeleo katika maeneo yao haioneshi kwamba ni kuwanyanyasa?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kuanzia sasa basi inatafuta namna gani na hawa wanawake watawezeshwa kufanya kazi zao vizuri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dada yangu Mheshimiwa Switi kama ifuatavyo:-

Naomba niwe mwangalifu katika swali hili linalozungumzwa hapa na sitaki hapa mimi kukurupuka nionekane kwamba mimi sitambui jitihada ambazo Wabunge wenzetu wa akina mama, katika nchi yetu kwa ajili ya kuleta maendeleo. Ninazijua jitihada za

Serikali za kuwapa fursa akina mama nafasi mbalimbali za nchi hii na sisi sote tunaozungumza hapa ni mashahidi tunajua kabisa kwamba Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, imesimama imara tumepata nafasi ya Wakuu wa Wilaya,Wakuu wa Mikoa, Mawaziri akina mama, wapo hapa, wakina Dr. Asha Rose Migiro, wameondoka hapa wamekwenda *United Nations* wametokea humu humu. Kwa hiyo, jitihada za Serikali hapa zinaonekana. *(Makofi)*

Ninataka nikiri mbele yako kwamba sisi tunatambua kabisa jitihada za Wabunge wanawake ambazo zinasaidia katika harakati za kumkomboa Mtanzania, tunazitambua. Ninachosema hapa ni kwamba sheria inasema nini? Sheria inasema kwamba Mbunge atakapopewa *Constituencies Development Catalyst Fund* ni Mbunge anayetoka katika Jimbo la Uchaguzi, *that is the bottom line* na huyu Mzee amekaa hapa ananiangalia nikitamka hapa kwamba Serikali ina mpango wa kuja hapa na kuleta hela kwa ajili ya Wabunge wa Viti Maalum, ataniuliza umepata wapi hii habari?

Jamani mimi nitafanya nini? Pili anazungumzia kuhusu ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ni kweli imetamka hapa, hapa tunazungumza habari ya sheria mwanafunzi wa sheria aliwahi kuuliza *what is law*? Akasema *law is simple common sense,* hapa ukiangalia inavyosema sheria hapa inakuambia kwamba huwezi kusema *Attorney General* ananiangalia siwezi kusema maneno mengi, ninachoweza kushauri hapa kama kuna mjadala tunataka kuuleta katika nchi hii kuhusu Wabunge wa Viti Maalum kuwa tuwaanzishie utaratibu kama tulioupitisha hapa juzi ili tuweze ku-*consider* pia eneo hili Mheshimiwa Switi analozungumza hapo.

Mheshimwa Spika, hayo ndiyo ambayo naweza nikayasema hapa kwa hiyo, ikija kwa utaratibu huo nina hakiki Serikali hii ni sikivu na itasikiliza na itafanya hivyo kama inavyotakwa lakini kwa sheria hii itakuwa ni vigumu kukubaliana na jambo hili ambalo anazungumza Mheshimiwa Switi. (*Makofi /Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelezo ya ziada.

**WAZIRI MKUU:** Naomba baada ya maelezo mazuri ya Ndugu Mwanri, nijaribu kusaidia kidogo juu ya jambo hili.

Jambo hili lilizungumzwa kwa kirefu zaidi kwanza kwenye *Cabinet* lakini hata hapa Bungeni kulikukwa na mjadala mkubwa tu kubwa hapa fedha hizi si za Mbunge hapana, fedha hizi ni fedha za Serikali zinapelekwa kwenye maeneo kwa ajili ya kuchochea shughuli za maendeleo. Walengwa ni wananchi wote waliomo katika maeneo ambayo sheria hii imetambua awe mwanaume awe mwanamke.

Miradi tunayokwenda kuishungulikia chini ya mfuko huu itahusu miradi ambayo ipo lakini inahitaji kupewa msukumo kwa jamii ambayo ndiyo tunawaomba sana wachangie. Kwa hiyo, kama ni bati vitakwenda kujenga shule kama ni kisima kitakwenda kuchimbwa kama ni barabara itatengenezwa watumiaji ni wananchi katika eneo hilo.

Kwa hiyo, tusije tukachukulia hili neno *Constituency* likaonekana kama vile ni Ubaguzi ni kwa maana tu kutaka kuonesha kwamba fedha hizi zitajikita zaidi katika eneo ambalo linaitwa Jimbo. Lakini kwa jamii iliyomo ndani ya Jimbo bila kujali jinsia kwa maana ya ubaguzi. Kwa hiyo, mimi nadhani tukielewana hivi nadhani halina tatizo hata kidogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu baada ya ufafanuzi huo tunaendelea na swali linalofuata nalo linaulizwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge wa Gairo.

Na. 3

**Kukarabati Barabara ya Gairo Iyogwe**

**MHE. AHMED MABKHUT SHABIBY** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, barabara ya Gairo-Iyogwe inaunganisha Mikoa mitatu na Wilaya tatu na kutokana na umuhimu wake Mheshimiwa Rais wakati wa ziara yake Jimboni Gairo aliamuru iwe chini ya *TANROADS;* na kwa kuwa, mafuriko ya mwaka huu yameharibu sana barabara hiyo, kiasi cha kushindwa kupitika:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani za haraka kuhakikisha barabara hiyo inapatikana?

(b) Je, mpaka sasa kuna hatua gani za dharura zilizochukuliwa ili wananchi hao wapate huduma kama hospitali na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mbunge wa Gairo, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ngiloli-Iyongwe ina urefu wa kilomita 42 na imekuwa ikifanyiwa matengenezo na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais katika Jimbo la Gairo aliagiza barabara hii ipandishwe daraja na kuwa chini ya wakala wa barabara *TANROADS* kwa kuwa barabara hiyo inaunganisha mikoa miwili ya Morogoro na Tanga.

Mkoa wa Morogoro ulipata nakala ya barua aliyoandikiwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Ikulu ya tarehe 27 Agosti 2009. Baada ya kupata maelekezo ya Mheshimiwa Rais,Mkoa wa Morogoro umewasiliana na Wizara hiyo na kupewa taarifa kwamba maagizo hayo bado yanafanyiwa kazi.

Barabara hii ilifanyiwa matengenezo ya muda maalaum (*Periodic Maintenance*) kilomita 9 mwaka wa fedha 2006/2007 kwa jumla ya shilingi 72 milioni ikiwa ni pamoja na kuweka makalvati mistari miwili na kuinua tuta sehemu za Nguyami.

Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 jumla ya kilomita 25 zilichongwa kwa jumla ya shilingi 13.3 milioni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, wakati wa kipindi cha mafuriko,Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa haikuwa na fedha za tahadhari za kuweza kukabiliana na matatizo yaliyotokea. Badala yake Halmashauri ilituma maombi ya fedha za dharura OWM-TAMISEMI kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo yenye thamani ya shilingi milioni 323.4.

Baada ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupokea maombi haya, yaliyounganishwa na maombi ya sehemu nyingine na kuyawasilisha Wizara ya Fedha na Uchumi,ufuatiliaji bado unaendelea kufanyika ili kuona uwezekano wa kupata fedha hizo ili kutengeneza barabara hiyo iweze kupitika kama ilivyokuwa mwanzoni.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge waliweza kufanya matengenezo ya sehemu iliyokuwa korofi zaidi kama kwenye tuta la Nguyami na *drift* la Chakwale ili barabara hiyo iweze kupitika wakati ikisubiri kufanyiwa matengenezo makubwa wakati Halmashauri hii itakapopata fedha ilizoomba.

Kwa wakati huu barabara hii inapitika na wananchi wanapata huduma mbalimbali kama vile za hospitalu, mashule na kadhalika.

**MHE. AHMED MABKHUT SHABIBY:** (a) Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini barabara hii ya Yogengelori si tu inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga vile vile inaunganisha vijiji ishirini na kata mbili za Jimbo la Gairo na kwa vile amezungumza kwamba zilitumika shilingi milion 72 kwa ajili ya kutengeneza tuta pamoja na makaravati.

Je, anayohabari kwamba hilo tuta halipo wala hayo makaravati hayapo?

(b) Kwa kuwa amekiri kwamba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake walijitahidi kuitengeneza hiyo barabara ili ipitike na kwa vile walifanya tathimini wakati wa mvua zikiwa zinaendelea.

Je, anayo habari kwamba sasa hivi hayo madaraja hayapo kabisa na wananchi na Mbunge hawana hela tena za kutengeneza hiyo barabara na sasa hivi inahitajika juhudi za makusudi ili barabara hiyo ipitike?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri

Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shabiby, kama ifuatavyo:-

Labda nieleze kwanza kidogo hapa na nimekuja na *file* lote zima kwa sababu nilijua hapa kutakuwa na kiti moto. Kwa hiyo, nina kila kitu na *documents* zote ninazo hapa.

Mheshimiwa Spika, hili la Mheshimiwa Mbunge la kwamba amefanya kazi amekwenda akaenda akahamasisha zaidi wanachi, Wizara yetu imekwenda mpaka kule tumekuta Mheshimiwa Shabiby badala ya kuisubiria Serikali yeye mwenyewe amewaita wanachi wakaenda wakatengeneza ile barabara wakaifanyia kazi kwenye *drift* hiyo na wakahakikisha kwamba na tuta linanyanyuliwa pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa niaba ya Serikali naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Shabiby kwa kazi nzuri ambayo amefanya sana kwa sababu fedha hazikupelekwa pale kama alivyosema Mheshimiwa.

Lakini ameonyesha mfano mzuri wa kuigwa na sisi Wabunge wengine wote tunatakiwa tuige mfano wa ndugu yetu Shabiby kama alivyofanya.

Sasa mimi siwezi kubishana na Shabiby, Shabiby anatokea Gairo, mimi natokea Siha. Nimetoka Dar es Salaam nimekuja hapa, siwezi kuanza kubishana na yeye hapa nianze kusema kwamba tuta liko na kumbe yeye ameshaona kwamba tuta halipo.

Lakini niseme maelekezo ya Rais yalitekelezwa. Hii barua niliyo nayo hapa inatoka kwa Mrema ambaye ndiye *CEO* wa Tanroads anamwandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Waziri yuko hapa.

Barabara hii ambayo anaizungumzia ambayo Mheshimiwa Rais alielekeza kwamba apelekwe *Tanroads i*meombewa shilingi milioni 461,383.00. Halafu barabara zote hizi wakija kuziunganisha jumla ni bilioni 2,430,683,000/=.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, ilipotokea hali hii sisi hapa tuna-*operate* kwa kutumia kitu kinachoitwa *Cash Budget.* Lilipotokea hili tatizo hela hizi zikaombwa Serikalini na zikaunganishwa na hela nyingine ambazo zilikuwa zimeombwa kwa maeneo mengine ambayo yalipata mafuriko. Matokeo yake sasa ni kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi imetuambia kwamba inaendelea kutafuta hizi hela, ndicho kilitokea hapa.

Kwa hiyo, kazi hii imefanyika na maelekezo ya Rais yamefanyiwa kazi na barua ninazo hapa mkitaka nitazitoa. Lakini hakuna lingine ambalo tungeweza kufanya. Sisi tunachofanya hapa kama Wizara sasa hivi ni kufuatilia zaidi na zaidi kuona kwamba tunalitoa jimbo lile la Gairo na Wilaya ile ya Kilosa katika hali hiyo ambayo ameizunguma hapa. Ningependa nijibu yote mawili kwa pamoja hivyo Mheshimiwa Spika.

Na. 4

**Ujenzi wa Barabara ya Nzega-Tabora**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya usafiri wa reli na barabara kati ya Tabora na Mikoa mingine nchini hairidhishi kiasi cha kuathiri sana hali ya maendeleo mkoani humo:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Nzega-Tabora utaanza ili kufika Tabora kwa urahisi kwa kutumia barabara kuu ya Mwanza-Dar es Salaa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Tabora hadi Nzega yenye urefu wa kilometa 116 kwa kiwango cha lami umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. *(Makofi)*

Jumla ya shilingi bilioni 5, 635,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Zabuni kwa ajili ya kazi hizi zimetangazwa tarehe *31 March, 2010* na ni matarajio yangu kuwa Mkandarasi atakuwa amepatikana kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha wa 2009/2010.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuishukuru Serikali au kuipongeza Serikali kwa mchakato uliofikiwa wa ujenzi wa barabara ya Nzega/Tabora. Maswali mawili ya nyongeza:-

La kwanza kusema kweli ni rai. Ningeiomba Serikali watakapokuwa wanatoa hii zabuni mkandarasi apewe sharti la kuanza kuijenga barabara hii kutokea Tabora kwenda Nzega. Hiyo ni rai. *(Kicheko)*

Swali la pili, ni kwamba katika swali langu la msingi Mheshimiwa Spika, nimegusia kwamba tuna matatizo ya reli vile vile kwa maana ya usafiri baina ya Tabora na sehemu nyingine za nchi yetu. Naiomba Serikali itupe kauli ni lini safari za abiria kwa treni zitaanzia Dodoma kwenda Tabora, Mwanza na Kigoma?

**SPIKA:** Hilo la pili ni swali jipya halihusiani na swali la kwanza. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ajibu lile la kwanza.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kaboyonga. Kuhusu eneo la kuanzia eneo la ujenzi wa barabara hii ya Tabora na Nzega. Rai tumesikia, tumeipokea, tutayazungumza na wadau

wote wa barabara hiyo, lile ambalo litakuwa limekubalika na wadau wahusika basi ndiyo hilo ambalo tutalifanya. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Bwana Spika. Na mimi nachukua nafasi hii kuipongea Serikali kwa jinsi ambavyo imeanza mchakato wa kuikamilisha hii barabara. Nina swali dogo kwamba barabara hii ni mwendelezo wa barabara inayotoka Mwanza, Nzega, Tabora, Sikonge, Ipole kwenda Mpanda, Ipole kwenda Mbeya. Je, kwa kuanza barabara kutoka Nzega mpaka Tabora yapo matumaini maendelezo wa barabara hii utaelekea pia kwenda Sikonge mpaka Mpanda, Sikonge mpaka Mbeya haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba barabara hiyo pia inategemewa kuendelea hadi katika mikoa ya Rukwa na Mbeya. Sasa kwa barabara ya Tabora-Ipole-Mpanda tayari mtaalam mshauri amepatikana kwa ajili ya kufanya upembezi pamoja na usanifu wa barabara hiyo, amepewa mkataba wa miezi 20 na yupo kazini mkataba huu ulikuwa umeanza tarehe 8 Juni, 2009. Nategemea kwamba ndani ya miezi 20 usanifu wa barabara hiyo kuanzia Tabora-Ipole hadi Mpanda nao utakuwa umekamilika.

Sasa kipande kingine ni kuanzia Ipole hadi Rungwa kuingia kwenye Mkoa wa Mbeya. Kazi hii ya usanifu wa barabara hii tumeipangia kuweka kwenye mchakato wa Bajeti ya mwaka mpya wa fedha 2010/2011. Kwa hiyo, tutatenga pesa katika mwaka mpya wa fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa barabara hiyo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, swali la msingi lilikuwa linaulizia kuhusu usafiri wa kutoridhisha wa reli na barabara kwa mikoa ya magharibi na sasa tatizo lililopo hapa ni kwamba sasa hivi watu wa Kigomba usafiri ni wa tabu sana. Kwa sababu hawawezi kutumia barabara kwa sababu barabara ya kuja Tabora haipitiki na vile hawawezi kutumia reli kwa sababu treni hazifiki Kigoma. Kwa hiyo nilikuwa naomba kwa ruhusa yako Waziri wa Miundombinu aeleze adha hii ya usafiri wa reli kwa watu wa Kigoma inakwisha lini?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nilishalikataa swali hili ambalo naomba liulizwe mahsusi. Kwa hiyo, siwezi kuliruhusu kwa mazingira haya. Ingawa kuna maneno pale yanasema, ndiyo lakini hii siyo sehemu yake, hili halikuandikwa vizuri. Maana yake swali lenyewe ni *paragraph (b).* Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Nzega-Tabora utaanza ili kufika Tabora kwa urahisi kwa kutumia barabara kuu ya Mwanza. Hilo ndiyo swali. Haya maelezo huwa mnajiwekea sijui hivi na hivi. Kwa tafsiri ya Kiti haihusiani kabisa na swali. Huwezi kuwa unataka kuuliza swali la barabara halafu ukaanza utangulizi maswali ya reli na meli Ziwa Victoria na meli Ziwa Tanganyika haiwezi kusaidia. Kwa hiyo, tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Kicheko)*

Na. 5

**Mapato yatokanayo na Shughuli za Uwindaji**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ni miongoni mwa Halmashauri zenye shughuli za uwindaji wa kitalii na kwa kuwa Serikali ilipojibu swali la nyongeza kwa swali la msingi Na. 133 katika Mkutano wa 18 wa Bunge ilikiri kuwa katika mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ni miongoni mwa Halmashauri ambazo hazikupata gawio la asilimia 25 ya mapato yatokanayo na shughuli za utalii:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, utaratibu wa mapato hayo kufanyikia Hazina unaumiza Halmashauri husika?

(b) Je, Serikali iko tayari kuanzisha utaratibu wa kutoa riba yenye tija kwa Halmashauri husika pale inapotokea ucheleweshwaji kwa ajili ya fidia?

(c) Je, Serikali iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kufanya uchunguzi wa kina juu ya uwiano wa hali halisi kwenye Hifadhi ya Buridi ikilinganishwa na kiasi cha Shs.12,000,000/= cha makusanyo katika Hifadhi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, (a)Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ni moja kati ya Wilaya 44 zenye maeneo ya uwindaji wa kitalii na ambazo zinastahili kunufaika na mgao wa fedha za asilimia 25 kutokana na shughuli za uwindaji wa kitalii. Mgao wa asilimia 25 hutokana na sehemu ya fedha inayopelekwa Hazina kutokana na ada za wanyamapori waliowindwa katika vitalu vilivyopo katika maeneo ya Wilaya husika.

Mfumo wa ukusanyaji na utumiaji wa fedha za Serikali (maduhuli) kwa Wizara na Idara (yaani, *Exchequer System)* unaelekeza kuwa fedha zote zinazokusanywa lazima ziingie kwenye mfuko mkuu wa Hazina na baadaye kutumika kwa idhini ya Bunge kupitia Bajeti za Wizara, Idara na Halmashauri. Na hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 135 ya Katiba ya nchi na Sheria ya Fedha za umma ya mwaka 2001 Kifungu Namba 11. Ni kweli kumekuwepo mapungufu na malalamiko kuhusu mfuno huu yakiwemo ucheleweshaji na ugumu wa usuluhisho *(reconciliation)*. Lakini kwa ujumla mfumo unaonekana kufaa sana hasa katika kuimarisha udhibiti. Hata hivyo, Wizara yangu ilishaanza kujadiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kupata namna bora zaidi ya kukusanya na kupeleka fedha kwenye Halmashauri ambako uwindaji unafanyika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilipata jumla ya Shs. 1,625,572.80 kama gawio la asilimia 25 ya mapato yatokanayo na shughuli za uwindaji wa kitalii kwa msimu wa uwindaji wa mwaka 2007. Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, Halmashauri za Wilaya zote ambazo zinastahili kupata mgao huo hazikuweza kupatiwa fedha kutokana na ufinyu wa Bajeti uliojitokeza kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, (a) Kama nilivyotangulia kusema awali, utaratibu wa mgao wa asilimia 25 kwa Halmashauri zinazonufaika na shughuli za uwindaji wa kitalii hautekelezwi kwa wakati kutokana na ufinyu wa Bajeti mara zingine unaojitokeza katika mfumo mzima wa Serikali. Pamoja na ucheleweshwaji wa malipo haya, Serikali haina mpango wa kulipa riba kwa kuwa ucheleweshwaji huu si wa makusudi. *(Makofi)*

(b) Hata hivyo, kama nilivyokwishaahidi katika mkutano wa 18 wa Bunge lako Tukufu, Wizara ya Fedha na Uchumi inaendelea na mchakato ili kuwezesha Halmashauri za Wilaya stahili ambazo zilikosa mgao wa fedha kati ya mwaka 2008/2009 kulipwa malimbikizo yaani *arrears* ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, (c) Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ina maeneo mawili yaani (vitalu) yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za uwindaji wa kitalii. Vitalu hivyo ni Buridi *Game Reserve (East)* na *Biharamulo Game Reserve.* Kitalu cha *Biharamulo Game Reserve* kwa sasa hakitumiki kwa shughuli za uwindaji wa kitalii kwa kuwa kina idadi ndogo ya wanyamapori ambao hawatoshelezi kuwindwa kibiashara.

Katika msimu wa uwindaji wa kitalii wa mwaka 2008, jumla ya wanyamapori 54 waliwindwa katika kitalu cha *Buridi Game Reserve (East).* Hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilistahili kupata shilingi milioni 3,794,256 kama mgao wa fedha yaani asilimia 25 iliyopelekwa Hazina kutokana na adha za wanyamapori waliowawinda katika kitalu hicho. Aidha kwa mwaka 2009 jumla ya wanyamapori 34 waliwindwa na kuwezesha Halmashauri kupata jumla ya shilingi 2,880,067.78.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo yangu ya msingi, Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo katika kuangalia uwiano wa mgawanyo wa mapato, na kuelimishana zaidi kuhusu utaratibu nzima wa mgao wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri za Wilaya.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Lakini nina mambo mawili ya nyongeza. Kutokana na maelezo ya Naibu Waziri kuna mahala ambapo Serikali inasisitiza kwamba mgao wa mwaka 2007/2008 haukupatikana kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Lakini kutokana na maelezo ya awali yaliyotangulia pale yanasema kwamba mgao wa asiliamia 25 ni mgao unaokwenda pale kutokana na makubaliano kwamba mapato ya pale ya asilimia 25 yanabaki pale. Sasa inakuwa haieleweki vizuri pale suala la ufinyu wa bajeti unatoka wapi?

Lakini pili, naishukuru Serikali kwa kuwa tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Biaharamulo kufanya ufuatiliaji wa mapato yanayopatikana pale. Kwa sisi ambao tunapita pale mara kwa mara. Shughuli zinazoendelea pale tunazozishuhudia, kwa kweli hatuwezi kuwa na imani kabisa kwamba idadi ya wanyama wanaowindwa kwa mwaka ni wanyama kidogo kiasi hicho. Kwa hiyo, tungeomba kuweka msisitizo kwamba tukae na Halmashauri na Wizara tuone ni namna gani suala hilo linakwisha.

**SPIKA:** La pili ni ombi. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Katiba ya nchi inaelekeza katika Ibara ya 135 kwamba fedha zote zinazokusanywa za Serikali zinakwenda Hazina na baada ya hapo zinakuja kugawanywa kwa mujibu wa Bajeti ambayo inakuwa imepitishwa. Sasa bajeti inapokuwa imepitishwa utoaji wa fedha hizi inategemea na makusanyo kama ambavyo tunajua kwamba tunatoa fedha kutokana na makusanyo yaani tuna-*operate Cash Budget.*

Kwa hiyo, mara nyingine, uwindaji unakuwa umefanyika lakini *process* ya kuzikusanya na kuzipeleka Hazina na kuja kuzirudisha kidogo inachukua muda. Kwa hiyo, nilitaka tu nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba *process* iliyoko ndiyo hiyo na ugumu wake ni kwamba haiwezekani kwa sasa kuziacha pale pale kwa sababu uataratibu unasema zipelekwe Hazina halafu baadaye ndiyo ziweze kurejeshwa. Lakini kama ambavyo nimekuja kusema tunaendelea kuzungumza na wenzetu wa Hazina na hata sisi kimsingi tuna-*admit* kwamba *concern* hiyo ni *serious* na tunapenda sana kupata njia nzuri zaidi na fedha nyingi zaidi ziweze kwenda kwenye Halmashauri lakini kwa sasa utaratibu bado haujaturuhusu.

Na. 6

**Kupeleka Umeme katika vijiji vya Jimbo la Karagwe**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES)** aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo mwaka 2006, Serikali iliahidi kupeleka umeme katika vijiji vya Ihanda, Rukole, Kamagambo, Kiruruma, Nyakagoyagoye na Nyabiyonza na kwa kuwa mradi wa Kanyangaa, Rukaka, Ndama, Kituntu, hadi Rwambaizi umenazan kwa kusimika nguzo tu, na kwa kuwa katika Bajeti ya m waka 2009/2010 Bunge liliidhinisha fedha kwa ajili ya kupeleka umeme vijiji vya Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi, Ibembe 1 na Ihembe II na mpaka sasa bado umeme haujapelekwa.

Je, ni lini umeme utapelekwa katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Serikali iliahidi hapa Bungeni wakati wa kujibu swali namba 12 tarehe 28 Machi, 2006 kuwa itapeleka umeme maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Aidha wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge mwaka jana tarehe 28 Julai, 2009 kuhusu upelekaji umeme katika maeneo ya vijiji hivyo hivyo, ilielezwa kuwa vijiji hivi vimeombewa fedha kutoka Wakala wa Nishati Vijijini *REA.*

Miradi ya kupeleka umeme kwenye vijiji vya Ihanda, Rukole, Kamagambo, Kiruruma, Nyakagoyagoye na Nyabiyonza ni mojawapo ya miradi iliyoombewa fedha za utekelezaji kutoka kwa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* mwaka 2008. Kutokana na ufinyu wa Bajeti, miradi iliyopata ufadhili wa utekelezaji kutoka *REA* kutoka Wilaya ya Karagwe ni ya kupeleka umeme kwenye vijiji vya Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi, pamoja na Ihembe I na Ihembe II. Ujenzi wa njia za umeme kwenye vijiji vilivyopata ufadhili kutoka *REA* unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2010 na utafanywa na Mkandarasi aliyeshinda zabuni *(Mufindi Service Ltd).* Tunawaomba wananchi wa maeneo yaliyobaki ya Wilaya ya Karagwe wawe na subira wakati Serikali inatafuta fedha za utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuvipatia umeme vijiji vya Kanyanga, Rukaka, Ndama, Kituntu, hadi Rwambaizi unatekelezwa na *TANESCO* na tayari nguzo zimekwishasimamishwa. Katika Bajeti ya shirika ya mwaka 2010, mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi 225,539,575.00 kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa niaba ya Mheshimiwa Blandes, naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza. La kwanza. Kwa kuwa Mheshimiwa Blandes amejitahidi sana kupiga kelele hapa Bungeni na wananchi wake huwa wanamsikia, na kwa kuwa Serikali fedha iliyopata kupeleka umeme katika vijiji nilivyovitaja imepata kiasi tu kipitia mradi wa umeme vijijini na kwa kuwa sasa Serikali inandaa Bajeti ya mwaka 2010/2011. Je, itamhakikishia Mheshimiwa Blandes kwamba kupitia Bajeti hiyo sasa watakumbuka vijiji vilivyosalia kukamilisha kupeleka umeme huko?

Kwa kuwa matatizo ya umeme yanafanana karibu nchi nzima na kwa kuwa Serikali tayari ilishaahidi hapa kupeleka umeme Wilaya ya Manyoni, vijiji vya Kilimatinde, Ferya, Supamaheya, Chikuyu, Kintinku na kwa kuwa Mheshimiwa Chiligati ametuomba sana kumsemea hili kwa niaba ya wananchi wake na Serikali ilifaulu kutenga fedha kwa kilometa 7 tu na vijiji vingine vyote havikupatiwa. Je, kupitia Bajeti inayokuja vijiji vilivyobakia nilivyovitaja vitapatiwa hizo fedha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Lengo lilikuwa ni lile la pili, siyo lile la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataraji huruma yako katika lile la pili. *(Kicheko)*

Hili la Mheshimiwa Blandes nakubaliana naye Mheshimiwa Chilolo kwamba siyo tu amekuwa akilizungumzia mara mbili, keshaliulizia mara mbili hapa Bungeni mwaka 2006, Machi na hii ingekuwa mara ya tatu na tatizo la umeme wa Nyaishozi na maeneo ya pale ni kwamba pana mambo mawili kwanza pale umeme ambao unapatina sasa hivi ni umeme ambao unatokana na gridi ya Uganda.

Kwa hiyo, kazi kubwa inayofanywa sasa hivi ni kwamba sisi na watu wa Serikali ya Uganda tuko kwenye mazungumzo ya kuboresha upatikanaji wa umeme katika Kanda yote ile kupitia mradi wa Mronga-Kikadati.

Ni mradi ambao umeingia hiana kidogo kwa sababu kuna mambo mawili, matatu ambayo hayajamalizika. Lakini Serikali ya Uganda imeonyesha nia ya kujadiliana na sisi kuhusu jambo hili na pamoja na kusambaza umeme vijiji vyote hivi kitu cha kwanza lazima huo umeme wenyewe uwepo.

Kwa hiyo, nadhani kitu kikubwa hapa napenda nimhakikishie Mheshimiwa Chilolo kwa niaba ya Mheshimiwa Blandes kwamba umeme tunafanyia kazi suala la upatikanaji umeme kupitia mradi huo wa Mrongo/Kikagati na kulingana na upatikanaji huo wa umeme na upatikanaji wa fedha ndani ya Bajeti yetu ya Serikali na naomba nimhakikishie Mheshimiwa kwamba umeme huo utakwenda kwenye vijiji hivi kama tulivyoahidi kwa sababu ni ahadi tangu 2005 wakati wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili hili la Manyoni Vijijini, mazingira anasema yanafanana. Yanafanana kidogo, lakini pia hayafanani sana.

Lakini pia naomba nimhakikishie Mheshimiwa Chilolo kwamba kupeleka umeme Manyoni kwa ujumla mimi mwenyewe nimekwenda mwaka jana mwezi wa 10, nimezungumza na *TANESCO*, tumezungumza na viongozi wa Wilaya ya Manyoni, lakini siyo hivyo tu tunarajia pia kwenda mwisho wa mwezi huu na ni suala ambalo tunalifuatilia kwa karibu kwa sababu tatizo lililokuwepo pale ni kwamba umeme unaopita pale unaotokana na gridi ni mdogo, lakini *transmission line* iliyokuja sasa hivi kutoka Iringa inahakikisha upatikanaji wa umeme mwingi zaidi.

Kwa hiyo, kazi iliyokuwepo hapa sasa hivi kusema kweli ni kuboresha tu ule mtandao wa kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo ambavyo tayari imeshakubaliwa lakini kazi yenyewe ni kubwa kwa sababu maeneo yako mbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo haya yanafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Kwa kuwa swali la msingi linafanana fanana sana na mahitaji ya umeme katika jimbo, umeme kwenda Bukene na umeme kutoka Nzega kwenda Ndala na kwa kuwa hii ahadi ya ni ya siku nyingi tangu awamu ya tatu na vile vile iko katika umeme vijijini na tenda imefunguliwa. Je, Waziri atatuambia lini yule aliyepewa tenda na atafanya kazi kuanzia lini kupitisha umeme Bukene kutoka Nzega na kutoka Nzega kupitisha umeme kwenda Ndala? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, miradi anayozungumzia Mheshimiwa Kasella-Bantu, pana miradi pale ya umeme moja ambayo ni hii inayotokea Nzega kuja huku. Lakini na nyingine ambayo inatokea maeneo ya Uyui. Sasa pale Uyui palikuwa kwanza kabisa Makao Makuu ya Wilaya palikuwa na mradi wa kufikisha umeme chini ya ule mpango wa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ile Tayari imeshakamilika. *(Makofi)*

Na ikitoka pale Mheshimiwa Spika, inakwenda mbele zaidi. Naomba samahani kidogo kwa sababu hayo siwezi kuyakumbuka vizuri. Lakini ninajua kwamba pale pana ka-*inter connection* fulani ambako kana-*involve* kupeleka umeme Ngala na Puge kwa Mheshimiwa Selelii na pia kuvuka kwenda Bukene kwa Mheshimiwa Kasella-Bantu. Lakini yote kuanzia huku Nzega kuja huku chini mpaka kuja Uyui.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba utekelezaji wa miradi hii ni jambo ambalo tayari limeshafanyiwa kazi kitaalam na linasubiri upatikanaji wa fedha.

Suala la upatikanaji wa fedha limekuwa gumu kidogo. Kwa sababu kwa miradi iliyokuwa *TANESCCO* kuna maswala ya upatikanaji wa fedha na yale ya *REA* nayo yana matatizo.

Kwa hiyo, tunasubiri tunavyowasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Uchumi kadri wao wanavyokuwa katika hali nzuri zaidi na sisi ndiyo tunapata uwezo wa kupeleka pesa *REA* na *REA* na kuwasiliana na *TANESCO.*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba siyo kwamba miradi haijafanyiwa kazi, hapana. Tumeshafikia hatua ambayo miradi imeshafanyiwa kazi *design* imeshachora lakini inabaki kwenye masuala ya *financing* ya upatikanaji wa fedha zikipatikana kwa sababu miradi tayari imeshachorwa, namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na utekelezaji wa miradi hiyo kama ilivyopangwa awali. Hakuna kinachobadilika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado tuko katika Wizara hiyo hiyo kwa swali linalofuata. Ila ningeomba tu kwamba kabla halijaulizwa nimepata taarifa mbili hapa kwamba Ukumbi huu una baridi sana. Kwa hiyo, naomba watu wa Idara ya Ufundi waweze kufanya marekebisho yanayopaswa wasiongeze ikawa joto kupita kiasi, lakini wapunguze baridi.

Na. 7

**Kupeleka Umeme Jimbo la Buchosa**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. SAMUEL M. CHITALILO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekwishaahidi kupeleka umeme katika jimbo la Buchosa kupitia katika Kata za Nyanzenda Luchili, Nyakasungwa, Nyakarilo Bukokwa, Kalebezo, Kazunzu, Nyehunge, Kafunzo, Bupandwamhela, Katwe hadi Kahunde?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samueli Mchele Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji katika jimbo la Buchosa vya Luchili, Nyakasungwa, Nyakarilo-Bukokwa, Kalebezo, Kazunzu, Nyehunge, Kafunzo, Bupandwamhela, Katwe hadi Kahunde vitapatiwa umeme chini ya mradi wa *MCC* unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani.

Sehemu mojawapo ya mradi huo katika Sekta ya Nishati ni upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kusambaza umeme katika mikoa 6 ya Tanzania.

Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa mpaka sasa ni kukamilisha kwa upimaji wa njia za umeme, zabuni zimetangazwa mwezi *Machi,* 2010 na zitafunguliwa mwezi Juni, 2010, zabuni ya ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme *(Sub Stations)* zitafunguliwa tarehe 30 Aprili, 2010, Taarifa kamili za uthamini wa mikoa ya Morogoro, Tanga, Iringa, Mbeya, Mwanza na Dodoma imekamilika na kuwasilishwa *MCA – T.*

Katika Jimbo la Buchosa, mradi huu wa *MCC* utahusisha ujenzi wa kilometa 189 za njia ya umeme, msongo wa kilovolti 33 na kilometa 19.5 za njia ya umeme msongo wa kilovolti 0.4 pamoja na ufungaji wa *transformer* 19. Hatua zilizofikiwa ni pamoja na utangazaji wa zabuni kwa umma mwezi Machi, 2010 ili kupata Mkandarasi wa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yatakayonufaika na mradi huo katika maeneo ya Wilaya hiyo ya Sengerema, ni maeneo yote kutoka Sengerema mjini, Ibondo, Nyamililo, Nyamtelela, Katunguru, Kasomeko, Chaabanda, Igalabalilo, Nyamatongo, Karumo, Igongo, Pamanda hadi Chifumfu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, ametupa matumaini ya mradi wa Wamarekani ambao ndio watahudumia sehemu hizo, cha kusikitisha ni kwamba sasa hivi tumebakiza miezi tu. Na ananiambia kwamba watachukua miezi mitatu kufungua zabuni. Je, hamwoni Jimbo hili la Buchosa hamlitendei haki kwa kutumia muda mrefu kufungua tu zabuni na hali mukijua kwamba tunaelekea kwenye Uchaguzi? *(Kicheko).*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Nyawazwa kwamba utaratibu unaotumika wa kuanza kwa Mkandarasi Muelekezi, mpaka kwa nani, mpaka kwa mzabuni, mpaka kwa nani, ni utaratibu ambao unachukua muda mrefu mno. Lakini ndio utaratibua ambao tumejiwekea kisheria na umeidhinishwa ndani ya Bunge hili. Utaratibu wa manunuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninaamini kwamba ingeweza kufanywa tofauti. Kwa sababu ahadi ya kwanza ya mradi huu na ninaomba niliseme hili kwa miradi yote ya *MCC,* tumekuwa tunaizungumzia miradi hii na tulikuwa tunatarajia kwamba tungepata utekelezaji tangu mwezi wa 10 au 11 mwaka jana. Lakini hizi taratibu za *procurement*

na nini, ambazo tumejiwekea ili kuhakikisha kwamba mambo yanakuwa mazuri zaidi lakini pia yanachukua muda mrefu. Sasa Mheshimiwa Nyawazwa anasema labda hatuwatendei haki wakazi wa Buchosa. Sio Buchosa tu, kuna mikoa mingine sita na wilaya zingine chungu nzima ambazo nazo zimekumbwa na ucheleweshaji huu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani kwamba kama ni jambo la ucheleweshaji wa masuala ya *procurement* na nini, hilo limo katika mfumo mkubwa zaidi wa kufanyiwa kazi na Bunge hili ili tupate ufanisi wa mfumo mzima wa utekelezaji wa miradi na manunuzi ndani ya Serikali. *(Makofi).*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Kwa kuwa iko miradi mingi ya usambazaji katika nchi, nzima ambayo imekaa takribani miaka 10 haijatekelezwa. Ukiwepo mradi wa Iduda wa kupeleka umeme pale Mbeya, Iganjo pamoja na Inyala, Kata ya Iyunga. Isingekuwa vema kwa Serikali, kwanza kumalizia miradi hii ambayo imekaa muda mrefu, kwanza kabla ya kuanza miradi mingine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii miradi ya usambazaji ambayo nilikuwa nimeitajwa kwenye swali la msingi, ni miradi ambayo *specifically* ni miradi ya *MCC* ambayo ni miradi kwa mikoa sita. Sasa katika utaratibu huu kweli *MCC* imeanza 2008 na iko miradi ambayo iko nyuma yake ambayo haijapata utekelezaji kwa sababu moja au nyingine. Na miradi ya Mbeya pale, iko mingine kwa Mheshimiwa Lackson Mwanjale ambayo nayo imechelewa na ina umri kama huo wa miaka nane, tisa. Nakubaliana na Mheshimiwa Mpesya kwamba ni vema kabla hatujaingia kwenye miradi mipya tukaangalia ile ya zamani ambayo tumekuwa tunafanya na ndio maana tumepata utekelezaji wa miradi kule kwa Mheshimiwa Lackson Mwanjale. Lakini naomba tu niseme kwamba hili tutalizingatia Wizarani, na pia liko katika upande mwingine wa utekelezaji wa miradi ya zamani na sio hii ya *MCC* ambayo imepata ucheleweshaji kwa sababu nyingine.

Na. 8

**Serikali Kusaidia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo Kikuu cha Tanzania kinatoa huduma ya elimu ya juu kwa gharama nafuu, ikilinganisha na vyuo vingine vya umma:-

(a) Je, Serikali inakisaidiaje chuo hicho ili kiwezi kutekeleza majukumu yake ipasavyo?

(b) Je, chuo hicho kinakabiliwa na changamoto zipi katika utendaji wake wa kazi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ni mojawapo ya Vyuo Vikuu vya Umma, Chuo hiki huendesha shughuli zake kwa ruzuku ya Serikali. Serikali inakisaidia Chuo Kikuu Huria katika nyanja kuu zifuatazo:-

(i) Serikali hulipa mishahara ya wafanyakazi (Wahadhiri na Waendeshaji) kwa asilimia mia moja.

(ii) Serikali inatoa fedha ya uendeshaji na matumizi mengine ya chuo. Fedha hizi ni kwa ajili ya shughuli za ufundishaji na ujifunzaji pamoja na vitendea kazi vya Ofisi.

(iii) Serikali pia hutoa fedha kwa ajili ya maendeleo ya chuo.

(iv) Wapo wanachuo wanaosoma chuo kikuu huria cha Tanzania ambao hupata mkopo kwa ajili ya masomo, gharama za mafunzo kwa vitendo na vitabu.

(b) Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kama vilivyo vyuo vikuu na taasisi nyingine za umma kinakabiliwa na changamoto mbalimnbali zikiwemo:-

- Upungufu wa miundo mbinu na majengo ya kufundishia na kujifunzia katika mikoa.

- Uhaba wa wanataaluma.

- Utegemezi wa magari ya kukodi kwa kusafirisha mitihani, vitabu na vifaa vingine kwenda mikoani.

- Ufinyu wa Bajeti ya matumizi mengine na maendeleo ambayo haiendani na kasi ya upanukaji wa shughuli za Chuo Kikuu.

- Gharama kubwa za uchapishaji kwa vile chuo hakina mtambo wa kuchapisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuvisaidia vyuo vikuu ili viweze kukabiliana na changamoto zinazovikabili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kikiwa kimojawapo.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Chuo Kikuu Huria, kinakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa Bajeti. Na ndio inayosababisha changamoto ambazo amezitaja Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Serikali itakuwa tayari

sasa kukiongezea Bajeti Chuo hiki muhimu ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo hapa imesikia na ninafikiri itakuwa tayari iwapo Chuo Kikuu chenyewe, kwa sababu mchakato wa Bajeti unaanzia kwenye taasisi. Kwa hivyo taasisi yenyewe yaani Chuo Kikuu Huria kitakapokuwa kimeleta mapendekezo basi tutaona hali halisi. Na sisi Wizara kama munavyojua tunapeleka Hazina na kila mwaka tunajenga hoja kuombea Chuo Kikuu Huria pesa kwa ajili ya maendeleo na kwa ajili ya kazi nyingine za Chuo. *(Makofi)*

Na. 9

**Kufufua Shule za Msingi za Ufundi – Lindi**

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa shule ya ufundi *VETA* Mkoani Lindi unachukua muda mrefu kumalizika:-

Je, Serikali haiwezi kusaidia kuanza kufufua shule za Ufundi za msingi zilizopo mkoani Lindi ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira binafsi kwa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa shule na vyuo vya ufundi stadi katika kuwawezesha vijana wa Kitanzania kujitegemea na kuongeza pato la Taifa. Hivyo nakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kuhusu umuhimu wa shule za ufundi za msingi.

Mheshimiwa Spika, shule za ufundi stadi zipo na zitaendelea kutoa mafunzo kujitegemea kwa vijana. Katika baadhi ya maeneo shule hizi bado zinafanya vizuri mfano shule za Mbinga na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mchango mkubwa unaofanywa na shule hizi kwa taifa, natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha katika Bajeti kwa ajili ya uendeshaji na ununuzi wa vifaa vya kuendeleza shule hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na wanachji wa Lindi kuwa kazi ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Lindi inaendelea kwa kasi ya kuridhisha na Serikali itaendelea kuhakikisha chuo kinakamlika na kutoa huduma kama inavyopasa.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwamba *VETA* inaendelea vizuri. Lakini mpaka kwisha *VETA* kufanya *finishing,* kukabidhiana, itachukua muda ule ule kama tunavyosubiri miaka yote. *(Kicheko).*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba sana kwa jitihada za makusudi kabisa, shule hizi ambazo zilikuwa za ufundi za msingi katika mkoa wa Lindi, Singino, Njinjo, Kipatimu, Kilimalondo, Liwale, Mbarikiwa Chimbuko, Kilimalondo tena – Nachingwea, Mnero, Marambo, Nachingwea Mjini, Mbekenyela, Mkowe, Mtama na Mpilipili, shule hizi ningeomba sana jitihada za makusudi zichukuliwe ili kuweza kuzisaidia ziweze kufanya kazi yake vizuri. Kwa sababu, mpaka sasa hazina vifaa. Zitasaidia sana shughuli za vijana kujiajiri. Naomba sana tusaidiwe. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO A UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Lindi, kwa umaarufu wake na ufuatiliaji wake wa karibu kuhusiana na masuala ya elimu na hasa kwa kuwa na yeye mwenyewe ni mwalimu mstaafu.

Lakini ninaomba nikubaliane naye kwamba vituo alivyovitaja vilikuwa vinatoa stadi mbalimbali kulingana na mahitaji ya vijana katika maeneo hayo. Na ninaomba nimwahidi kwamba tutalifanyia kazi hilo suala kuangalia labda angalao shule mbili, basi tuweze kuzisaidia, hasa hasa Halmashauri za Wilaya ile ziweze kuanza kutoa stadi hizo kwa ajili ya vijana wa maeneo hayo *(Makofi).*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Swali linalofuata linaelekezwa Wizara ya Fedha na Uchumi, na linaulizwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

Na. 10

**Taasisi Binafsi za Mikopo kutoza Riba Kubwa**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa taasisi mbalimbali za binafsi kama vile *Bay Port Financial Services, Blue Financial Sevices, Pride Tanzania, Ease Financing* na kadhalika, zinazojishughulisha na utoaji wa mikopo hutoza kiasi kikubwa sana cha riba katika mikopo yao:-

Je, Serikali haioni kwamba taasisi hizo zinawanyonya wananchi wetu kuliko kuwasaidia?

Je, ni chombo gani hasa cha Serikai kinachodhibinti mwenendo wa taasisi hizo hasa katika suala zima la riba?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, taasisi binafsi zinazojishughulisha na utoaji wa mikopo zipo nyingi hapa nchini kwetu na kila mojawapo na kwa nguvu zake zote inatafuta wateja wengi zaidi. Kwa maana hiyo, wanachi wanao uwanja mpana wa kuchangua taasisi zinazokidhi pamoja na mambo mengine, mahitaji yao na huduma bora. Serikali ilitegemea kuona kwamba wananchi watachagua taasisi ambazo zinatoa huduma za kuridhisha pamoja na riba nafuu, ili wao wenyewe waweze kufaidika na mikopo hiyo. Kwa kuwa, taasisi za fedha zina uelewa mkubwa zaidi wa masuala ya fedha na uchumi, kinachohitajika kwa sasa ni kuwasaidia wananchi wetu katika kuwapatia elimu ya ujasiriamali pamoja na kuwaelimisha juu ya mwenendo wa soko. Maeneo hayo mawili yatawawezesha sana wananchi wetu kuelewa kuwa mkopo wanaotaka kuuchukua utawasaidiaje kuwakomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, *Financial NGOs* zinajumuisha kampuni kama ya *Bay Port Financial Services, Blue Financial Services, Pride Tanzania* na *Easy Finance* ni taasisi zinazotumia fedha zao wenyewe kukopesha jamii. Taasisi hizi zinatoa mikopo kwa kutumia mitaji iliyowekezwa na wamiliki bila kupokea amana toka kwa wateja wao, hivyobasi hakuna chombo kilichopewa dhamana ya kudhibiti mwenendo wa riba kwa taasisihizi. Sera ya Taifa ya *Microfinance* inaelekeza kwamba viwango vya riba kwa ajili ya mikopo vitapangwa na taasisi zenyewe bila kuingiliwa na Serikali, Benki Kuu wala Wafadhili.

Hali hii inatokana na kwamba ni taasisi zenyewe ndizo zinazofahamu gharama, soko na mbinu za biashara na wateja wao wote. Cha msingi ni kuhakikisha kuwa idadi ya taasisi zinazokopesha zinaongezeka ili kutoa huduma kwa ushindani pamoja na kuwa na chombo kitakacho simamia mwenendo mzima wa shughuli za taasisi hizi na hii ndio njia muafaka ya kuleta suluhisho katika taasisi hizi pamoja na tatizo la riba.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Mheshimiwa Naibu Waziri, amelieleza Bunge lako Tukufu kwamba taasisi hizi zinatumia mitaji yake kwa kukopesha na ndio sababu serikali inashindwa kudhibiti mwenendo wa riba ambazo ni kubwa sana.

Sasa naomba kujua ni kwa nini Taasisi za Serikali kama vile Wizara, Taasisi mbalimbali kama wakala wa Serikali na Halmashauri, zitumike kama *agents* wa makampuni haya kuwaingiza wafanyakazi hawa kwenye mikopo ambayo riba yake ni kubwa sana, wakati hawajaonesha njia nyingine ambazo wafanyakazi wangeweza kukopa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Hivi ni nchi gani duniani ambayo imeacha tu Serikali au wananchi wake au makampuni yaendelee tu kukopesha wanavyoona wao wenyewe bila kuwa na chombo chochote cha kuyasimamia? Hivi kazi ya Benki Kuu, ni nini hasa? Tunaomba Mheshimiwa Waziri, atueleze. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Katika jibu la msingi nimeeleza, *The Microfinance Policy* ndio iliyotuelekeza kwamba taasisi hizi zisiingiliwe katika kupanga viwango vya riba. Ni Sera yetu wenyewe, lakini ninataka nikiri kwamba, hili tumeliona ni upungufu na tunalifanyia kazi.

Lakini la msingi ambalo Mheshimiwa Zambi, amelielekeza, ni kwa nini Taasisi za serikali zinaingia katika kuwakata mikopo au kuwadhamini. Nataka niseme tu kwamba hawa wanaokopesha ni lazima waangalie soko lao liko wapi. Soko kubwa ni wafanyakazi wa Taasisi za Serikali na ni kwa sababu mfanyakazi mwenyewe anajidhamini kwa mshahara wake. Na ni kwa maana hiyo Taasisi za Serikali zinakubali kwamba huyo ni mfanyakazi na hatimaye wakikubaliana baina ya mkopaji na mkopeshwaji, Taasisi ile itakata sehemu ya mshahara wake ili kuweza kufidia mkopo husika.

Mheshimiwa Spika, swali *(b).* Mheshimiwa Zambi, amesema ni kwa nini tunawaanchia wananchi wetu wanaingia katika mikopo hii ambayo ina riba kubwa?

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba Serikali kupitia Benki Kuu imeliona tatizo hili na sasa tunaangalia jinsi ya kuwa na chombo ambacho kitadhibiti hizi *Financial NGOs. (Makofi)*

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, swali hili limeulizwa ndani ya Bunge hili mara kadhaa. Wanaoumia ni Watanzania wetu, wananchi wetu, kama tatizo ni la Sera na Waziri anakiri kwamba wameliona. Linachukua muda gani kufanya marekebisho kuwaokoa wananchi hawa ambao wanateseka, wanalalamika kimya kimya, hawana mahali pengine pa kwenda kwa sababu taasisi hizi ndizo pekee zinazotoa hela.

Lakini wanakwenda kule kwa sababu hawana namna nyingine, kwa sababu ni taasisi pekee. Na kwa kweli kama alivyosema wananchi watachagua, hawana pa kuchagua kwa sababu haziko zote katika maeneo yote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, wananchi wanalazimika kwenda.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lini Serikali itatoa utaratibu ulio mzuri kurekebisha Sera ambayo Waziri ameisema ili wananchi waweze kulindwa kama nchi nyingine zinavyolinda watu wao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI ( MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Dr. Slaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi. Taasisi hizi usajili wake uko chini ya *NGO,* na baadhi ya Taasisi zinasajiliwa na *BRELLA* kwa maana ya makampuni, kama ni kampuni. Tulichokifanya sisi kupitia Benki Kuu, ni kuangalia mwenendo mzima wa Riba ndani ya Taasisi hizi na tumegundua kwamba baadhi ya Taasisi hizi zinatoza riba kwa wiki, baadhi kwa mwezi. Hili ndilo linalofanya kwamba riba kwa mwaka inakuwa kubwa sana. Sasa Dr. Slaa, anataka niseme ni lini tutarekebisha hiyo Sera.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie tu kwamba katika kipindi kifupi kijacho tutarekebisha hii sera na kuunda chombo ili kiweze kusimamia hizi *Financial NGOs. (Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, bado Wizara hiyo hiyo. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mbunge wa Mikumi, hayupo!

Na. 11

**Hitaji la Benki Katika Mji Mdogo Wa Mikumi**

**MHE. MWANNE J. MCHEMBA K.n.y. MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakazi wa mji mdogo wa Mikumi wapatao 20,000 hawana huduma ya Benki na hulazimika kufuata huduma hiyo umbali wa Kilometa 72 mpaka Ruaha; na kwa kuwa, mji huo ni kitovu cha biashara na hukutanisha wafanyabiashara wengi, wasafiri na hata watalii kutoka Mahenge, Dar-es-Salaam na kadhalika.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzishawishi Benki za *NMB/CRDB* kufungua matawi katika mji huo ili kuondoa usumbufu kwa wananchi hao?

**SPIKA:** Inaonekana ni utaratibu sasa Mbunge mwanaume asipokuwapo, basi swali kwa niaba linaulizwa na mwanamke! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa tawi la Benki hutegemea vigezo mbalimbali ambavyo vitakidhi matarajio ya biashara ya kibenki. Katika kufikia maamuzi ya kufungua tawi la Benki, vigezo vifuatavyo hutumika:-

(i) Kuzingatia uwezo wa kifedha wa eneo husika.

(ii) Jamii husika kuhitaji pamoja na kuwa na uwezo wa kulipia huduma mbalimbali za kibenki kutokana na shughuli zao za kiuchumi zilizopo.

(iii) Kuwepo kwa miundombinu kama vile barabara, umeme, mawasiliano ya simu, usalama na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa kwa benki yoyote ile ni kufungua matawi kwa nia ya kusogeza huduma karibu na wananchi. Ufunguaji wa matawi ya benki unaambatana na utafiti wa kina wa kiuchumi ambao unaonesha kuwa tawi likifunguliwa litatengeneza faida na litakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mabenki yanaendesha shughuli zake kwa ushindani, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuwahamasisha *NMB* na *CRDB* pamoja na wananchi kuanzisha benki katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mji mdogo wa Mikumi kwa lengo la kuwapatia huduma za kibenki wananchi na kwa gharama nafuu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametueleza hapa kuna vigezo kamili vya kufuata ili tawi liweze kufunguliwa mahali husika. Na kwa kuwa, kwa mji mdogo wa Mikumi, vigezo alivyovisema Mheshimiwa Waziri, vyote vimetimia na sio mara ya kwanza kwa mji huu mdogo kuombewa tawi la Benki. Na kwa kuwa, pale kuna wafanyabiashara wengi wanateseka kwenda Kilombero, wengine kwenda Morogoro Mjini, wengine kwenda Ruaha na ni miaka mingi wamekuwa wakipata adha hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali tunaomba ituambie sasa kwa kuwa imekuwa inatoa ahadi ambazo hazina *limit.* Ni lini sasa tawi lile litafunguliwa pale angalao wananchi waweze kufanya kazi zao kwa tija na kutopoteza hela nyingi kusafiri kwenda mbali na ku-*risk* hela zao kwa ajili ya kwenda kuzihifadhi benki kwa ajili ya maendeleo yao? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI ( MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *I wish* ingekuwa hizo benki ninazo mfukoni, ningekwenda nikaweka pale. Lakini kwa sababu tu kazi ya Serikali ni kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya Benki hizi kufungua matawi yao katika maeneo mbalimbali, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Sakaya, kwamba tutajitahidi kwa upande wetu kuzisukuma hizi Benki ili ziweze kufungua matawi yao katika mji wa Mikumi. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kuwa kuwa vigezo alivyovitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, vimekidhiwa kabisa katika eneo la Bumbuli. Na kwa kuwa, suala hili nimeshaliuliza mara nyingi na aliyekuwa naibu Waziri, Mheshimiwa Mustapha Mkullo, aliahidi kwamba tutasaidiana kulisukuma hili na kwa kuwa *NMB* wana habari.

Je, Naibu Waziri, anasemaje kuhusu hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shellukindo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nadhani sisi sote ni mashahidi, sio Mheshimiwa Shellukindo peke yake ambaye ameomba katika eneo lake kupata tawi la benki, ni Wabunge wengi sana tumeomba. Na sisi ni mashahidi, baadhi ya maeneo tayari tumeshafungua matawi ya Benki.

Namwomba sana Mheshimiwa Shellukindo avute subira na sisi tutaendelea kuwahimiza wenzetu hawa na hatimaye, kama biashara Bumbuli ipo, basi *definately* hakuna ambaye anakataa kuweka tawi la benki kwa ajili ya biashara yake. Tutahimiza na *inshallah* watafungua katika eneo la Bumbuli.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya ziada. Kwanza namshukuru Naibu Waziri, kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuelezea tu kwamba, kwa kweli maombi ya matawi katika majimbo yetu ni mengi sana. Tumejitahidi kwa upande wa Tanga kwa mfano Kilindi, nadhani tayari tawi limeshafunguliwa na mahali pengine tumefanya hivyo. Sasa ni vigumu sana kwamba kila utakaposema mimi nataka nifunguliwe tawi watalifungua, kwa mfano kwa upande wa Mikumi, maombi yalikuwa matatu, *NMB* wameshafungua tawi Gairo, wakati wowote wanaweza wakafungua tawi Mikumi. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subira, tutajitahidi kadri tutakavyoweza, bahati mbaya ni kwamba zile benki sasa hivi zote sio za Serikali ni za binafsi, Serikali inachoweza kufanya ni kuwaomba, sasa wanafanya *feasibility study*, wakiona sehemu ile kweli vile vigezo kama vinavyosemekana vinakidhi, watakwenda kufungua tawi na tutajitahidi kufanya kila kinachowezekana kuhakikisha kwamba hilo linafanyika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, tunahamia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, nitoe taarifa tu kwamba kutokana na Taarifa ya Spika na kusomwa kwa

nyaraka mbalimbali zilizokuwa zinawasilishwa Mezani, tunaongeza muda kidogo ili tuyamalize maswali yote.

Na. 12

**Tatizo la Maji Kijiji cha Bumila Wilaya ya Mpwapwa.**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kijiji cha Bumila katika Kata ya Kimagai Wilayani Mpwapwa, kina tatizo kubwa la maji na kwa kuwa, kijiji cha Bumila kina mabomba ya maji lakini hayatoi maji kutokana na uchakavu wa miundombinu hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati mabomba hayo ili wananchi wa Bumila waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALIZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la maji katika kijiji cha Bumila. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, imepanga kutumia kiasi cha shilingi milioni 51,350,000, kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji kwa mtiririko wa kijiji cha Bumila, kupitia Mfuko wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa, ili kuuboresha na hivyo kuondoa kero za maji katika kijiji cha Bumila. Ukarabati huo umepangwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango mzuri wa Serikali, uendelevu na uhai wa mradi wa maji unategemea pia uimara na dhamira ya dhati ya utunzaji kupitia Kamati ya Maji ya Kijiji cha Bumila. Kutoweka ulinzi wa kutosha katika miundombinu ya mradi, kunaweza kusababisha uharibifu na hatimaye kukosa huduma za maji, hivyo ni muhimu kwa wananchi wenyewe kushiriki kikamilifu katika kumiliki, kuutunza na kuusimamia mradi huo. Ni imani yangu kuwa mradi utasimamiwa vizuri mara baada ya ukarabati kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na wananchi wa kijiji cha Bumila, kuimarisha ulinzi wa mradi, ili wizi zaidi usiendelee kutokea wakati Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ukarabati.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa, kijiji hiki cha Bumila pamoja na vijiji vya Chibochagula, Lupeta na Makutupa, vinatumia chanzo kimoja cha maji ambacho kwa kweli maji hayatoshelezi kwa huduma ya maji katika vijiji hivyo na kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kufanya utafiti wa vyanzo vingine vya maji, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa wakati umefika utafiti huo ufanyike ili tuweze kuongeza vyanzo vingine kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALIZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi nataka nilifahamishe Bunge lako kwamba katika mji wa Mpwapwa ambapo Mheshimiwa Mbunge anatoka, mradi uliopo pale wa maji ni wa shilingi bilioni nne ambao unahisaniwa na nchi ya Ufaransa. Kuna jitihada kubwa sana zinafanyika katika kuhakikisha kwamba mji wa Mpwapwa unapata maji ya kuaminika na Mheshimiwa Lubeleje amefanya kazi kubwa sana katika kuhimiza na kuhakikisha mradi huu unakamilika. *(Makofi)*

Sasa anauliza vijiji hapa amevitaja ambavyo siwezi kuvikumbuka kwa kichwa lakini mimi nimekwenda mpaka kule na nimeona haya maeneo anayazungumzia, katika hii miradi ya maji ambayo inaendelea kuna visima ambavyo vinachimbwa kupitia *Quick Wins* ambazo zimepatikana kutokana na *World Bank.* Nina hakika tukimueleza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhusu hiki anachokizungumza kwa ajili ya kusaidia hivi vijiji, sina tatizo kwamba atakataa au kwamba hatakubaliana na jambo hili. Kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Malima Lubeleje kwamba suala hili tutalifikisha na litafanyiwa kazi, ataona kitakachokuwa kinaendelea baada ya hapo. *(Makofi)*

Na. 13

**Miradi ya Kilimo katika Bonde na Maji ya Mto Ruvuma**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Kumi na Saba, Bunge lilipitia na kuridhia Mpango wa Matumizi ya pamoja na Bonde na Maji ya Mto Ruvuma ambapo nchi wanachama watanufaika na miradi mikubwa ya kilimo katika mpango huo:-

(a) Je, ni mradi gani katika Mkoa wa Ruvuma umeshaingizwa katika mpango huo mpaka sasa?

(b) Je, ni miradi mingapi ya umwagiliaji imeshatambuliwa katika Jimbo la Peramiho na Halmashauri ya Wilaya ya Songea?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya miradi hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALIZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a), (a) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa ni jumla ya miradi kumi na ya jamii yaani *community based projects* kutoka Mkoa wa Ruvuma ndiyo iliyopendekezwa kutekelezwa katika Mpango wa Matumizi ya Pamoja ya Bonde na Maji ya Mto Ruvuma. Miradi hiyo inajumuisha:-

(i) Mradi mmoja wa umwagiliaji katika Wilaya ya Songea katika eneo la Namatuhi;

(ii) Miradi ya minne ya Hifadhi ya Mazingira, katika eneo la Mbinga kuna mmoja, Namtumbo kuna mmoja na Tunduru kuna miwili;

(iii) Kuna miradi minne ya maji ya kijamii ambayo iko katika Wilaya ya Mbinga, kuna mmoja Tunduru, kuna mmoja Namtumbo na Songea vijijini kuna mmoja; na

(iv) Mradi mmoja wa kuboresha maji safi na uondoaji taka katika Manispaa ya Songea.

(b) Mheshimiwa Spika, ni mradi mmoja tu wa umwagiliaji uliotambuliwa katika Jimbo la Peramiho na Halmashauri ya Wilaya Songea ili utekelezwe katika mpango huu ambao ni Mradi wa Umwagiliaji wa Namatuhi. Mradi huu umetengewa kiasi cha U$D200,000 na mpango huu umeanza kukarabatiwa kwa kutumia fedha hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotengwa kwa kutekeleza miradi kumi niliyoitaja hapo juu katika sehemu (a) ni Dola za Kimarekani 3,610,750.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanri kwa ustadi wake mkubwa sana katika kujibu maswali yetu hapa ndani, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ninalo swali moja la nyongeza, kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Peramiho na hasa wale wa Kata ya Ndogosi, kijiji cha Namatuhi, watafaidika sana na mradi huo mkubwa kupitia Mkakati huo wa Matumizi ya Bonde na Maji ya Mto Ruvuma wenye pesa nyingi sana za Kitanzania ambazo zitasaidia sana uzalishaji kwa njia ya kilimo cha umwagiliaji. Sasa Serikali inafikiri nini katika kusaidia uzalishaji huu uendane na miundombinu mingine ? Labda katika mipango ya baadaye miradi hii mikubwa ingeunganishwa na miradi ya miundombinu kama barabara na masoko, umeme ili kukamilisha ile *chain* nzima ya uzalishaji katika maeneo hayo makubwa ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ninaomba tu kujua je, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Wizara hiyo, wako tayari sasa kuja kule Jimboni Peramiho na hasa katika maeneo hayo niliyoyataja kuja kupokea shukrani za dhati kwa Serikali hii ya Awamu ya Nne, kwa kutekeleza mradi huu mkubwa sana wa kihistoria katika Jimbo hili la Peramiho? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALIZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa maneno yake ya ushuhuda aliyotoa kuhusu mimi namshukuru sana.

Pili, niende kwenye hili analozungumzia la kwenda kule Peramiho, kwa moyo mkunjufu, nitawashauri waweze kufika kule, mimi mwenyewe nilifika, nimeona kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Jenista anafanya, tulimuonea wivu kwa kazi ambayo anaifanya pale, tunampongeza sana kwa kazi nzuri anayofanya. Kwa hiyo, nitamshauri Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji ili ama yeye mwenyewe au Naibu wake waweze kwenda kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo analizungumza hapa, nimeu-*study* ule mradi, ule mradi unaendeshwa chini ya *SADC*, tuliupitisha hapa Bungeni, kama mnakumbuka, kuna nchi ya Msumbiji, kuna nchi ya Zambia, Malawi wako pale pamoja na hizi nchi zote za *SADC* pamoja na sisi wenyewe Tanzania. Ukiangalia maudhui ya mradi ule kwa maana ya *content* yake, unaangalia zaidi suala la mazingira, suala la mifereji, suala la kuanzisha vyanzo vya maji, ninayo orodha za miradi iliyoko hapa. Lakini Mheshimiwa Mhagama analeta jambo lingine kubwa zaidi, anazungumzia suala *structural linkage* kwamba huwezi tu ukafanya kazi hiyo peke yake ukainua uchumi, watu wakamwagilia lakini wakati huo huo hujajenga miundombinu kwa maana ya masoko, barabara na vitu vingine na anajaribu kuona kwamba ni vitu gani ambavyo vinaweza vikafanyika hapa. Mradi huu unaendeshwa chini ya sekretarieti ambayo ni ya *SADC* na chini ya *African Development Bank* na hela zinapokuja, zinakuja Wizarani halafu zinakwenda kule.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema hapa sasa hivi kwa sababu tunajibu kwa niaba ya Waziri ni kwamba nitalichukua hili wazo kwa sababu hiki ni kitu kingine sasa ambacho kinaweza kikafanyiwa kazi na *I am quite sure* ukiangalia *projection* za muda mrefu itakuwa inaonyesha pia mambo kama hayo. *For the time being,* naomba nimhakikishie Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba nalichukua hili, tutakwenda kulifanyia kazi lakini turudie tena kusema kwamba tunampongeza sana kwa kazi nzuri anazofanya. *(Makofi)*

Na. 14

**Shughuli za Biashara Nchini.**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, muda mrefu tangu nchi yetu ipate uhuru hadi mwaka 1992 Serikali ilikuwa ikifanya biashara kupitia Mashirika ya Umma, hivyo muda wa shughuli za biashara kama maduka ulifuata saa za kuanza kazi na kumaliza kazi za ofisi za Serikali:-

Kwa kuwa, Serikali sasa haifanyi biashara, je, kuna sababu gani za msingi kwa wafanyabiashara hasa wa maduka kufunga maduka saa 9.30 alasiri kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na kutofungua kabisa Jumamosi na Jumapili, hasa eneo la Kati la Jiji *(City Centre)?*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hadi kufikia mwaka 1992, wakati uchumi ulikuwa unaendeshwa na sekta ya umma, maduka ya biashara ya Mikoa yaani *RTCs*, maduka ya wafanyakazi sehemu za kazi, maduka ya ushirika na maduka ya vijiji, yalikuwa yakifanya biashara kwa kufuata muda wa kazi uliowekwa wa saa za Serikali kwa kuwa waliohudumiwa na maduka hayo, wengi wao walikuwa watumishi wa umma na wananchi wachache waliokuwa jirani na maduka hayo. Hata hivyo, wakati huo maduka ya watu binafsi yaliachwa yajiendeshe yenyewe bila kupangiwa muda maalum wa kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazoea kwamba jioni, usiku na siku za mwisho wa wiki ni muda wa mapumziko kwa wananchi walio wengi, shughuli za biashara wakati huo hupungua. Katika kipindi hiki cha soko huria, hakuna sheria inayozuia wafanyabisha kuendelea na biashara zao baada ya saa tisa na nusu au siku za Jumamosi na Jumapili. Hata hivyo, wafanyabiashara walio wengi hasa katikati ya majiji na miji huamua kufunga kwa hiari maduka yao mwisho wa wiki kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kuwepo kwa uwezekano wa mauzo kuwa kidogo muda huo kutokana na wadau wengine kuwa mapumzikoni mbali na maduka hayo;

(ii) Kupunguza gharama za uendeshaji kwa kukwepa kulipa posho au mishahara ya masaa ya ziada;

(iii) Kushamiri kwa biashara kuanzia muda wa saa mbili na nusu hadi saa tisa na nusu jioni katika Majiji, Manispaa na Makao Makuu ya Wilaya kwa siku za wiki isipokuwa Jumamosi na Jumapili;

(iv) Kutoa nafasi kwa wafanyakazi wa maduka husika kupumzika; na

(v) Sababu za usalama.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa

Naibu Waziri, napenda tu kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, je, si wakati muafaka sasa wafanyabiashara wa Tanzania wabadilike, wasifanye biashara kwa mazoea? Nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa shahidi kwamba katika miji mingi alikotembelea huko katika wadhifa wake, unakuta maduka makubwa kama *Super Markets* yanafanya kazi mpaka saa nne usiku, kutoa nafasi kwa watu walioko maofisini kuweza kwenda kupata mahitaji yao. Sasa hivi ukipata *Samora Avenue* utaona wafanyakazi wa Serikali saa za kazi wanakwenda madukani kwa sababu hawana muda mwingine, je, si vizuri wakabadilika?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema mwanzoni, hakuna sheria ambayo inakataza mtu yeyote kuendelea kufanya biashara isipokuwa zile sababu ambazo nimezitaja hapa pengine mtu anaona kwamba haitalipa kama akifungua duka wakati wateja wote wameshakwenda maeneo yao ya kuishi hasa katikati ya majiji. Isipokuwa napenda kukubaliana na ushauri wake kwamba katika maeneo yale ambapo wafanyabiashara wanaona kabisa kwamba inalipa, ni vizuri maduka yale yakawa wazi ili mtu akifanya kazi hata akitoka ofisini saa moja au saa mbili atajua kwamba akienda kwenye *super market* atapata bidhaa, akienda kwenye duka fulani atapata bidhaa. Kwa kweli katika maeneo ya miji kule ambako watu wanaishi, kwa mfano Temeke ukienda pale utakuta maduka yako wazi mpaka saa nne usiku. Ukienda maeneo fulani kule Ilala utakuta maduka yako wazi mpaka saa sita usiku. Sasa niungane naye kutoa wito kwa Watanzania kwamba wale ambao wanaona inalipa, ni vizuri wakafanya kama anavyoshauri na Serikali tutaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba usalama katika maeneo husika unakuwepo wakati biashara inafanyika muda huo ambao unaweza ukawa muda wa hatari kidogo. *(Makofi)*

Na. 15

**Kuanzisha SIDO - Pemba**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA – K.n.y MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, *SIDO*, ni shirika linalosaidia sana kuwaendeleza wajasiriamali hapa Tanzania hasa wanawake:-

Je, Serikali haioni haja ya kuiagiza *SIDO* kuanzisha harakati zao kwa wanawake Kisiwani Pemba?

**SPIKA**: Nilikuwa nauliza kwa sababu si kawaida kuruhusu Mheshimiwa Mbunge aulize maswali mara mbili, sasa kwa kuwa ndiyo aliyeachiwa basi Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chakechake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* linasaidia sana kuwaendeleza wajasiriamali hapa nchini wakiwemo wanawake. Aidha, Shirika hilo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge, Na. 28 ya mwaka 1973 kwa lengo la kuendeleza viwanda vidogo. Chombo hiki kina ofisi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na kwa sasa hakina mipango ya kuanzisha haraka za shughuli zake Pemba, kwani sheria iliyokianzisha chombo hiki iliweka bayana kuwa eneo lake la kufanyia kazi ni Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, *SIDO* imekuwa ikitoa huduma zake Visiwani ikiwemo kutoa mafunzo ya usindikaji wa matunda, nafaka, mboga na viungo (*spices*). Hadi mwishoni mwa mwaka 2008, ni zaidi ya wajasiriamali 60 wengi wao wakiwa wanawake, wamefaidika na hayo. Aidha, shirika liko tayari kuendelea kutoa ushirikiano kwa makubaliano na wadau au vyombo vinavyotoa huduma za kuendeleza sekta hasa katika harakati za kutekeleza sera maalum ya kuendeleza sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo huko Visiwani.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni mwisho wa maswali, maswali yamekwisha na kipindi kimepita, kama kawaida tunayo matangazo yetu hapa tukianza na wageni.

Kwa heshima na taadhima na pia kwa furaha kubwa, napenda mtambue uwepo kwa Wabunge wenzetu kutoka Kamati ya Kupambana na Ukimwi kutoka Bunge la Uganda, ambao ni Mheshimiwa Beatrice Rwakimari, kiongozi wa msafara, Mheshimiwa Prof. Willy Anokbonggo, Mheshimiwa Beatrice Atim, Mheshimiwa Dk. Cris Baryomunsi, wao wanne halafu wasaidizi wao ni ndugu Ignatius Kasirye, Mkurugenzi Msaidizi Kamati, Bi. Josephine Watera, Mtafiti wa Kamati na Bi. Aceng Florence, Mwanasheria wa Kamati. *(Makofi)*

*On behalf of Tanzanian Parliament, we have pleasure to welcome brothers and sisters Honorable from Uganda. We value this cooperation between us because it makes possible for us to run from each other and to encourage each other. Thank you very much and long leave East Africa. (Applause)*

Wapo wageni kumi na watatu wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira kutoka bodi ya *SACCOS*, Bunda, wakiongozwa na Ndugu Mussa Magohe, Makamu Mwenyekiti, wale wa Bunda, karibuni sana tuwaone. Namuomba ndugu Mussa Magohe, apunge mkono peke yake, yule ndiyo kiongozi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kutoka *CCBRT* ambao ni ndugu Jacqueline Kweka, *Research Officer* na ndugu Fredrick Msigalla, nadhani hawezi kusimama kwa sababu ya maungo yake, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge wenye ulemavu ambapo Wabunge hao ni Mheshimiwa Zuleikha, Mheshimiwa Al-Shymaa na Mheshimiwa Margreth Mkanga, wanatoka Taasisi za Watu Wenye Ulemavu SHIVYAWATA, ICD, *CCBRT* na viongozi

wa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu, Mkoa wa Dodoma, tunawaomba nao tuwatambue, wanaoweza kusimama, wasimame. *(Makofi)*

Kipekee, nashukuru kuwepo Mkalimani wa wale wasioweza kusikia, kwa hiyo, tunampongeza, mnaona anafanya zile ishara, huwa tunaangalia, unashangaa kwamba inawezekana kwa binadamu kutengeneza aina fulani za ishara na zikaleta maana, hongera sana. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Masuala ya UKIMWI, ameomba saa sita mchana ambayo tayari imepita, nadhani itakuwa ni mara baada ya kikao hiki, wakutane pamoja na wageni wetu kutoka Uganda, katika Ukumbi Namba 231, *Chamber Room No.231, second floor, administration building, for the meeting with our colleagues from the Republic of Uganda and from the Parliament of Uganda, one o'clock and ten minutes.*

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo kutakuwa na kikao cha Kamati, saa saba na kitafanyika ukumbi namba 227, ghorofa ya pili jengo la utawala.

## MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

*(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2010 *[The Persons with Disabilities Bill, 2010].*

Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010 *[The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010].*

Muswada wa Sheria ya Malisho na Vyakula vya Mifugo 2010 *[The Grazing land and Animal Feed Resources Bill, 2010].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Fedha wa Mwaka 2010 *[The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2010].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana wa Mwaka 2010 *[The Capital Markets and Securities (Amendment) Bill, 2010].*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, Miswada inaposomwa kwa Mara ya Kwanza maana yake itaingia katika hatua ya kusomwa Mara ya Pili kwenye kikao kinachofuata au vinavyofuata, sasa hii inaelekea itabidi ifanyiwe kazi kwenye kikao au kwenye Mkutano huu wa Kumi na Tisa, kwa hiyo, Katibu naomba uendelee kumuita…

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, naomba kukukumbusha kwamba kwa kuwa kanuni ya muda hatujaizingatia, tungefuata utaratibu kwanza wa kutengua kanuni kwa sababu ya wakati ili tuweze kuendelea na shughuli zetu bila kuvunja kanuni.

**SPIKA:** Ahsante kwa kutukumbusha hilo. Nilikuwa naona kama dakika nne zile zingetosha lakini pengine ni kweli basi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, atoe hoja ya kutengua kanuni ya kusitisha shughuli saa saba kamili ili hata ikipita kidogo basi tuweze kukamilisha shughuli anayoiwasilisha yeye, ahsante.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liendelee kujadili hoja zilizopo mbele yetu hadi tutakapokamilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msibabaike, kiti kitafafanua tu. Mheshimiwa Waziri ametoa hoja kwamba kanuni inayohusika na muda wa Bunge itenguliwe ili tuendelee na shughuli hata kama ni baada ya saa saba kwa madhumuni ya kukamilisha shughuli iliyopo mbele yetu ingawa naona Mawaziri waliosimama kuunga mkono hoja hii wengine walikuwa bado wanashangaa, kwa kuwa leo ni siku ya kwanza ya Mkutano wa Kumi na Tisa basi Kiti kinakuwa na huruma kwa Serikali na kwa hiyo tunaendelea, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, hoja ya kuruhusu Miswada kupitishwa katika hatua zake zote.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 80(2), Kanuni ya 83 na Kanuni ya 93(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2007, zimeweka masharti kwamba Muswada wa Sheria mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali, utasomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni na kwamba Bunge halitashughulikia kwa hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika mkutano mmoja wa Bunge na ninaomba ninukuu Kanuni ya 80(2), inasema:-

*"Tangazo la kwanza la Muswada wa Sheria litatolewa na kumfikia Katibu katika muda usiopungua siku 21 kabla ya Muswada huo kusomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza, na litaonyesha Muswada mzima ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu madhumuni ya Muswada huo yaliyotiwa saini na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali".*

Kanuni ya 83(1) inasema:-

*"Muswada wowote wa Sheria ambao umetangazwa kwenye Gazeti, unaweza kuwasilishwa Bungeni kufuatana na Orodha ya Shughuli ili Kusomwa Mara ya Kwanza na katika hatua hiyo Katibu atasoma jina refu la Muswada wa Sheria unaohusika bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili hiyo".*

Kanuni ya 83(2) inasema:-

*"Hakutakuwa na mjadala wowote wakati Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Kwanza".*

Kanuni ya 93(1) inasema:-
*"Bunge halitashughulikia hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika Mkutano mmoja wa Bunge".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Nane uliokamilisha shughuli zake tarehe 12 Februari, 2010, hakuna Muswada wowote uliowasilishwa kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Kwanza kama yalivyo matakwa ya kanuni zetu. Hata hivyo, zilikuwepo sababu na haja za Serikali kuleta Miswada ambayo inakusudiwa kusomwa hatua zake zote katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge ambao umeanza leo tarehe 13 Aprili, 2010.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2007, imetoa utaratibu wa kuipeleka Miswada hiyo Bungeni na kushughulikiwa katika hatua zake zote na ninaomba kunukuu:-

*"Bila kuathiri masharti ya fasili ya (1) ya Kanuni hii, Bunge linaweza kushughulikia Muswada wa Sheria kupitia hatua zake zote endapo:-*

*(a) hoja mahususi itatolewa kwamba Muswada huo ushughulikiwe katika hatua zaidi ya moja;*

*(b) Spika ataridhika na hoja hiyo; na*

*(c) Bunge litaafiki hoja hiyo kwa kupiga kura".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni hiyo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuishughulikia Miswada hii ifuatayo kwa hatua zake zote katika Mkutano wa Kumi na Tisa.

Kwanza, Muswada wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2010 *[The Persons with Disabilities Bill, 2010].*

Pili, Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010 *[The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010].*

Tatu, Muswada wa Sheria ya Malisho na Vyakula vya Mifugo 2010 *[The Grazing land and Animal Feed Resources Bill, 2010].*

Nne, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Fedha wa Mwaka 2010 *[The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2010].*

Tano, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana wa Mwaka 2010 *[The Capital Markets and Securities (Amendment) Bill, 2010].*

Mheshimiwa Spika, pia kuna Miswada ambayo inakuja kwa utaratibu wa *Certificate of Agency* ambayo baadaye itasomwa tena kwa Mara ya Kwanza na tutaleta tena hoja kama hii kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, sababu zilizoifanya Serikali kutoa hoja hii, zinatokana na ukweli kwamba Bunge hili la Tisa linafikia ukomo wake mwezi Julai mwaka huu. Hivyo, Miswada hii isipopitishwa katika mkutano huu, kuna uwezekano mkubwa wa kutokamilisha kazi ya utunzi wa Sheria zilizopangwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya kutengua Kanuni ili Miswada hii iliyosomwa Mara ya Kwanza iweze kushughulikiwa katika hatua zote katika Mkutano huu huu wa Kumi na Tisa.

Hoja imetolewa na hoja hiyo imeungwa mkono, kwa hiyo tumetengua Kanuni na tutawezesha sasa Miswada kuendelea na kwa maana hiyo pendekezo lililoko kwenye orodha ya shughuli za leo kwamba Muswada wa kwanza kabisa ni Muswada wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu tutaanza kuujadili hapo saa kumi na moja jioni.

Naomba nitoe tangazo kwamba kuna Miswada mingine ile miwili ambayo yote inahusu Sekta ya Mifugo, maudhui yake yanafanana na yote ni huduma kwa mifugo yetu hapa nchini. Kwa hiyo, nimekubaliana na Serikali kwamba Waziri mhusika ataiwasilisha Miswada hii kwa pamoja, Kamati pia na Kambi ya Upinzani watatoa taarifa zao hata kama ni wawili tofauti lakini kwa mtiririko mmoja. Hii itawezesha ufanisi katika kujadili badala ya kuwa na mipaka kati ya Miswada miwili ambayo kwa hakika inafanana na madhumuni yake yanajulikana ni yale yale, naomba kuwapa taarifa.

Baada ya hapo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.10 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2010 *(The Personal With Disabilities Bill, 2010)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele nikiwa na afya njema. Aidha, napenda nikushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2010 *(The Persons With Disabilities Act, 2010*) kama ulivyopangwa katika shughuli za leo, sasa Usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, kabla sijaanza kuwasilisha hoja yangu, naomba nichukue fursa hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, chini ya Uenyekiti wa Kaimu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame, Mbunge wa Mbozi Mashariki aliyekalia Kiti wakati wa kuuchambua kwa kina Muswada ulioko mbele yenu Jijini Dar es Salalam tarehe 1 Aprili, 2010. Kamati hii iliweza kuuchambua Muswada kwa kina na kutoa michango na maelekezo ambayo yameniwezesha kuwasilisha Muswada huu hapa Bungeni. Jedwali la mabadiliko, ni matokeo ya uchambuzi wa kina, michango na ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa kuchangia Muswada huu katika ngazi za Kamati, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile sina budi kutoa shukrani zangu kwa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania chini ya Mwenyekiti Jaji Professa Ibrahim Juma, kwa kutumia mamlaka yake chini ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania, kifungu cha 4 (1) na kifungu cha 9 ambavyo vinatoa mamlaka kwa Tume kufanyia utafiti suala lolote linalohitaji sheria kama ambavyo itakavyoona inafaa. Hata hivyo, Februari 2006, Tume hii chini ya mradi maalum ilianza kufanya mapitio ya Sheria zote zinazohusu Masuala ya

Watu Wenye Ulemavu na kuangalia ni kwa namna gani zinaendana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na mila na desturi na viwango vya kikanda na Kimataifa ambavyo Tanzania tumeviridhia. Kutokana na mapitio hayo pamoja na mawasiliano na wadau mbalimbali, Tume iliandaa maeneo ya kufanyiwa kazi ambayo kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya Muswada huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nashuikuru pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria chini ya Bwana Casmir Kyuki, katika hatua zote za maandalizi na hatimaye kukamilisha Muswada huu pamoja na jedwali la mabadiliko. Aidha, shukrani za pekee ziwaendee wadau wote ambao kwa namna moja au nyingine walichangia katika kukamilisha Muswada huu. Naomba niwatambue wadau walioshiriki katika kutoa maoni wakati wa Muswada ulipowasilishwa mbele ya Kamati mjini Dar es Salaam tarehe 31 Machi, 2010. Wadau hao ni pamoja na kwanza Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Kamati ya Taifa ya Usalama Barabarani kwa Watu Wenye Ulemavu, *Disability Organisation for Legal Assistants for Social Economic Development* (DOLASED), *Legal and Human Right Centre (LHC)* ambao pia waliwawakilisha *National Organisationm for Legal Assistance na The Foundation for Civil Society* na Sauti ya Wanawake Wenye Ulemavu Tanzania (SWAUTA). Wadau wote nawashukuru kwa michango yao kwani kwa kiasi kikubwa imeboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitishwa kwa Sheria hii, ni moja ya utekelezaji wa maagizo ya Serikali, majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ibara ya 11 na 13 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 ambazo zinazungumzia umuhimu wa nchi kuweka taratibu ambazo zitawezesha makundi mbalimbali wakiwemo Watu Wenye Ulemavu kwenye masuala ya haki ya kufanya kazi, kupata elimu ya kujitegemea, kutobaguliwa kutokana na hali ya mtu na kutoa fursa sawa ya kupata elimu na elimu ya ufundi kwa watu wote. Aidha, Ibara ya 23 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 inasisitiza umuhimu wa Serikali kuweka msingi na taratibu zinazoleta maendeleo na maisha bora kwa Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la kuwa na Sheria mpya ya Watu Wenye Ulemavu. Muswada ulio mbele yenu, unakusudia kutunga Sheria ya Watu Wenye Ulemavu na kufuta sheria zifuatazo. Kwanza, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Uangalizi na Matunzo) Sura Na.183 *(The Disabled Persons (Care and Maintanance) Act, Cap. 183)* na pili Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Ajira) Sura Na.184 *(The Disabled Persons (Employment) Act, Cap. 184)* ambazo zimekuwa na upungufu wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sheria hizi haziendani na Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004, Sera ya mwaka ya 2007 na Maazimio na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia kwa mfano, viwango vya Kimataifa kuhusu haki na usawa kwa Watu Wenye Ulemavu na Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu na Mkataba wake wa nyongeza ambao uliridhiwa na Watanzania mwezi Aprili 2009.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Matunzo ya Watu Wenye Ulemavu, Sura Na.183 na Sheria ya Ajira kwa Watu Wenye Ulemavu, Sura Na.184 zilitungwa mwaka 1982. Tangu kipindi hicho, ni takriban miaka 28 ambapo kumetokea mabadiliko mengi ya kisera na kisheria ambayo yanakinzana na yaliyomo kwenye Sheria za sasa na hivyo kupitwa na wakati. Mabadiliko haya ni pamoja na kupitishwa kwa Sera ya Taifa na Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2008 ambayo imezingatia maendeleo ya usawa na fursa kwa Watu Wenye Ulemavu. Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza fursa sawa za upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi. Kupitishwa kwa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini mwaka 2004 ambayo inakataza ubaguzi na kuachishwa kazi kwa mwajiriwa kutokana na ulemavu wake. Aidha, Tanzania kukubali viwango vya Kimataifa kuhusu haki na usawa kwa Watu Wenye Ulemavu na kuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Watu Wenye Ulemavu pamoja na Mkataba wa Nyongeza ambao uliridhiwa na Bunge letu Tukufu tarehe 24 Aprili, 2009.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni, kutungwa kwa Sheria mpya ya Watu Wenye Ulemavu ili kurekebisha upungufu uliojitokeza katika Sheria zilizopo hadi sasa na vile vile kwa kuzingatia kwamba kuna mabadiliko mbalimbali yaliyojitokeza. Upungufu uliopo katika Sheria za sasa ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Sheria zinaweka sharti kwa mtu mwenye ulemavu kujisajili ili apate haki mbalimbali kwa mujibu wa sheria;

(b) Sheria zinaelekeza kuwa kila mwajiri mwenye waajiriwa zaidi ya 50 na kuendelea atenge asilimia mbili ya ajira yote kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Hata hivyo, Sheria hizo hazitoi sharti au hitaji la mwajiri kutoa taarifa ya idadi ya watu wenye ulemavu aliowaajiri;

(c) Sheria haitoi nafasi ya kuwalinda waajiriwa wenye ulemavu dhidi ya kupunguzwa kazi pindi zoezi hilo linapotokea;

(d) Sheria zinazingatia masuala ya ajira na matunzo pekee, masuala mengine ya kijamii mfano ujongeaji, nyenzo za kujimudu, lugha za alama na michezo hayajawekwa;

(e) Suala la haki na fursa kwa Watu Wenye Ulemavu halikupewa nafasi katika Sheria hizi;

(f) Misamiati iliyotumika kwenye Sheria hizi imepitwa na wakati;

(g) Sheria hazielekezi utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu kwa kuzingatia utengamano wa kijamii yaani *community base rehabilitation;*

(h) Wajibu wa Serikali kwa Watu Wenye Ulemavu hauko bayana;

(i) Sheria haielekezi namna jamii inavyoshirikishwa katika kuhudumia Watu Wenye Ulemavu;

(j) Tafsiri ya ulemavu na mtu mwenye ulemavu iko ya tiba zaidi yaani *medical* badala ya kijamii yaani *social;*

(k) Sheria zinaelekeza mashtaka dhidi ya waajiri yapate ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka; na

(l) Makosa na adhabu zilizoainishwa hazilingani na hali ya sasa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ndani ya Muswada huu ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya 2004 ambayo inasisitiza haki na usawa wa fursa;

(b) Kuzingatia Sera ya Afya ya 2007 inayoelekeza kuwepo kwa mfumo wa kisheria na fursa sawa katika utoaji na upatikanaji wa huduma za afya nchini;

(c) Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu;

(d) Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu;

(e) Kuweka taratibu na wajibu wa utoaji haki kwa Watu Wenye Ulemavu;

(f) Kuweka muundo utakaoruhusu mchangamano wa Watu Wenye Ulemavu katika jamii na vyombo vya usafiri;

(g) Kuweka utaratibu wa upatikanaji wa huduma za afya, elimu, utengamano na ajira kwa kuondoa sharti la ulazima wa kujisajili ndipo Watu Wenye Ulemavu waweze kuruhusiwa kupata haki hizi;

(h) Kuweka utaratibu utakaoruhusu ujongeaji (*accessibility)* kwenye majengo na huduma mbalimbali za umma;

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa haki na usawa wa fursa katika nyanja zote za maisha kwa watu wenye ulemavu;

(j) Kuhakikisha ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika masuala ya kijamii, kiuchumi na siasa;

(k) Kuanzisha Daftari la Watu Wenye Ulemavu litakalotoa takwimu sahihi zitakazosaidia kupanga mipango ya maendeleo;

(l) Kuanzishwa Baraza la Taifa na Kamati za Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu katika ngazi ya Kijiji, Mtaa, Halmashauri na Mikoa;

(m) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu ambapo vyanzo vyake vya mapato vitatokana na fedha itakayotolewa katika bajeti ya Serikali, misaada ya wadau wa maendeleo, michango ya taasisi, watu binafsi na vyanzo vingine halali vya mapato; na

(n) Kuainisha makosa mbalimbali na adhabu zake kutokana na kukiukwa kwa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 12 kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza, inatoa masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Muswada na ufafanuzi wa maeneo yaliyotumika katika Muswada huu.

Sehemu ya Pili, inatoa sababu za Muswada, misingi, wajibu wa namna ya kupatikana kwa haki za Watu Wenye Ulemavu, usawa na kutobaguliwa; Haki ya usawa katika kupata haki na kulinda pamoja na kuhamasisha jamii kushiriki katika kulinda haki za Watu Wenye Ulemavu.

Sehemu ya Tatu, inahusu mambo ya utawala. Sehemu hii inapendekeza kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Ushauri ambalo litakuwa linamshauri Waziri katika mambo yote yanayohusiana na haki za Watu Wenye Ulemavu na utekelezaji wake. Aidha, sehemu hii inaeleza madhumuni ya kuundwa kwa Baraza, kazi za Baraza, Wajumbe wa baraza na namna watakavyopatikana. Pia inapendekeza kuanzishwa kwa Baraza la Taifa na Kamati mbalimbali za kushughulikia haki na masuala ya Watu Wenye Ulemavu kuanzia katika ngazi ya Kijiji au Mtaa, Halmashauri hadi kufikia Mkoani.

Sehemu ya Nne, inaweka utaratibu wa namna ambavyo Watu Wenye Ulemavu wanaweza kujumuishwa katika kazi na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii ili waweze kuishi katika maisha ya kujitegemea kama watu wengine. Sehemu hii inatoa wajibu wa Serikali za Mitaa kujenga mazingira rafiki ili kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuwawezesha kuishi katika maisha ya kujitegemea. Pia sehemu hii inatoa wajibu kwa ndugu wa Watu Wenye Ulemavu kuwatunza na kutoa msaada wowote wa kijamii kwao ili kuhakikisha wanaweza kuishi katika maisha ya kujitegemea.

Aidha, sehemu hii inazuia mtu yeyote kumlazimisha mtu mwenye ulemavu kuishi katika kituo au sehemu yoyote ile asiyoipenda. Hivyo, inatoa hiari kwa mtu mwenye ulemavu kuchagua mahali pa kuishi ikijumuisha katika Kituo cha Watu Wenye Ulemavu ili mradi hakiuki Sheria yoyote ya nchi. Aidha, inatoa wajibu kwa Serikali za Mitaa au Taasisi yoyote kumtunza mtu mwenye ulemavu ikiwa hana ndugu wa kumtunza.

Sehemu ya Tano, inatoa wajibu na mwongozo kwa Serikali za Mitaa juu ya namna ya kutoa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu hasa baada ya Serikali kufungamanisha huduma za ustawi wa jamii katika ngazi ya Halmashauri.

Sehemu ya Sita, inaweka utaratibu wa kuwasajili Watu Wenye Ulemavu ambapo Kamishna wa Ustawi wa Jamii ataainisha aina ya taarifa zitakazotakiwa kuingizwa katika regista. Aidha, sehemu hii inazuia mtu mwenye ulemavu kuondoa jina hilo katika regista na pia itatumika katika utambuzi tu na haitakuwa msingi wa kutoa haki kwa watu wenye ulemavu.

Sehemu ya Saba, inaainisha kuwa Watu Wenye Ulemavu wana haki ya kupata huduma za afya, elimu, huduma ya utengamao na ajira. Aidha, sehemu hii inazitaka taasisi zinazotoa huduma za afya na wataalamu wa huduma za utengamao kupata mafunzo yanayohusu namna ya kutoa huduma kwa kundi hili. Vile vile sehemu hii inazuia ubaguzi wa aina yoyote ile kwa Watu Wenye Ulemavu katika kupata huduma za jamii kwa mfano kuandikishwa katika shule au kupata ajira.

Sehemu hii inatoa wajibu kwa kila mwajiri mwenye watumishi 20 na kuendelea kuajiri asilimia tatu ya Watu Wenye Ulemavu wenye sifa husika na kutoa taarifa mara moja kwa mwaka kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii. Pia inashawishi waajiri kutowaachisha kazi waajiriwa wenye ulemavu wakati wa zoezi la kupunguza wafanyakazi. Aidha, inamtaka kila mwajiri kuweka mazingira mazuri yatakayomwezesha mtu mwenye ulemavu kufanya kazi zake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Sehemu ya Nane, inapendekeza masharti yanayohusu ujongeaji, huduma, upataji taarifa na mazingira (*physical environment)*. Sehemu hii inataka majengo yote yaliyopo na yatakayojengwa pamoja na sehemu za utalii zinazotoa huduma kwa jamii, ziwe na ujongeaji. Pia inapendekeza kuwe na mfumo wa lugha husika ya kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kupata taarifa sawa na watu wengine wasio na ulemavu. Aidha, sehemu hii inapendekeza kuhakikisha kuwa kila taasisi inayotoa huduma za jamii, kuhakikisha kuwa huduma hizo zinazotolewa zitawafikia kirahisi Watu Wenye Ulemavu. Pia inaweka utaratibu wa kupokea na kuchunguza malalamiko ya Watu Wenye Ulemavu. Sehemu hii inaainisha kwamba itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumzuia mtu mwenye ulemavu kuingia katika jengo lolote la umma.

Sehemu ya Tisa, sehemu hii inahusu ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika siasa na maisha ya jamii. Sehemu hii inaainisha haki za Watu Wenye Ulemavu kushiriki katika siasa kama vile kupiga kura, kuchaguliwa na kushiriki katika maisha ya jamii. Aidha, inatoa haki ya kushiriki katika maisha ya utamaduni bila ubaguzi wowote ule. Hivyo, kunakutaka mfumo wa mawasiliano ambao utawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli hizo uwekwe. Aidha, sehemu hii inampa mamlaka Kamishna wa Ustawi wa Jamii kuzisimamia na kuzitaka taasisi zote zinazotoa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu kutoa taarifa kila baada ya miezi mitatu au kadri itakavyoziagiza ili kuhakikisha fedha na misaada zinawafikia walengwa.

Sehemu ya Kumi, inahusu vipindi vya televisheni na huduma za simu kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu. Sehemu hii inazitaka televisheni zote kuwa na mfumo wa lugha au tafsiri ya vipindi vya televisheni au kuwa na vipindi maalum kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu ili kuwawezesha kupata taarifa zote muhimu za Kitaifa. Aidha, watoa huduma

za simu pia wanatakiwa kuwa na muundo wa vifaa na simu rahisi kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu ili kuwawezesha kuwasiliana na watu wengine.

Sehemu ya Kumi na Moja, inahusu masuala ya fedha. Sehemu hii inaanzisha Mfuko wa Taifa kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu ambao utatumika katika kutoa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu katika kuwasomesha ngazi mbalimbali za elimu ikijumuisha elimu ya ufundi, utafiti na kadhalika. Aidha, sehemu hii inaainisha vyanzo vya mapato ya mfuko ikijumuisha ruzuku kutoka Serikali Kuu, wahisani, michango ya watu binafsi na vyanzo vingine halali vya mapato. Mfuko huu utakuwa chini ya usimamizi wa Baraza la Ushauri la Taifa la Watu Wenye Ulemavu na utakaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali.

Mwisho, Sehemu ya Kumi na Mbili, sehemu hii inajumuisha mambo mbalimbali ya kiutendaji na taratibu zake kama vile Maafisa walioidhinishwa kuingia katika majengo kuchunguza utekelezaji wa sheria hii ikiwa ni pamoja na kumpa uwezo Waziri mwenye dhamana kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii. Pia Sheria hii inapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Ungalizi na Matunzo) Sura Na.183 na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Ajira) Sura Na.184. Aidha, Muswada umejumuisha majedwali yatakayotumika katika utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, kwa heshima na taadhima, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wajadili Muswada ulio mbele yao na kuuridhia hatimaye kupitisha na kuwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu 2010 *(The Persons With Disabilities Act 2010).*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa ufafanuzi mzuri sana wa Muswada huu muhimu sana katika maisha ya Watanzania wengi. Kama ilivyo kawaida na kanuni, nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ili tuweze kupata maoni ya Kamati yake kuhusu Muswada huu.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii yanayohusu Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, 2010 *(The Persons With Disabilities Act, 2010).*

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wa mwaka 2010 *(The Persons With Disabilities Act, 2010),* sasa umekamilisha historia ndefu ya

kuwa na Sheria moja ya Watu Wenye Ulemavu na hivyo kufuta Sheria mbili zilizokuwepo ambazo ni:-

- Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Uangalizi na Matunzo) Sura Na.183 *(The Disabled Persons (Care and Maintenance) Act, Cap.183;* na

- Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Ajira) Sura ya 184 *(The Disabled Persons (Employment) Act, Cap.184*.

Mheshimiwa Spika, Sheria hizi mbili zimekuwepo kwa miaka 28 na hivyo kwa vigezo vyovyote na kwa hakika zimepitwa na mabadiliko mengi na haziendani na Sera ya Taifa ya Maendeleo kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004, Sera ya Afya ya mwaka 2007 pamoja na Maazimio na Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki na Usawa kwa Watu Wenye Ulemavu kama ambavyo Bunge hili lilivyoridhia Aprili, 2009.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaafiki kuwa Bunge lako Tukufu katika kikao hiki cha leo tarehe 13/4/2010 ikiwa ni mwaka mmoja tangu liliridhie Mkataba wa Kimataifa wa Watu Wenye Ulemavu, sasa likamilishe Historia ya kuwa na Sheria moja kwa kundi hili la Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kufikia hatua hii muhimu na ya kihistoria, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu. Aidha, kwa namna ya pekee, nazipongeza Taasisi zote zilizojihusisha na kukusanya mawazo tangu hatua za awali hasa zile za Watu Wenye Ulemavu na Tume ya Kurekebisha Sheria, kwa tafiti zake na kwa kushirikisha jamii ya Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia, nitambue umuhimu wa wadau mbalimbali ambao nao katika hatua za mwanzo, wamekuwa mstari wa mbele katika kuwa na Sheria moja ya Watu Wenye Ulemavu. Asasi na wadau ambao wameshiriki kwa namna mbalimbali na baadhi yao kufika mbele ya Kamati ni:-

- Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA);
- *Disabled Organization for Legal Affairs and Social Economic Development (DOLASED);*
- Kamati ya Taifa ya Usalama Barabarani kwa Watu Wenye Ulemavu;
- Chama cha Walemavu Tanzania (CHAWATA);
- Mkukuta *Disability Network (MDN);*
- Chama cha Maalbino Tanzania *(TAS);*
- Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA);
- *Tanzania Society for Blind (TSB);*
- *The Foundation for Civil Society;*
- Sauti ya Wanawake Wenye Ulemavu Tanzania (SWAUTA);
- Chama cha Watu Wenye Ulemavu wa Akili *(TAMH);*
- *Legal and Human Right Centre;*
- *Tanzania League for the Blind (TLB);*

- *Action on Disability and Development (ADD); na*
- *Tanzania Users of Psychiatric Organization (TUPO).*

Mheshimiwa Spika, baada ya Muswada huu kupitishwa rasmi na Bunge na Mheshimiwa Rais kuukubali kuwa Sheria, Kamati inatoa maoni ya jumla kwa Serikali katika maeneo yafuatayo:-

- Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha kwa Idara ya Ustawi wa Jamii chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii;

- Halmashauri zijengewe uwezo wa kifedha na rasilimali watu ili Sheria hii iweze kutekelezwa ipasavyo katika kutoa haki za Watu Wenye Ulemavu;

- Asasi zisizo za Kiserikali na taasisi za habari zijumuishwe katika utoaji wa elimu juu ya haki za Watu Wenye Ulemavu ili kuondoa mila na dhana potofu katika jamii dhidi ya Watu Wenye Ulemavu;

- Tunaishauri Serikali kuwa masuala ya Watu Wenye Ulemavu sasa yawe masuala MTAMBUKA na hivyo yajumuishwe katika kila mipango ya Serikali na hasa katika bajeti za Wizara zote, Idara na Mamlaka mbalimbali; ni vizuri hapo baadaye masuala haya Mtambuka yakawa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama vile masuala ya UKIMWI yalivyo sasa hivi;

- Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Kimataifa na za Kitaifa kuunda Mfuko Maalum wa Kusaidia Watu Wenye Ulamavu; na

- Kutokana na ajali nyingi zinazowakumba Watu Wenye Ulemavu, Serikali na Mamlaka husika zihakikishe kuwepo kwa alama maalum barabarani zinazowatambulisha Madereva muda wote kuwa na TAHADHARI ili kulinda usalama wa Watu wenye Ulemavu wanapovuka barabara kwa kuzingatia usalama wa makundi ya Watu Wenye Ulemavu wa Viungo, Macho, Kutokusikia, Ulemavu wa Ngozi ya Mwili usiohimili mwanga mkubwa wa jua *(Albino)* na Watu Wenye Ulemavu wa Akili kama inavyosisitizwa kwenye Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu (2004, Ibara ya 3 (17).

Aidha, tunaishauri Serikali ishirikiane na mbunifu wa Alama hizi Tano, Ndugu Jitoram Kabatele ambaye yuko hapa leo. Ubunifu wake umeanza kufikiriwa na wenzetu kule Uganda. Sasa ni vizuri kujua, ubunifu usiwe Tanzania halafu matumizi yawe Uganda. Tunaomba Serikali ishirikiane na mbunifu huyu Jitoram Kabatele ambaye amebuni Alama hizi Tano maalum kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa vifungu vya Muswada, Kamati ilipitia Sehemu na Vifungu vya Muswada na kuishauri Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu kurekebisha maneno, sentensi na jedwali la marekebisho liletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Marekebisho yalioainishwa na Kamati ni kama yafuatayo:-

Katika Kichwa Kirefu cha Muswada *(Long Title)* kuongeza maneno '*and protection'* ili kuweka msisitizo wa Muswada husika na kisomeke kama ifuatavyo:-

"*An Act to make provisions for the health care, social support, accessibility, rehabilitation, education and vocational training, communication, employment or work, promotion and protection of basic rights for the persons with disabilities and to provide for related matters".*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza vifungu vifuatavyo viangaliwe:-

- Kifungu cha 3, kufuta neno *parent* katika tafsiri ya neno *relative* kwa sababu mtu huyu anatakiwa kuwajibika moja kwa moja;

- Kifungu cha 3, kwenye tafsiri ya neno *social support* neno *provided* liondolewe ili kuleta maana kusudiwa;

- Kifungu cha 3, *Minister* lisomeke: "*The Minister responsible for the rights of persons with disabilities".* Tafsiri hii itasaidia kuendana na mabadiliko yanayoweza kutokea mara kwa mara;

- Kifungu cha 3, neno *Discriminate* tafsiri yake iendane na tafsiri iliyopo kwenye *Convention on the Rights of Persons with Disabilities na Settlement* badala ya kupewa tafsiri kwenye kifungu cha tafsiri lipewe tafsiri pale lilipotumika;

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya Pili, katika Kifungu kipya cha 4(g) ambacho kitasomeka *'provide adequate standard of living and social protection'.* Hii ni kwa kuzingatia kwamba mtu atafurahia haki zake pale tu ambapo haishi katika mazingira magumu *(degrading condition);*

- Kifungu cha 6, Kamati inaona kuna kujirudia kwa maneno ambayo hayana msingi na kushauri kifungu cha 6(a) maneno *all persons with disabilities* yaliyoko katika mstari wa pili yaondolewe na isomeke …*under this Act, and that they are fully entitled;*

- Kifungu cha 6(c), mstari wa tatu, neno *is provided* lisomeke *are provided* ili kuweka lugha sawa; na

- Kifungu cha 6(c) maneno *of all ages and genders* yaondolewe na kusomeka *of all genders* ili kuleta maana nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tatu. Katika Kifungu cha 12(1) kiongezwe kifungu kipya katika kazi za Baraza ambacho tunashauri kisomeke: "*To monitor and evaluate the implementation of this Act in relation to the Convention on the Rights of the Persons with Disabilities"* ili kulipa Baraza jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezai wa Sheria hii kufuatana na matakwa ya Mkataba wa Watu Wenye Ulemavu ambao Tanzania imesaini; Kifungu cha 12(2)(a), kuongeza maneno *and inclusion* baada ya neno *integration*. Kifungu cha 12(d) na (e) neno *the* mwanzoni mwa vifungu hivyo yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya nne, Kifungu cha 18(2), Kamati inapendekeza kufuta maneno *Council Committee* na badala yake kusomeka *Council or Local Government Authority or Respective Settlement;*

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tano, Kifungu cha 21(1) neno *medical case* lisomeke *medical care* ili kuleta maana tarajiwa. Kifungu cha 21(1), kuongeza maneno as *well as to the relevant authorities* baada ya neno *authority*.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya saba, kifungu cha 27(1) kufuta neno *if relevant* kwa sababu linakinzana na Ibara ya 24 ya *Convention on the Rights of Persons with Disabilities*. Kifungu cha 27(1) maneno *of all ages and genders* yaondolewe na kusomeka *of all genders* ili kuleta maana nzuri zaidi. Kifungu cha 31(1), kufuta neno *fit for a person with disability* ili kuepuka ubaguzi wa ajira kwa watu wenye ulemavu.

Katika Kifungu cha 31(2) kufuta neno *fifty* na badala yake kuandika *twenty*. Kifungu cha 31(4), kufuta neno *quarterly* na badala yake kuandika neno *annual*. Taarifa iwe inatolewa kila baada ya miezi sita na iwe mara mbili kwa mwaka (semi *annual and annual reports)*. Hii itasaidia Kamishna/Serikali kujua utekelezaji wa Sheria hii kwa kila mwajiri.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 33(1) kufuta neno *treat* na badala yake kuandika neno *discriminate* na pia kufuta neno *different*.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya nane, kifungu cha 35 neno *physical environment* lisomeke *built environment* ili kuondoa maeneo ya asili ambayo sio rahisi kuyachukua. Kifungu hicho hicho cha 35, neno *buildings* lisomeke *infrastructure* ili kujumuisha maeneo ya usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya kumi na mbili, kifungu cha 61(d) kufuta neno *assertive* linalojitokeza kabla ya neno *devices* na badala yake kuandika neno *assistive*. Kifungu cha 62(1)(ii) kuongeza maneno *or two years imprisonment or both*.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Sehemu ya Madhumuni, Kamati imeona maeneo yafuatayo yafanyiwe marekebisho japo hayaingii kama sehemu ya Sheria:-

Katika ukurasa wa 53 na 54, madhumuni ya Muswada, maneno yaliyojirudia yarekebishwe.

Sehemu zilizopo kwenye Muswada na zile za kwenye Madhumuni ya Muswada kuanzia Sehemu ya Tisa ya Muswada haziendani na zile za kwenye madhumuni ambapo Sehemu ya Tisa ya Muswada inaongelea kuhusu vipindi vya televisheni, huduma za simu, posta na Forodha kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu wakati kwenye Madhumuni inaongelea kuhusu ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika siasa na maisha ya jamii.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya tunamuachia Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii atayaleta katika Jedwali la Marekebisho na haya mengine ambayo tumeyasema.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni matumaini ya Kamati kuwa baada ya Muswada huu kuwa Sheria, Serikali itaweka utaratibu mzuri kwenye Kanuni ili Sheria hii iweze kueleweka kwa wananchi na inapowezekana tafsiri ya Kiswahili ni muhimu kwa jamii katika kuleta ufanisi wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa, Muswada huu umebeba maoni mengi ya wadau na bila shaka utakapokuwa Sheria kamili, mabadiliko ya kweli yatadhihirika katika maisha ya Watu Wenye Ulemavu. Pia tunaishauri Serikali kuwa, wakati wa utekelezaji wa sheria hii, Kanuni zitakazotungwa ni muhimu zizingatie maoni ya Wadau na endapo kuna maeneo yanayohitaji marekebisho, Serikali isisite kuleta mabadiliko mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Naomba sasa nichukue nafasi hii, kumshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Prof.David H. Mwakyusa, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dr. Aisha O.Kigoda, Katibu Mkuu Ndugu. Blandina S.J Nyoni na Wataalam wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr.Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M.Hemed, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Susan A.J.Lymo, Mheshimiwa Haroon Ali Suleiman, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame,

Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Oscar R. Mukasa na mimi Omar S. Kwaangw'

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashilillah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John na Ndugu Asia Minja kwa kuratibu vikao vya Kamati hadi maoni haya kutoka katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nimalizie kwa kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Babati Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano na imani yao kwangu. Nawashukuru sana. Naunga mkono Muswada na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kwaangw', uzoefu wako ni msaada mkubwa, Kamati imechambua vizuri sana Muswada huu. Sasa ni zamu ya Kambi ya Upinzani kutoa maoni, simuoni Waziri kivuli Dr. Ali Taarab Ali kwa niaba yake Mheshimiwa Omar Ali Mzee atatoa maoni ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. OMAR ALI MZEE – NAIBU MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa sheria ya watu wenye ulemavu wa mwaka 2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya watendaji katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuandaa Muswada huu na kuuwasilisha hapa Bungeni. Aidha, nitoe shukrani kwa Viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid pamoja na Dr. Willbrod Slaa kwa kazi yao kubwa ya kuhakikisha kuwa Wasemaji wote wa Wizara tunatimiza matakwa ya Kanuni za Bunge kwa wakati na kuwa hotuba za Kambi zimeandaliwa kwa viwango na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pia shukrani kwa asasi zote za kiraia na wananchi wote ambao wamekuwa wa msaada mkubwa katika kutimiza majukumu yangu nikiwa Waziri kivuli katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Muswada. Katika Sehemu ya Tafsiri, inazungumzia kuwa Waziri, ni yule atakayekuwa akishughulikia masuala ya Afya kwa wakati huo. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani, kwa kuzingatia upana wa shughuli hasa za "*Rehabilitation*", inatakiwa Shughuli za watu wenye ulemavu ziwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii itasaidia katika utekelezaji wa shughuli zilizotajwa chini ya kipengele cha Tafsiri ya shughuli za *Rehabilitation*, vinginevyo uratibu wa shughuli hizo chini ya Wizara moja utakuwa mgumu sana.

Katika kifungu cha 3 kinachohusu tafsiri ya maneno, maneno "*positive discrimination*" yametumika. Kambi ya Upinzani inaona maneno hayo kutumika katika Muswada si sawa kwani "ubaguzi au unyanyapaa" au uwe ni chanya au hasi ni ubaguzi tu, na hivyo linaondoa dhana nzima ya usawa. Kambi ya Upinzani ina hakika, ndugu zetu wenye ulemavu wanao uwezo mkubwa, wanachohitaji kuwezeshwa na kupewa nafasi, lakini siyo kupewa upendeleo kwa sababu ya ulemavu. Shirika la Umoja wa Mataifa, ILO limeeleza wazi kuwa watu wenye ulemavu, mathalan wa macho wana aina 47 za kazi wanazoweza kuzifanya, ikiwa ni pamoja na kuendesha ndege ya masafa marefu, lakini mazingira lazima wapate nafasi ya kutosha ya Elimu na kuondoa unyanyapaa unaoweza kuwanyima fursa na kadhalika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika kusisitiza hoja yetu hiyo kifungu cha 6(c) kinasisitiza kuwa nanukuu " *The Government shall for purpose of promoting equality and elimination of all forms of discrimination, take all appropriate measures to ensure that reasonable changes is provided to persons with disabilities of all ages and genders".*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza sasa hiki kinachoitwa "*positive discrimination*" kinatoka wapi? Hivyo basi, tunaona tusiweke vitu vitakavyoleta unyanyapaa kwa ndugu zetu wenye ulemavu badala ya kuweka vitu vya kuwawezesha na kuwapa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(a) kinachosema kuwa nanukuu: "*The Government shall ensure that all persons with disabilities are equal under this Act,……….."*. Kambi ya Upinzani inaona kuwa sentensi hii inakosa ile dhana nzima ya watu wenye ulemavu kuwa sawa na wale wasio na ulemavu na hivyo inazidi kuwatenga walio na ulemavu. Haya sio madhumuni na sababu za utunzi wa Muswada huu wa Sheria. Suala siyo watu wenye ulemavu kuwa sawa kati yao wenyewe, bali ni wao kuwa sawa na binadamu mwingine yeyote katika jamii, kwani ulemavu haupunguzi ubinadam wa mtu. Tofauti ya mahitaji inayotokana na ulemavu ndiyo jambo linalohitaji kushughulikiwa kufuatana na aina ya ulemavu na mahitaji maalum ya ulemavu huo.

Mheshimiwa Spika, Katika kifungu cha 16 kinachosema kuwa jamaa wa mtu mwenye ulemavu ndio wanaotakiwa kutoa "*social support".* Aidha, kifungu cha 17 kinabainisha pale ndugu na jamaa wanaposhindwa kufanya hivyo, Mahakama imetoa miongozo ya jinsi malipo ya kila mwezi *"monthly payment"* yatakavyofanyika katika mchakato mzima wa mlemavu kupata hiyo *"social support*".

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa watu wenye ulemavu wengi wanatoka na wapo katika familia zinazoishi vijijini na familia hizo ni maskini na hata zile zinazoishi mijini ni masikini pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua hali halisi ya maisha zinavyoishi familia nyingi wanamoishi walemavu ndio maana ikaweka kifungu cha 14 katika Muswada huu. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ionyeshe, jukumu lake katika usaidizi wa kutoa *"social support".* Serikali isianze kukwepa majukumu yake ya msingi. Ikumbukwe kuwa watu wenye ulemavu wengi wako vijijini, au hata kama wako

mijini ni maskini, hivyo hata uwezo wa kufuatilia miongozo hiyo ya Mahakama watafanyaje kuipata. Kifungu hiki kikiachwa hivi hakitekelezeki na kitabakia kwenye vitabu tu, hadi pale Sheria itakapoweka mfumo mzuri wa haki hizo kupatikana Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19 cha Muswada kinahusu uundwaji (*formulation*) wa program, ambapo Waziri mwenye dhamana kwa mashauriano na Baraza la Ushauri la Watu Wenye Ulemavu, pamoja na Mawaziri wengine ndio watаunda (*formulate*) *program*. Wajumbe walemavu ni wawili tu katika Baraza zima, ambapo kati ya wajumbe wapatao 12 watu wenye ulemavu wanawakilishwa na mjumbe mmoja tu kutoka kwenye Chombo chao *(umbrella organization/apex organization).* Serikali siku zote imekuwepo, kilichokosekana ni ushirikishwaji wenye tija wa walemavu wenyewe na sheria hii inaelekea kurudia makosa hayo hayo. Wadau walipendekeza washiriki kutoka Vyama vya Watu Wenye Ulemavu waongezeke kama wajumbe na pia Vyama vya Kuhudumia Walemavu na Vyama vya Haki za Binadamu washirikishwe kikamilifu. Vinginevyo chombo kinachoundwa na Sheria hakina tofauti na Idara ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa makosa ambayo yamekuwa yakitokea hapa nchini yanaendelea kutokea, kwani kutowashirikisha wahusika katika utayarishaji wa program zinazowahusu wao katika utekelezaji wake ni kosa kubwa. Watu wenye ulemavu wanazo jumuiya na vyama vyao hivyo na wao wanatakiwa kuwa sehemu ya uandaaji wa program zinazowahusu, hivyo na wao kuwa sehemu ya program *hizo (bottom up kind of programmes and not top down kind of programmes).* Hii itafanya umiliki (*ownership*) wa mipango au pragram hizo uwe wa watu wenye ulemavu wenyewe au mmoja mmoja au kupitia vyama na vyombo vyao.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 33, dhana nzima ya kifungu hicho ni kumtaka mwajiri kuzuia ubaguzi wa aina yoyote ile katika mchakato wa ajira na kazi kwa mtazamo mpana kati ya watu wenye ulemavu na wale wasio na ulemavu. Aidha, kifungu cha 34(1), vifungu vidogo vya (c), (d), (e) na (f) vinamtaka mwajiri kuweka mazingira ya utofauti kwa watumishi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe maelezo, hivi hapa si mkanganyo baina ya vifungu tajwa hapo juu na huo si ndio ubaguzi wenyewe? Kwani sheria inamlazimisha mwajiri kuwabagua watumishi wenye ulemavu kutoka kwa wale wasio na ulemavu. Kambi ya Upinzani inaona ubaguzi wa aina yoyote ile hatima yake ni kuleta unyanyapaa na badala yake Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwe na uwezeshwaji lakini siyo kubaguliwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33(3), kinachohusu adhabu kwa watakaofanya kosa la ubaguzi au kunyanyapaa mtu mwenye ulemavu kuwa ni faini ya shilingi milioni mbili au kwenda jela kwa muda wa miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona litakuwa ni jambo la busara kama Muswada wa sheria utataja viwango vya chini na juu tu, mengingeyo Hakimu ndiye

atakayetoa adhabu stahili kulingana na uzito wa kosa lenyewe. Vinginevyo hakuna haja ya kwenda Mahakamani kwani adhabu inajulikana na inaweza kutoa nafasi kwa mtenda kosa kupima kabla ya kutenda kosa lenyewe kwa kuwa adhabu atakuwa anaielewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, Kambi ya Upinzani haina pingamizi lolote juu ya upitishwaji wa sheria hii, isipokuwa inataka ufafanuzi kwa hoja zilizotolewa na kuyafanyia marakebisho ambayo tumeyataja hapa juu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar Ali Mzee kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge katika hatua hii ninao wachangiaji tisa na nitakavyowataja si lazima niwaite kwa mtiririko huu kwa sababu lazima nizingatie hali yetu humu ndani. Kwa kuzingatia Upinzani, jinsia, Zanzibar na Bara. Lakini ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Janeth Kahama, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Aboubakir Khamis Bakar, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto.

Sasa tutaanza na Mheshimiwa Herbert Mntangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Kahama, lakini watatu nitapenda kumwita Mheshimiwa Aboubakar Khamis Bakar kwa mtiririko huo. Mheshimiwa Mntangi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa ili niweze kuchangia katika Muswada huu mzuri sana wa Sheria ya Walemavu. Lakini naomba nianze kwa kuwashukuru Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wake katika jitihada zao kuwezesha Muswada huu kukamilika. Lakini pia niwashukuru na kuwapongeza viongozi wa Jumuiya mbalimbali ya walemavu ambao wameweza kuhudhuria katika Mkutano huu leo. Wale waliopata nafasi ya kuhudhuria na hata wale wengine ambao kwa bahati mbaya hawakupata nafasi za kuhudhuria.

Mheshimiwa Spika, walemavu wako katika makundi mengi ambayo wengi tunayafahamu. Wapo walemavu wa viungo lakini wapo walemavu ambao hawaoni, lakini wapo wasiosikia, wapo wasioweza kuzungumza na wapo walemavu wa ngozi. Hawa wote kwa kimsingi ni walemavu na sheria hii imewalenga wote.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuwa na Sheria ya kuwathamini na kuwatambua walemavu. Haiwezekani katika nchi au katika Taifa ambalo kwa kweli linao walemavu lile Taifa likakaa kimya bila kutambua na kujali hali ya mazingira ya walemavu waliopo. Wapo walemavu ambao ulemavu wao ni wa kuzaliwa na hao ni wengi. Lakini vilevile wapo walemavu ambao hupata ulemavu baada ya kuishi japokuwa hawakuzaliwa na ulemavu. Wote kwa ujumla wanabaki kuwa walemavu.

Mheshimiwa Spika, walemavu ambao kwa kweli wanapata matatizo makubwa sana katika nchi hii na katika sehemu nyingi duniani ni wale walemavu ambao wamezaliwa katika familia au mazingira duni. Hawa wanapata matatizo makubwa sana. Nasema matatizo makubwa sana kwa sababu gani? Inawezekana katika baadhi ya familia ambako walemavu wengine wamezaliwa familia hizo zikawa na uwezo wa kuwasaidia walemavu wale. Kwa mfano, wale wa viungo, wazazi wanaweza kupata baiskeli zikawasaidia na wengine wakawa na hali kidogo ya afadhali.

Lakini wale wanaozaliwa katika familia duni hawa wanapata matatizo makubwa kupita kiasi. Wapo wasioweza kutembea, hawana msaada wowote hata vifaa vya kuwawezesha kutembea. Lakini wanaishi katika familia duni na familia zao hazina uwezo za kuwasaidia. Hawa wanapata shida kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, katika wiki mbili, tatu zilizopita kufuatwa na mlemavu mmoja katika Wilaya yangu ile ya Muheza katika kipindi ambacho kulikuwa na matatizo ya maji. Mlemavu huyu alikuwa anashindwa katika familia yake kupata maji. Lakini alifunga safari akanitafuta na alipokuja kunitafuta aliniomba msaada kwamba nimsaidie kumwajiria mtu wa kumsaidia kupata maji. Jambo hili ni zito na nisingeweza kuwa na uwezo wa aina hiyo, lakini nilipata uchungu kuona kwamba mlemavu yule anashindwa kujihudumia na familia haina uwezo wa kumsaidia.Maskini ya mungu yule atawezaje kuibeba ndoo ya maji kutoka katika eneo ambapo kisima kipo mita zaidi ya 500 kutoka mahali anapoishi. Maana yake ni kwamba siku akikosa mtu wa kumsaidia maana wapo watu wanaoweza kujitolea kujisaidia basi mlemavu yule anakaa bila kupata huduma ya maji. Hata kuoga na inawezakana hata chakula kinakuwa matatizo kwake. Hali nasema ni mbaya sana kwa walemavu hawa.

Mheshimiwa Spika, tuangalie na sisi wenyewe mazingira yetu kama Taifa. Tuna mazingira gani yanayoelekeza nguvu za kuwasaidia walemavu. Katazame na tembea katika shule zetu nyingi ambapo walemavu wanasoma. Shule za msingi na hata katika baadhi ya sekondari. Mazingira yaliyoko kule hayawapi nafasi ya walemavu kusoma vizuri. Wanashindwa kupanda katika ngazi kwa sababu shule hazikujengwa kwa mazingira ya kuwasaidia. Wanashindwa kufika shuleni kwa sababu hawana uwezo wa kusafiri kutoka katika maeneo yao kwenda katika shule zilizoko kilomita chache au kilomita mbili tatu kutoka katika nyumba wanazoishi.

Mheshimiwa Spika, tazama vile vile katika baadhi, nasema baadhi za ofisi za Serikali zimejengwa kwa namna ambayo haiwatambui wala haikuwathamini walemavu. Wanashindwa kuingia katika maofisi hayo kwenda kutafuta huduma maalum kwa sababu mazingira ya majengo hayawaruhusu kuweza kuingia kwa urahisi. Nashukuru sana Bunge letu liliona jambo hilo na katika mazingira mengi ya Bunge hili walemavu wanaweza wakaingia kwa urahisi na katika Bunge lile jipya hali imezingatiwa vizuri zaidi.

Lakini kuna maeneo mengine hata hapa katika Bunge kupanda kule juu na kwenda katika baadhi ya maofisi hawana uwezo na hawafiki kule. Kwa hiyo, wanapata

huduma kwa kuomba msaada wa wahisani wachache. Kwa hiyo, ni vema tukajiangalia na sisi wenyewe tukabadilisha mazingira ili tuweze kuwathamini na kuwasaidia walemavu.

Mheshimiwa Spika, hebu tutazame nini wenzetu katika baadhi ya nchi duniani wanafanya. Nilipata bahati ya kutembelea nchi ya Italia miezi miwili iliyopita na nilipata bahati na kupokelewa na wahisani wanaotazama makundi haya ya watu wasiojiweza. Walinitembeza katika vituo vyao zaidi ya 30 na nilishangaa kweli kweli. Wana maeneo na vituo maalum ambavyo vimetengwa kwa ajili ya kuwasaidia watoto ambao wazazi wao wamefariki wakiwa na matatizo ya UKIMWI na watoto hao kuwa na magonjwa hayo ya UKIMWI wanawalea, wanawasomesha na wanawasaidia katika kipindi kirefu sana cha maisha yao watoto hawa. Moja ya taasisi hiyo ya Italia imefungua kituo chake pale Mjini Tanga karibu na eneo la *Rasca Zone* na hivi ninavyozungumza wameshapokea watoto zaidi ya 20, wanawatunza na wanawalea pale.

Watoto ambao wazazi wao wamefariki kwa ugonjwa na wao wenyewe watoto wana maambukizi hayo ya UKIMWI. Kwa taarifa ni kwamba, taasisi hizi nyingi kwa mfano, hizo nilizozitembelea inayoitwa *Casarozeta Famigria Association* wako tayari kuisaidia Tanzania, wako tayari kusaidia ujenzi wa vituo hapa Tanzania, wako tayari kusaidia kuwalea watoto wa Tanzania. Pia wapo tayari kujenga vyuo vya kuwafundisha Watanzania namna ya kuwalea watu wenye ulemavu pamoja na kuangalia hawa waliopatwa na ugonjwa wa UKIMWI, wako tayari vile vile kusaidia kuweka kambi na kuwalea watu walioathirika na madawa ya kulevya na katika baadhi ya vituo ambavyo nimevitembelea wameweza kuwaweka watu kwa zaidi ya miaka mitatu, minne pale.

Walioathirika kwa mfano na madawa ya kulevya na wanakaa nao na wanawafundisha na wanawapa pango maalum ya huduma mpaka wanafikia mahali watu wale wanarejea tena katika hali yao ya kawaida. Baada ya hapo wanatoka katika kambi na kurejea katika jumuiya wanakoishi wananchi. Kwa hiyo, taasisi kama hizi zinapokuja na kuwa tayari kusaidia Tanzania, nawaomba Watanzania tuwe tayari kuwapokea na nitakuwa tayari kuifahamisha Wizara ya Afya, hawa wote ambao wako tayari kuanzisha taasisi hizo ili Wizara iweze kutoa utaratibu wa namna ya kupokea watu kama hao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania si kwamba hatuna makambi ya kuwalea watu wenye matatizo, yapo, lakini ni machache na yanahitaji kuongezwa na kuimarishwa. Hatuna mpango kama Taifa wa kuwekeza kwa walemavu.

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati, baada ya kutengeneza sheria, sasa tusije tukaiacha tu sheria na kanuni zake, lazima kama Taifa tujenge mfumo utakaoweza kusaidia kuwatambua na kuwasaidia na kuwalea walemavu waliopo.

Mheshimiwa Spika, nazishukuru sana baadhi ya taasisi hasa za dini na watu binafsi ambao wamejitolea sana kuwasaidia walemavu katika nchi yetu. Kule Muheza tuna taasisi kama *World Vision,* watu binafsi na taasisi za dini zimetoa baiskeli; mwaka jana wametoa baiskeli karibu 100 kwa ajili ya walemavu katika Wilaya ya Muheza, msaada mkubwa sana. Tunawashukuru sana. Tunawaomba na wale wengine ambao wana uwezo basi wakumbuke kuwasaidia walemavu hawa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ambayo baada ya kuitengeneza sheria hii, kwanza ni kutoa mafungo kwa watu ambao watakuwa wanawahudumia walemavu. Najua Wizara ya Afya wanatambua hilo, lakini hatuna mpango maalum wa kuwaandaa watu kwa ajili ya kukaa na watu wenye ulemavu na kuwasaidia. Kwa hiyo, lazima tuunde na tutengeneze mpango maalum wa kuwezesha kuwa na watu maalum watakaoweza kukaa na walemavu hawa.

La pili, ni kuongeza idadi ya vituo vitakavyowezesha kuwasaidia walemavu. Tulivyo navyo ni vichache, havitoshi, idadi ya walemavu ni kubwa sana na wanateseka sana. Tujitahidi kama Taifa kutambua hilo na tuongeze idadi ya vituo. Lakini, tutoe elimu kwa umma watu waache kuwanyanyasa walemavu. Bado watu wanaendelea kuwanyanyasa walemavu. Tutoe elimu kwa umma, jambo hili liachwe kabisa. Lakini, vile vile tujitahidi kufikiria uwezekano wa kutoa elimu ya bure hasa elimu ya afya na elimu kama ya msingi na sekondari na kuendedelea huko juu kwa ajili ya walemavu. Tuwe na mpango maalum. Tunao mpango nafahamu katika shule za msingi kuwasaidia watu wachache wasiojiweza, kweli hilo linafanyika, lakini tujenge mazingira mazuri ya uhakika kwamba kweli kama Taifa hilo linafanyika.

Mheshimiwa Spika, ni vema vile vile tukajitahidi kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya kuwasaidia au kusaidia miradi ya walemavu. Walemavu wengi wana uwezo wakisaidiwa, wana miradi ambayo wako tayari kuifanya na ukiwasaidia watafanya miradi yao. Tumewaona wengi wanafanya biashara hata za kuuza kadi za simu. Tumewazoea pale Bungeni Dar es salaam. Tunashukuru sana hizi kampuni za simu zimesaidia kuchangia kwa kiasi kikubwa kuwezesha walemavu kama wale kufanya biashara hizo. Wanakuja na baiskeli zao pale wanafanya, lakini wanahitaji kupewa mradi mkubwa, wanahitaji kupewa msaada ili kuwezesha miradi yao kuboreshwa. Uwezo wao ni mdogo na faida wanayopata kwa kadi moja anayouza ni ndogo haiwatoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuwasaidie ili waweze kupata miradi mikubwa, waweze kujitegemea si kwa kuuza kadi tu, wako wengine wenye uwezo mkubwa sana na wengine wana uwezo mkubwa sana hata wa kufanya kazi ofisini. Nashukuru sana sheria imetambua hilo na imeweka hata viwango vya kutambua na kuendelea kuwaheshimu na kuwapa nafasi ya kufanya kazi katika maofisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwamba tuangalie pia baadhi ya sheria zingine. Kwa mfano, imezungumzwa hapa Sheria ya Usalama Barabarani. Sheria hiyo inaangalia tu usalama wa barabarani na katika maeneo mengine zimewekwa hata alama za kuonyesha kwamba hapa wanyama wanapita, watoto wanapita, lakini hatufanyi lolote kuhusu walemavu. Lazima tuwe na mpango utakaowezesha katika baadhi ya maeneo hawa walemavu wasaidiwe kuvushwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Herbert Mntangi kwa mchango wako huo. Namwita Mheshimiwa Janet Kahama, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, halafu wakati huo ajiandae Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu. Kwanza kabisa, naomba kuishukuru Wizara hii na Serikali kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu ambao kwa kweli ungelikwishaletwa siku nyingi zilizopita, lakini hata hivyo umekuja, basi tunashukuru. Tunaomba kutoa pongezi zetu kwa Mheshimiwa Waziri Prof. Mwakyusa na Naibu wake na Katibu Mkuu na wengine wengi waliofanya na kushughulika katika maeneo haya ya kuiwezesha kazi hii kufika hapa leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ningeomba tuliangalie lile eneo la Baraza. Kwa upande wangu nakubaliana pia na wadau kuwa hili Baraza hebu tuongeze Wizara nyingine, tuongeze wajumbe kutoka Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya na pia kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani kama vile ulivyokwishasikia mwenzangu amezungumzia kuwa wanahitaji sheria, lakini pia sheria zinahitaji kufuatiliwa na Wizara hii itatusaidia sana katika kufuatilia. Lakini pia, katika kuangalia wajumbe, basi tufikirie kuwaongezea idadi ya wajumbe walemavu wenyewe tukizingatia sana jinsia.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya afya ya jamii, Serikali imekwishaazimia kuanzisha Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii na imeweka kabisa kuwa Halmashauri zitapewa wajibu wa kufuatilia na kusaidia na kulipia wale walio na uwezo mdogo. Sasa, kwa maana hiyo katika kipengele cha 26(3) hapo wameendelea wakaishia hapo, lakini hakuna mahali palipojitambulisha kuwa walemavu nao wako chini ya eneo hilo. Kwa hiyo, naomba tu kuwa liongezwe eneo la “D” ambalo litajumuisha kuwa walemavu nao wawe katika kipengele na kifungu hicho. Pia, ningeomba sana katika Bima ya Afya na kwa sababu Bima ya Afya iko chini ya Wizara hii, basi wakae, wafikirie sana uwezekano wa kuwafikiria sana hawa ndugu zetu walemavu kwa jinsi gani wataweza kuwasaidia katika kuwawezesha ili waweze kupatwa na kulindwa na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tumeona kuwa wengine wamekwishapata misaada ya baiskeli na pia wamekwishapata vifaa vya viungo bandia, vingine viko katika Karakana zetu Hospitali za *MOI*, *CCBRT*, lakini bado idadi yake ni ndogo, haitoshelezi na pia naona hata ubora wake bado haujatekelezwa vizuri, kwa sababu unaweza ukaona wakati mwingine wanapotembea kwa kweli huwa wanaumia. Unamwona kabisa mtu hata anapokaa, anakunja uso kuonyesha anapata maumivu. Kwa hiyo, ubora, tunaomba uzingatiwe. Lakini, haitoshi, bei ya viungo hivi pia ifikiriwe kwa sababu bei yake bado ni juu na siyo kila mmoja anaweza kulipia viungo hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nataka kuzungumzia kidogo kuhusu kulindwa kwa walemavu. Kulindwa kwa maana ya UKIMWI. Eneo la *HIV-AIDS* ni eneo pana na linatufunga sisi wote. Eneo hili tumeliangalia, lakini kwa upande huu wa ndugu zetu wenye ulemavu hatujaliangalia vizuri sana. Wao ni binadam kama sisi, wana hali ile ile

na maumbile sawa na sisi wote wengine na hata hivyo na sisi tuelewe kuwa ni walemavu watarajiwa. Kwa maana hiyo basi, kuna eneo unakuta mtu anakwenda kubaka mlemavu, hana *speed* ya kukimbia, hana uwezo wa kuinuka, hawezi kujitetea kwa aina nyingine na mwingine hawezi hata kuzungumza, kwa hiyo hata kupiga kelele hawezi akasikiwa na mtu yeyote. Kwa hiyo, tunaomba eneo hili liangaliwe sana, waweze kupatiwa mafunzo ya kuweza hata wao wenyewe kujikinga. Lakini pia tuangalie pale wanapopatikana waliotenda vitendo kama vya ubakaji, wanachukuliwa hatua gani kwa kuwabaka hawa ndugu zetu wenye ulamavu.

Mheshimiwa Spika, naomba tukumbushane, nafasi ya kuelimisha kama mwenzangu alivyosema, ni muhimu sana. Inabidi kwa kweli tukae tufikirie Serikali yetu na umma uelimishwe vizuri kuhusu hawa ndugu zetu wenye ulemavu ili tuweze kujua kuwa, kuwa mlemavu siyo tofauti na kuwa mtu asiyelemaa, kwani sisi ni jamii moja. Kwanza kabisa, kama unaweza kukumbuka, tulianza na mauaji ya wazee kama mnaweza kukumbuka, Mkoa wa Shinyanga wazee waliuawa kwa kutuhumiwa wengine kuwa ni wachawi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, tukaanza kuingiliwa kuchunwa ngozi maeneo ya Mbeya huko na sehemu nyingine. Tukanyamaza, hatukuweka vivutio vya kutosha kuwaelimisha watu wetu. Wakaendelea, wakafuata watu wenye vipara na humu tunao wengi katika Bunge hili. Sasa, ndugu zetu ma-*Albino* wameitamani ile ngozi nyeupe kwa kufanyia kafara zao mbalimbali. Sasa nasema, haya yote ni matokeo ya kutoelimisha watu wetu. Kwa hiyo, chonde chonde Serikali iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu eneo la usafiri, najua limekwishaguswa. Lakini hapa ingelifaa tuwafikirie, ulemavu ni wa aina mbalimbali; kuna mlemavu kwanza anayejiweza, anapata mshahara, anaweza akawa mfanyabiashara, kuna mwingine hawezi kabisa. Sasa unamtegemea huyu ambaye hana kipato kikubwa aweze kweli kuingia kwenye basi au kwenye treni au kwenye boti akilipa kiwango kile kile cha pesa ambacho watu wengine wanacholipa! Kwa upande huo naona haifai, bora tungeshuka tukawapa nusu ya kiwango kwa ajili ya nauli ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tukumbuke kuwa hawa ndugu zetu walemavu wengine wana watoto na wakati mwingine watoto wanapokuwa wadogo wanahitaji mtu wa kuwaangalia na kuhakikisha kuwa hawatoki hata nje wakaumizwa, wakagongwa na magari na kadhalika. Kwa hiyo, tuone kuwa kama Serikali inaweza ikaliangalia eneo hili na kutoa msaada wa aina yoyote kwa ajili ya watoto hawa, msaada wa matunzo, msaada wa elimu, msaada wa afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu mioundombinu. Tumekuwa na barabara nzuri, tunashukuru Mungu, hasa Dar es salaam na Mikoa mingine na hasa barabara za kuvuka kutoka Dar es salaam mpaka Mwanza lami. Lakini hasa nazungumzia barabara zilizo katika Miji. Mara nyingi inakuwa ngumu sana kwa ndugu zetu wakiwa katika baiskeli zao kuvuka barabara na mara nyingi tunaona wanaingia katika barabara ambazo magari nayo yanaingia. Kwa hiyo, tungeomba katika

miundombinu wafikirie kutenga eneo la pembeni katika sehemu nyingi ili na wao waweze kufaidi kupita huko wasije kupata ajali ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu alama za barabarani sitazungumzia kwa kuwa zimezungumzwa. Naomba nizungumzie alama katika mabasi, maboti na treni. Alama za watu kukaa, watu wenye ulemavu. Viti vitengwe, iwe ni sheria sasa kuwa vitengwe vitu na alama pale iwekwe ya picha ya mlemavu, picha ya mzee, picha ya mwanamke mjamzito, tuendelee kama wenzetu walivyoendelea nchi za nje, kwa sababu bila hivyo siku hizi maadili yamekwisha, unakuta mtu amekuja, mtoto mdogo amekaa hampishi mtu mzima, hampishi mlemavu. Kwa hiyo, tunaomba hilo lizingatiwe ili tuweze kupata alama kamili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niongelee tena katika miundombinu hiyo, ni kweli tumejitahidi kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa hapa, Bunge tumejitahidi. Lakini bado, tunahitaji hata wanapotembea, wapate ngazi za kukamata pembeni hasa vyooni anapokaa kwenye choo, kuinuka anainukaje bila kuwa na kishikio pembeni! Kwa hiyo, vitu kama hivyo tunaviona ni vidogo, lakini ni vitu muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana Serikali ijitahidi kwa sasa bila kuchelewa, hawa wanataka kusikia taarifa za habari, anayeweza kusikia, *alhamdulillah* atasikia, lakini kuna mwingine hawezi ila anafuata kwa alama na utakuta sehemu nyingine za nchi nyingine wanaziweka zile alama. Tusiweke alama tu siku ambapo kunatokea labda kipindi maalum, hapana, la hasha! Ningeomba katika na hasa maeneo ambapo tunakuwa na taarifa za habari, basi tuhakikishe kwamba tunapata watu ambao wanatumia alama hizi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuwawezesha kiuchumi, ingekuwa vema basi hata yale mabilioni yanayotengwa wakati mwingine yanaitwa mabilioni ya JK, basi yangefikiriwa angalau *percent* fulani wakapewa na pia wakapewa mafunzo ya ujasiriamali, mafunzo ya biashara ili na wao wawewe kuanzisha miradi itakayowakimu kimaisha.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali katika eneo la michezo kwani imejitahidi sana Serikali hii siku hizi,…. naona Mheshimiwa Bendera pale anapiga makofi amefurahi, maana yake hii inakwenda kwake na kwa Waziri wake,….wameshirikishwa vizuri sana katika michezo, tuzidi kuendelea kuwapa moyo katika eneo hilo na maeneo mengine ya kucheza dansi na mengine na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, sitaki kuchukua muda nipigiwe kengele ya pili; ni kuwa naomba kabisa kwa dhati tumshukuru sana Reginald Mengi, sijawahi kuhudhuria hafla hizi, lakini kwenye *TV* ninaona akiwakaribisha. Sasa, atakuwa ni Mengi, lakini wapo na wengine ambao wamekwishafanya vile. Basi kwa ujumla hao wenzetu waliojitolea kufanya hivi, basi tuwashukuru kwa hatua hiyo waliyochukua, ni *style* nzuri na ni moyo wa upendo wa kuwakaribisha wenzetu na kuwajali na kuwasaidia. Basi tunashukuru kwa hayo, Mwenyezi Mungu na wao awajalie na wao wawe na maisha

mazuri na tunawakaribisha wanapokuwa na manung'uniko mengine, watwambie ili tuweze kukaa na kuzungumza pamoja.

Mheshimiwa Spika, nasema ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Janet Kahama. Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji anayefuatia ni Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo, wakati huo Mheshimiwa Zuleikha Yunis Hajj ajiandae.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo kuhusu Muswada huu. Kwa ujumla Muswada ni mzuri na utasaidia kwa kiwango kikubwa sana. Uunaweza ukawasaidia hawa ndugu zetu ambao wana ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba nipitie baadhi ya vifungu ambavyo nahisi kidogo ama vinataka ufafanuzi au vinataka kuwekwa sawa ili kuboresha zaidi Muswada huu. Lakini, kabla ya hapo, kwa ujumla Muswada huu au suala hili ambalo tunalizungumza ni suala tunaloita ni mtambuka. Sasa kama suala ni *crosscutting*, nilikuwa sioni haja ya Wizara ya Afya kuwa ndiye mdhamini wa suala hili. Nafikiria mahala pazuri ingelikuwa ni *Prime Minister's Office* ambayo mara nyingi inashughulika na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, tukitoka hapo, naomba twende katika ukurasa wa 9 katika kifungu cha 4, wanasema *"the principles of this Act shall be….(*sasa kuna a, b, c ), sasa hii "b" wanasema ni *"non discrimination"*. Sasa nilikuwa najiuliza, *"non discrimination"* ya kitu gani? Kwa sababu hapa, kwa mfano "a" wamesema *"respect for human dignity, individuals freedom…..*(inaendelea)*…of persons with disabilities"* . Sasa, nilikuwa nafikiria na hapa *"non discrimination"* iendelee iseme *"of persons with disability"* ili kuiweka sawa sawa. Hivyo hivyo itarejea kwa kifungu kidogo cha 4(d) maana hapa wamesema *"equality of opportunity"*. Sasa *equality of opportunity* katika misingi gani? Kwa hiyo, nayo hiyo pia ningeomba iongezwe ili kufanya hii sentensi iwe nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika kifungu cha 4(f) wanasema *"equality between men and women with disabilities and recognition of their rights and needs"*. Sasa, hii nina wasiwasi kidogo kwa sababu kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 12(1) pale kinasema kwamba binadam wote ni sawa na binadam hapa wana-*include* hawa wenzetu wenye ulemavu. Sasa unapoweka kifungu hiki, je, kwa kanuni za kutafsiri haionyeshi kwamba sisi tunaona kwamba kama hawa wenzetu kidogo hawamo katika kile kifungu ambacho kimekuwa *covered* na Katiba? Hilo naomba nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 13, kifungu cha 11, wenzangu wamezungumzia kuhusu *composition* ya *council* hii. *Composition* hii nahisi kidogo ni mbaya. Ni mbaya kwa sababu moja kubwa; hapa inaonyesha dhahiri kwamba sisi tunafanya sheria ya kuwasaidia hawa wenzetu, lakini kwa mujibu wa kifungu hiki, inaonyesha dhahiri kwamba sisi tunawatenga. Kwa sababu *composition* yote hii, kuna mtu mmoja tu ambaye ni mlemavu. Je, sasa tunaweza tukajiuliza, wao katika *council* hii

watakuwa hawawezi kusema, hawawezi kuchangia au hawawezi kufanya kitu gani? Sasa, nahisi kwamba *council* hii *composition* yake ni vyema ikarekebishwa ili na wao wajione kwamba wamo katika kushughulikia masuala yao.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 18, kifungu cha 20, hapa wameweka kazi za *Local Government Authorities* ambazo wanasema ni *"to safeguard persons with disability"*. Halafu kifungu cha 20(1) na (2) wanasema: *"A Local Government Authority shall have the duty to safeguard and promote the welfare of persons with disabilities within its areas of jurisdiction"*. Sasa, kifungu hiki kinaonyesha kwamba *Local Government Authority* inalazimishwa, ni *mandatory* hapa.

Sasa, naomba Mheshimiwa Waziri anielezee, kifungu hiki kwa lugha za wenzetu wanasema ni *justiceable*, yaani ikiwa mlemavu hakupata haki hii kutoka kwa *Local Government Authority*, je, mlemavu huyu anayo haki ya kwenda mahakamani kushtaki na kusema kwamba *Local Government Authority* ya *area* yake haikumtendea haya? Kwa sababu hii ni sheria ambayo *Local Government Authority* imekwishapewa ulazima kwa mujibu wa sheria. Sasa je, ikiwa mlemavu hakufanyiwa hivi anaweza kwenda mahakamani?

Mheshimiwa Spika, suala hilo hilo liko katika ukurasa wa 19, kifungu cha 22(1) na kifungu cha 22(2) ambapo hapa inaonyesha *responsibility of Local Government Authorities*. Je, *responsibilities* hizi ambazo zimewekwa hapa, ikiwa hazikutekelezwa na ndugu yetu mlemavu akaona kwamba amenyimwa haki yake kutokana na kifungu hiki, anayo haki ya kwenda mahakamani kudai?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 20, kifungu cha 26(1) na (2) wanasema kwamba *"every person with disability shall have the right to enjoy the attainable standard of healthcare services without any discrimination*. Hapa swali langu ni lile lile kama nililouliza mwanzo. Kwa sababu hapa inaonyesha kwamba hawa wenzetu ambao wana *disability* tumewawekea kifungu hiki kuonyesha kwamba huko nyuma walikuwa kama wananyimwa haki hizi. Sifikirii hivyo kwa sababu Ibara ya 13(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, inasema hivi "watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria".

Halafu, kwa madhumuni ya ufafanuzi wa Ibara hii, kubagua (sasa hapa imeelezea kubagua, kubagua inaendelea mpaka inaingiza jinsia au hali yao ya maisha kwa namna ambavyo watu hao wanayo). Kwa hiyo, ikiwa Katiba imekwishasema kwamba hata hali ya mtu ambayo anayo ikiwa utamfanyia jambo lolote lile kwa misingi ya kubagua, kwa hiyo unakwenda kinyume na Katiba. Sasa, je, kuna umuhimu wowote wa kuweka kifungu hiki cha 26(1) ambacho kinasema *"every person with disability shall have the right to enjoy the attainable standard*" wakati *already* amekwishapewa *right* hiyo katika Katiba? Au madhumuni yake hasa ni kitu gani?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 22, kifungu cha 28, hapa wanasema kwamba *"every learning institution shall be under the general obligation not to discriminate against persons with disabilities"*. Sasa swali langu ni kwamba je, kifungu hiki tumekiweka tu kwa *every learning institution* au kwa *every public institution?* Kwa sababu, tukisema kwamba ni *every learning institution*, ina maana kwamba *institutions* nyingine ambazo ni za *public* wanaweza wakafanya mambo ambayo ni kinyume na utaratibu ule ambao tunataka ufanywe kwa wenzetu hawa ambao ni walemavu. Naomba hapa nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 23 kifungu cha 31 kinasema kwamba *every employer, public or private shall, where there is a vacant post fit for the person with disability and the person applies for the vacancy, give the employment to the persons with disabilities* halafu inaendelea. Sasa nilikuwa ninauliza kwa nini hatuweki kifungu hiki kukifanya kwamba lazima hapa pawe na *preference* kwa hawa watu ambao wana ulemavu?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 31 hapa anasema kwamba kuna suala la *complaint* katika kifungu cha 47. Ni kwamba *Commissioner or the Committee may, on its own motion or where a person aggrieved or a legal representative lodge complaint relating to.* Kwa hiyo hao wanaweza wakafanya *complaints* katika maeneo haya sasa swali langu ni kwamba je, pale mlemavu anapofanya *complaint* hatima ya mwisho itakuwa ni kitu gani, kwa sababu kuna *complains* tu hakuna *releafs* ambazo zimewekwa hapa kwa hiyo, nilikuwa naomba tujue ni *releafs* gani ambazo mtu anaweza akazipata au mlemavu anaweza akapata ikiwa atapeleka *complaints* hizo?

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 51 ukurasa wa 33 hapa vilevile wanasema kwamba, *every person with disability who has attained the age of eighteen years and above shall be entitled to enjoy and exercise political rights and opportunity* na ina endelea.

Sasa hizi inaonyesha vilevile kwamba hawa wenzetu tunawafanya kana kwamba wao hawamo katika ile Katiba au kidogo imewatenga kitu ambacho sicho kwa sababu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 5 (1) ina *include* hawa wote.

Sasa mimi ushauri wangu labda ni kusema kwamba ni kuweka kwamba mtu yeyote ambaye atawanyima haki watu hawa kwa mujibu wa utaratibu huu kwa hiyo, huyo mtu atakuwa ni mkosaji kwa sababu haki ipo katika Katiba sasa haina haja tena kurejea haki hiyo katika kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kuweka kuwa mtu yeyote ambaye atawanyima haki kwa mujibu wa Katiba au kwa mujibu wa Sheria nyingine zilizowekwa basi mtu huyo sasa ndiyo atakuwa ndiye mkosaji. Ninafikiri tukiweza kuyarekebisha haya naamini kwamba Muswada huu unaweza ukawa ni mzuri zaidi kwa kuwasaidia wenzetu hawa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nilikuwa naomba niseme ni kwamba katika Muswada huu na maeneo ambayo yamezungumzwa na wenzangu lakini hasa utaona hakuna Kanuni, hakuna kifungu ambacho kimezungumzia hasa haya masuala ya

*signs* ambazo zinatakiwa ziwepo. Kwa mfano katika *parking,* mlemavu maskini ya Mungu atakwenda atatafuta *parking* na siku hizi tulivyokuwa na magari mengi atahangaika saa nzima hajapata *parking.*

Mheshimiwa Spika, kwa nini maeneo kwa mfano kama *parking areas* zile hatuweki maeneo maalum kama nafasi mbili, tatu *specifically* hizo zikawa ni kwa ajili ya walemavu kama wanavyofanya wenzetu. Mimi ninafikiri tukifanya hivyo tunaweza tukawasaidia sana katika shughuli zao hasa katika maeneo yale mfano ya sokoni, *market* pale au kama mahali penye maofisi ambapo mara kwa mara wenzetu hawa wanakwenda kwa kufanya shughuli zao zinazohitajika. Kwa hiyo, kwa kumalizia naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuyatazama haya ambayo nimeyazungumza naamini yanaweza yakasaidia sana katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abubakar kwa kudhihirisha kwamba umeusoma vizuri sana huu Muswada, tunadhani mchango wako umesaidia.

Mchangiaji anayefuta sasa ni Mheshimiwa Diana Chilolo, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, baada yake ajiandae Mheshimiwa Kabwe Zitto. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, naelekeza shukrani zangu kwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Katibu Mkuu Mama Blandina Nyoni na watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu, bila kuwasahau wadau mbalimbali ambao wametoa mchango mzuri na utasaidia sana kuleta tija endapo utapitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuleta Muswada huu ni jambo moja zuri sana lakini jambo ambalo ni la muhimu sana baada ya Muswada huu kupitishwa na utakapokuwa umepitishwa na Mheshimiwa Rais ni utekelezaji. Ni kuomba wahusika wote wanaoguswa na Muswada huu utakapopitishwa wawe makini katika kutekeleza yote ambayo yameainishwa katika Muswada huu kwani kama hawatakuwa makini katika utekelezaji au utoaji huduma basi Muswada huu utakuwa hauna tija kwa wenzetu wenye ulemavu.

Napenda nitoe shukrani zingine kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri wa Afya kwa kutekeleza ombi langu. Ndani ya Bunge lako Tukufu niliomba kukarabatiwa Chuo cha Wanawake Wasioona Singida Mjini napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Chuo kiko tayari kimekwisha karabatiwa, naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niliomba kituo cha watu wenye ulemavu cha Sukamahela kilichoko Manyoni Mashariki, Jimboni kwa Mheshimiwa Kepteni John

Chiligati, nacho napenda kutoa taarifa kwamba tayari nyumba hizo zimeshaanza kukarabatiwa, naishukuru sana Serikali.

Vilevile nimshukuru Ndugu yangu rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa ufuatiliaji wake makini juzi juzi ametembelea Mkoani Singida na amepitia maeneo hayo na ameona jitihada za wakandarasi wanaokarabati vituo hivyo, kwa kweli nampongeza sana, nimuombe aendelee na moyo huo kusaidia maeneo mengine ili yote yanayozungumzwa katika Bunge lako Tukufu yawe na tija kwa maslahi ya Watanzania wote, baada ya pongezi hizo sasa nami nijaribu kudodosa machache katika Muswada huu ingawa Muswada huu kwa kweli uko wazi umeainishwa vizuri umegusa karibu maeneo mengi muhimu, nina hakika kabisa Muswada huu ukipitishwa utafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, labda tu kuainisha maeneo machache nikiongelea sehemu ya njia za kupita hawa wenzetu hasa wenye ulemavu wa viungo. Kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba wenzetu wenye ulemavu nao wanahitaji haki sawa kama sisi wengine ambao bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametuumba tukiwa salama kabisa wenzetu wengi wanakosa haki zao za msingi, wanakosa huduma kwa kushindwa tu kuingia maeneo mbalimbali ambayo hayakuwekewa barabara za wao kupita kulingana na ulemavu wao wa viungo, Wizara mbalimbali hazina barabara za wenzetu kupita, hospitali nyingi hazina njia za wenzetu kupita, shule nyingi hazina barabara za wenzetu kupita nina hakika baada ya Muswada huu kupitishwa kila mmoja kwa nafasi yake ataangalia umuhimu wa kuweka barabara za hao wenzetu ili na wenzetu sasa waweze kupita maeneo yote kama binadamu mwingine ambavyo anakwenda ili waweze kupata haki za msingi, ninaamini katika kuweka barabara hizo hawatasahau maeneo muhimu.

Mheshimiwa Spika, vyoo ni vitu muhimu sana kwa wenzetu walemavu, wengi wao wanapata maradhi bila wao kutegemea kutokana tu maumbile yao. Utakuta hata anapokwenda chooni anajivuta, anashika sakafu kwa mikono yake mambo mangapi hapo mtu mwenye ulemavu anayapata pale.

Mimi naomba sana maeneo haya yapewe kipaumbele kabisa kama ilivyoelekezwa katika Muswada huu ili tuweze kuwanusuru wenzetu, ili tuweze kutoa wanayostahili wenzetu kwani hata wao wana haki zao za msingi kabisa kufika eneo lolote na kupata huduma yoyote endapo watatengenezewa barabara zinazostahili wao kupita.

Mheshimiwa Spika, na siyo barabara za kwenye majengo tu, vilevile hata katika barabara za kawaida tunakopita. Kusema kweli tunashukuru matuta yamewekwa barabarani na yana kazi zao za msingi lakini matuta yale yamekuwa mengi zile *bumps* ni nyingi, mimi mwenyewe Diana nina macho na ninaona, ninayeona kwamba pale sasa tunapokwenda kuna tuta, anaponirusha dereva ninashtuka, je, huyo kipofu asiyeona hivi anashtuka kiasi gani?

Mimi naomba pamoja na huduma za msingi ambazo tunatakiwa tuwekewe barabarani, matuta yawekwe kwa kiasi, yasiwe makubwa sana na yasizidishwe kiasi

kwamba kila mahali yamshtue mwenzetu mwenye ulemavu wa macho nalo ni tatizo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukawapa ma-*pressure* kutokana na mishtuko shtuko, tunaweza tukawapa hata wale wengine wenye ulemavu wa viungo kwa sababu unapokosa kiungo fulani katika mwili tayari *balance* fulani unaikosa. Kwa hiyo, hata unapokaa kwenye kiti, unaporushwa unaweza kujikuta unatoka kwenye kiti umedondoka kutokana na ule ulemavu kwa kukosa *balance* ya viungo, ninaomba nayo yatazamwe katika barabara zetu ili hata wenzetu walemavu tunaposafiri nao waweze kutembea salama bila matatizo na vilevile kwenye magari ya abiria kwa maana ya mabasi.

Mheshimiwa Spika, mabasi hayana uwezo wowote wa kuwapitisha wenzetu wenye ulemavu kuwapandisha. Watengeneze vivuko vya wenzetu wenye ulemavu ili mwenye ulemavu yoyote anapotaka kusafiri, anapotaka kuingia kwenye gari lolote la abiria basi kuwe na utaratibu mzuri wa wenzetu kupanda kuliko ilivyo sasa hivi wanapata shida wananyanyuliwa wakati mwingine hata nguo zinaanza kukaa vibaya halafu wanakosa raha kwa kweli yaani wanajisikia unyonge fulani, ninaomba wote wenye magari ya abiria kupitia Muswada huu waone umuhimu kuwawekea vivuko vya wenzetu wenye ulemavu ili waweze kupanda kwenye magari yenye abiria bila matatizo ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, vilevile lazima tuangalie wenzetu wenye ulemavu kuhakikisha kwamba wanapata ajira. Nashukuru kwa kweli sasa hivi wengi tu wamepata elimu za kutosha wana *CV* zao nzuri tu lakini hapajapatikana kipaumbele cha kutosha kuhakikisha kwamba wote wenye ulemavu, wenye elimu zao, wenye *CV* zao za kutosha wanapatiwa ajira ni vibaya sana kwa wenzetu wenye ulemavu wale ambao wamejitahidi kabisa kujikwamua, wamejielimisha, wana fani zao wanapofika mahali wanakosa ajira, naomba Serikali na naziomba Taasisi zote za mashirika binafsi na mashirika ya Serikali iwatazame walemavu kwa jicho la huruma kuhakikisha kwamba mlemavu anapofika kuomba ajira kama ana sifa za kutosha ninaomba wapewe ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana kupitia Muswada huu nimeona niliseme hili kwa sababu haipendezi tena mtu mwenye ulemavu kuwa omba omba, kuwa tegemezi wakati tayari amekwishajikwamua kwa namna moja ama nyingine. Ana elimu yake, ana fani yake anakuwa omba omba kwa sababu tu eti amekosa ajira, tuwaonee huruma sana tuwafikirie, tuwaunge mkono, tuwe nao karibu. Tuwapende, tuwape ushirikiano ili wajisikie vizuri katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, vilevile walemavu wana haki ya kupata huduma za matibabu sijui ndani ya Muswada huu tumeangalia kwa kiasi gani kuangalia hawa wenzetu wenye ulemavu wako ambao hawana uwezo, wako ambao familia zao hazina uwezo tutawasaidia habari ya matibabu kwa *style* ipi.

Naomba nalo Serikali ilitazame kwa kina kabisa kuhakikisha watoto wenye ulemavu, wale ambao hawana uwezo kabisa na viongozi wanakoishi wamehakikisha

hivyo basi wapewe huduma bure kwa wale wengine wenye uwezo angalau kidogo basi wapewe punguzo la makusudi kabisa ili na wenyewe waweze kupata haki ya kutibiwa katika hospitali zetu ambazo zinatoa huduma ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la vifaa vya watu wenye ulemavu. Nashukuru kwamba vifaa vinapatikana patikana ingawa bado siyo vingi, lakini vifaa hivi bado vina bei kubwa sana nilikuwa ninaongea na Mheshimiwa Mkanga leo amevaa kiatu kipya nikamwambia Mheshimiwa hiki kiatu umenunua shilingi ngapi, akaniambia nimenunua shilingi 1,000,000 hapa niambie huyu ni Mheshimiwa Mbunge kiatu *pair* moja amenunua shilingi 1,000,000 na yeye ni Mbunge angalau anakipato kile cha Ubunge, je, walemavu wa aina yake walioko huko Kijijini wasiokuwa na uwezo wanafanyaje?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali itafakari kwa kina sana ione namna ya kuwasaidia hawa wenzetu wenye ulemavu kupata vifaa kwa bei nafuu na ikiwezekana wale mbao hawana uwezo kabisa wale wenye uwezo mdogo wapewe kwa bei nafuu na wale wasio na uwezo kabisa Serikali iwape bure. Nawaombea kwa huruma kabisa hawa ni wenzetu, wanapata mateso makubwa, wanatamani hivi na mimi ningetembea kama Diana lakini uwezo huo hawana, hebu tuwafikirie Serikali iainishe kabisa, iweke wazi vipengele ambavyo vinamgusa mlemavu ni jinsi gani atapata huduma zake za msingi, iainishe ili watu hawa wapate huduma, wapunguziwe bei kama siyo kupunguziwa basi wapewe bure ili waweze kupata huduma zao. *( Makofi).*

Mheshimiwa Spika, kuna vifaa vingi, siyo viatu tu wanahitaji baiskeli za kutembelea, wanahitaji mashine za kuandikia, wanahitaji magongo ya kutembelea na vifaa mbalimbali, nakuomba vifaa hivi vipatakane kwa urahisi na kama inawezekana wapewe bure. Hawa hawakuomba kuwa walemavu bali ni mpango wa Mwenyezi Mungu na mpango wa Mwenyezi Mungu hauna makosa tunatakiwa kukubali yote maandiko matakatifu yamesema; "Ukifanikiwa jambo zuri sema *Alhamdulilah* na hata likiwa baya *Alhamdulilah."* kwa hiyo, naamini lugha hiyo wanaifahamu na sisi tuitikie hivyo hivyo kama wanavyoitikia wao tuwape mahitaji yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, bado walemavu hawa wanahitaji pia kupata mawasiliano lakini unakuta mwingine ana ulemavu wa kuzungumza ni bubu. Sasa kuwasiliana inakuwa ni taabu, kuwepo basi hata na wakalimani kwenye maeneo muhimu ya kutolea huduma kwa mfano hospitali wako wengi wanaoshindwa kupata tiba zao vizuri kwa kule kushindwa kujieleza.

Mheshimiwa Spika, sijui nimemaliza nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Diana Chilolo kwa mchango wako mzuri, anayefuata ni Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji na kama nilivyotangualia kutangaza atafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, wakati huo Mheshimiwa Margreth Mkanga, ajiandae.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi nitatoa shukrani zangu zingine. Sina budi kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi kubwa aliyochukua mpaka kuhakikisha Muswada huu siku ya leo umefikishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu ubarikiwe na *Inshallah* urudi tena. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kuuchambua, kuutayarisha na kuutengeneza Muswada huu hadi hivi leo umefika hapa kwani mimi nilikuwa nina wasiwasi sana labda Muswada huu tutamaliza Bunge bila kuletwa. Lakini tunashukuru na kwa niaba ya watu wenye ulemavu wote Tanzania tunaishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Nne kwa juhudi zake inazozifanya kwa makundi maalumu, ibarikiwe Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani mimi mengi yameshachangiwa kwenye Muswada huu, lakini zaidi ningeomba kusisitiza kwenye suala la hilo Baraza. Ni kweli hilo Baraza wenyewe wahusika wawe wengi zaidi na ikiwezekana waongezwe, kuna usemi unasema, *nothing about us, without us,* kwa hiyo, kutokana na huo muundo wa Baraza ungeangaliwa tena, wenyewe tunahusika tuwe wengi zaidi. *( Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuhusu hilo ni suala la vifaa, mimi hapa nimekaa miaka mitano kuna vifaa ambavyo vinastahiki wala havina gharama sana vinaingizwa humu chenyewe kina *transcribe* (kinatafsiri) kwa *brailler* kinaweka kwa *sighted,* na ya *sighted* inawekwa kwa *brailler,* lakini hata hiyo nina imani baadae yatatengenezwa haya. Kwani sifaidiki vizuri kama huu Muswada, mimi sikupata kuogelea nao zaidi kwa sababu mengi inabidi kusomewa lakini ingekuwa imechapishwa kwa *brailler* ningefaidi mimi mwenyewe zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuna hili suala la usafiri, pia wajumbe wamekwishalichangia. Suala la usafiri kweli la barabarani vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa mara ya kwanza jana nilipokuja Dodoma nilipanda gari la Kampuni ya Shabiby naona wamefanya marekebisho mazuri mabasi kufunga mikanda, vioo, *air condition,* mwendo mzuri labda ningeomba Mheshimiwa Shabiby ungekuwa wa kwanza ukaleta walau mabasi mawili, matatu ya watu wenye ulemavu nao wakaweza kuyatumia, na wengine kama *Mohamed Trans* labda mngeanza kuonyesha nyie mfano ili yale mabasi yakawa na milango miwili mmoja kwa wa kawaida na mmoja kwa watu wenye ulemavu anaweza kuingia na *wheel chair* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuhusu barabarani ni kuwa mimi nilibahatika, ni muasisi wa Jumuiya za watu wenye ulemavu Zanzibar kwa hiyo nilibahatika sana kusafiri nchi mbalimbali kuangalia maendeleo yao. Mwaka 2000 nilikwenda Australia, Merlbourne kulifanyika Mkutano wa Watu Wasiiona Duniani *(World Blind Union).* Kwenye mkutano ule na ile sehemu ilivyojengeka kule Australia kidogo niseme bora na mimi nikae kule kule nisirudi kwetu kutokana na maendeleo wenzetu waliyoyapiga na hatua. *( Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye *lift* wameweka alama za *brailler* kwa hiyo mtu asiyeona yeye mwenyewe hana haja ya msaada, anabonyeza anafika anakofika. Lakini mimi nilikuwa muoga, muoga, mshamba, mshamba nilikuwa siamini vizuri kwa hiyo, wenzangu walinicheka wanabonyeza *lift* imewekwa alama ile ya *brailler* anapanda anakwenda anakotaka. Barabarani kuna ile inaitwa sijui *keep* sijui nini watu msioona mnapita wenyewe mnabonyeza ikilia hao mnavuka barabara bila msaada wa mtu.

Siku ya kwanza nilifuatana na wenzangu wasioona ndiyo wameishi Ulaya, wakafanya nikashangaa usiku kucha sikulala. Siku ya pili nikawaomba wale wahudumu hebu na mimi kanionyesheni pale wanapobonyeza kile kidude halafu unasubiri kikilia unavuka barabara bila ya msaada wa mtu ingawa ni kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali najua bado ndiyo hali ilivyo ya kiuchumi lakini kuna baadhi ya maeneo yangeangaliwa yakaanza kupewa kipaumbele hasa hayo maeneo ya usafiri ya humu barabarani, kuongeza elimu zaidi vifaa zaidi na sehemu ya matibabu kama alivyozungumza Mheshimiwa Chilolo.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya mambo Serikali ilianzisha mwaka 1981 ulipotangazwa mwaka wa kimataifa wa watu wenye ulemavu. Ilijitahidi kweli Serikali yetu walivyoweza kama hili suala la mfuko wa watu wenye ulemavu nakumbuka ulianzishwa mwaka ule chini ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi na uliendelea vizuri lakini sijui uliishia wapi mfuko ule, na leo kwenye Muswada naona umo labda ungefanyiwa utafiti ule wa mwanzo ulianzwaje, ilikuwaje, ilikuwa vipi ikatumiwa sera ile ile labda uboreshwe kwa hiyo, hilo nalo ni jambo zuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali yetu wakati ule ilipanga kuanzisha majengo kwa watu wenye ulemavu ya shughuli mbalimbali na majengo hayo mpaka leo yapo hapo Kinondoni kwa Manyanya. Mengine baadhi ya watu wenye ulemavu wanayatumia kama ofisi na mambo mengine yapo kama magofu kwa hiyo, kutokana na Muswada huu ningeshauri majengo yale yaangaliwe upya, yashughulikiwe na kufanyiwa kazi kama ilivyokuwa imeamuliwa hapo mwanzo bila ya kupata hasara kujenga mengine au kufanya shughuli nyingine yangeshughulikiwa yale yakaboreshwa na yakafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyuo, vyuo vipo vingi vya watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Lakini kuna haja tu ya vyuo vile kuviboresha na kama hivyo kuvikarabati kama hivyo vingine tayari vimekwishakarabatiwa, vingine vingeangaliwa viko Tabora kule Manoleo, viko Mtapika - Masasi, viko Yombo na sehemu zingine mbalimbali ili kupunguza gharama nafikiri Wizara na Serikali ingeviangalia vilevile ambavyo vipo ikaviboresha na kuvikarabati ili kupunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuna baadhi ya shule za watu wenye ulemavu maalumu sijui Serikali imeshindwa kutoa huduma ipasavyo, nilisikia kwenye redio siku moja nikasikitika, kuna shule hii ya Lushoto inayoitwa Irente, inasomesha watoto wenye ulemavu na wengine hufichuliwa vijijini na maaskofu, mapadri wanawaleta. Mwalimu mkuu wa shule alisikitika sana kwamba huduma zimekuwa chache, vijana wengi wanaoletwa Mungu anawajaalia, wanakuwa na vipaji, wanasoma vizuri, wanatambua,

kwa hiyo, hizo shule zilizopo zingeboreshwa zikaanza pia kushughulikiwa zaidi na kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine huwa kunakuwepo na mikutano ya Kimataifa ya watu wenye ulemavu. Tungeomba Wizara, Serikali na baadhi ya sisi Wabunge wawakilishe watu wenye ulemavu tuwe tunasaidiwa kushiriki, vingine wanatufadhili wenyewe, wengine inabidi utafute mfadhili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lingeangaliwa hilo hata na baadhi ya viongozi kwa watu wenye ulemavu kwenye Jumuiya zetu, wengine wanapata mialiko wanashindwa.

Mheshimiwa Spika, sisi tunawawakilisha watu wenye ulemavu, lakini kuna jambo sijui nimlaumu Waziri au Wizara, hivi karibuni kulifanyika mkutano unaouhusu masuala ya watu wenye ulemavu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Waziri alishiriki na ulifanyika Uganda mwezi Februari, kwa bahati mbaya mimi kuna jamaa kule wananifahamu wakawa hawakupata *email* yangu, wakawa wananitafuta, nafikiri walinitafuta kwa suala hilo, nasikitika Mheshimiwa Waziri kashiriki na watalaam wake ameshindwa kutuchukua sisi hata mtu mmoja angalau tukaenda kusikiliza ule mkutano.

Mheshimiwa Spika, yakitokea mambo kama hayo tujumuishwe na sisi, tushirikishwe, tupewe nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui muda, mengi yamezungumzwa naomba kupitia Muswada huu nizungumze lingine la mwisho ambalo watu wenye ulemavu wamenituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka mitano inakwisha, tumepeleka barua kwa Rais na tumezungumza sana na hata kuomba, lakini hatujabahatika kumwona, kwa hiyo, kupitia Muswada huu, Waziri wa Afya na Waziri Mkuu hii miezi minne iliyobakia basi tupewe nafasi tukamwone Rais walau tukamshike mkono tu na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisikiliza na kupata nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji kwa mchango wako na kama nilivyotamka awali kwamba anayefuata ni Mheshimiwa Kabwe Zitto, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Margreth Mkanga.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2010, ambao Bunge lako Tukufu, Bunge la Tisa linapata bahati ya kuweza kuupitisha baada ya maombi ya muda mrefu sana ya watu wenye ulemavu kuhitaji kuwa na Muswada ambao utafanya makubaliano mbalimbali ambayo nchi yetu imeingia katika Jumuiya ya Kimataifa, ili yaweze kuwa *domesticated* na yaweze kushughulikiwa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia siku ya leo na kwa kupitia Muswada huu, kwangu binafsi ni siku muhimu sana kwa sababu mimi ni mtoto wa mtu mwenye ulemavu, mama yangu ni mlemavu na ninafurahi kwamba mama yangu ni Kiongozi wa Chama cha Walemavu, ninapozungumza hapa na yeye yupo hapa ananisikiliza, kwa hiyo, ni furaha kubwa sana kwamba Bunge la Tisa ambalo nami nimo limeweza kuhakikisha kwamba sheria hii inaweza kupita lakini siyo hilo tu kwamba sheria inapita mama yangu akiwa ni kiongozi wa chama cha walemavu. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ningekuomba Mheshimiwa Zitto ukae kidogo, Bi. Shida pengine ungejitambulisha ili Waheshimiwa Wabunge wafahamu kwamba upo hapa.

*(Hapa Bibi Shida alisimama na kupunga mkono)*

**SPIKA**: Ahsante sana, huyo ndiye mama yake Mheshimiwa Mbunge Kabwe Zitto, endelea.*(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa heshima hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wamezungumza kwamba watu wenye ulemavu tuwaonee huruma, watu wenye ulemavu tuwasaidie, walipe vitu nusu, bidhaa mbalimbali wanunue nusu.

Mheshimiwa Spika, watu wenye ulemavu hawahitaji huruma, watu wenye ulemavu wanahitaji haki zao zitekelezwe, hawahitaji huruma, watu wenye ulemavu wanahitaji kuhakikisha kwamba mazingira ndani ya nchi yanawekwa ili kuweza kuondoa *mentality* ya wao kuonekana kwamba siyo watu kamili au siyo watu ambao wanastahili masuala fulani fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hata lugha ambayo tunaweza tukatumia ya kusema kwamba tuwahurumie, tuwape vitu nusu ni lugha ambayo tunawafanya kuwadogosha zaidi kwa Kiswahili cha Kipemba, jambo la msingi kama Taifa ni kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira ambayo yatahakikisha kwamba Mtanzania yeyote anayezaliwa ama ana ulemavu au hana ulemavu anapata haki zake za msingi kama Mtanzania mwingine yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuunganisha hapo katika mchango ambao ameutoa Mheshimiwa Abubakar Bakar, kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ime-*guarantee* haki za Watanzania, haki ya mtu binafsi na haki za kijamii, ningependekeza katika Muswada huu kwamba katika sehemu fulani kama ni *preamble* ama chochote kile tuweze ku-*recognise* hizo haki ambazo zinatolewa na Katiba hata kwa kusema tu kwamba kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua haki kwa mujibu wa Ibara hii mpaka hii ya Katiba, Muswada huu tunauweka kwa ajili ya kutekeleza masharti hayo ya Katiba. Kwa sababu tukumbuke pia Ibara ya 13(5) ya Katiba ambayo inakataza ubaguzi inasema, neno ubaguzi halitafafanuliwa kwa namna ambayo itazuia Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kuwezesha matatizo mahsusi katika jamii kuchukuliwa hatua na ndiyo hii sheria tunaitunga.

Mheshimiwa Spika, tunaitunga hii sheria kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kile kipengele cha 13(5) cha Katiba kinaweza kikazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la pamoja na kwamba tunatunga sheria bado kuna kazi ya msingi sana ya kuifanya jamii iweze kufahamu ya kwamba kama nilivyosema hapo awali kwamba watu wenye ulemavu ni watu kama watu wengine wowote kwa sababu kuna hilo tatizo, kuna unyanyapaa, mtu mwenye ulemavu akionekana tu anaonekana kwamba ni mtu wa taabu, ni maskini, ni omba omba na juzi juzi hapa tumesikia kuna watu wanasema mtu mwenye ulemavu akikuomba mkono sijui unaota manyoya, na vitu kama hivyo, lakini hivi ni sehemu ya vitu ambavyo ndani ya jamii vinawadidimiza watu wenye ulemavu, kwa hiyo kuna kazi ya ziada ya kufanya na kwamba tukiwaona tujue ni madaktari, wanasheria, ni walimu na ni wazazi na wengine wamewazaa watoto kama Zitto Kabwe, kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba wanapata zile stahili zao ambazo zinastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria imeweka suala la *accessibility*, nimelifafanua vizuri na nimeweka mazingira ambayo hasa kuanzia na majengo ya umma yanatakiwa yawe na hali ambayo watu wenye ulemavu wataweza kuyafikia bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa katika Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO* Mheshimiwa Peter Ngumbulu sasa hivi ni mgonjwa kwa hiyo, hawezi kupanda katika nyumba ambazo hazina misaada ile ya watu wenye ulemavu inavyotakiwa, siku za nyuma tulikuwa tunatumia Karimjee kama jengo, sasa tukaenda kutumia Ofisi za Bunge za Dar es Salaam, ilikuwa taabu sana mpaka tulifikiria labda Kamati ishuke chini itafute Jengo la chini kuweza ku-*accommodate* hali ile ya Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*. Jambo kama lile ni jambo ambalo inabidi pia tuweze kuangalia kwamba majengo yetu, jengo la Bunge la Dodoma lipo sawasawa lakini pia Jengo la Bunge la Dar es Salaam liweze kuangaliwa ili watu ambao wana ulemavu ambao tunawatungia sheria leo, wanapofika kwa ajili ya huduma mbalimbali za Kibunge waweze kuzipata bila tatizo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inazungumzia utambuzi wa watu wenye ulemavu, ningependa nipate tafsiri kwa sababu ni woga kidogo kwamba kama tutakuwa na daftari la ku-*register* watu wenye ulemavu, sheria inasema kwamba ni kwa madhumuni ya utambuzi tu lakini daftari hili lisiweze kutumika kwa madhumuni mengine, na je, hakuna njia nyingine ya kuweza kufanya watu wenye ulemavu wakatambuliwa na jamii badala ya kuwa na *register* ya watu wenye ulemavu, napata mashaka kidogo kwamba hii inaweza kuwa ni sehemu ya ubaguzi, kwa sababu hatuna *register* ya watu wengine mbalimbali, ningependa nipate ufafanuzi inawezekana ni nia njema kabisa lakini pia *register* za namna hii zinaweza zikatumika vibaya, kuna masuala ya *privacy* na vitu kama hivyo kwa hiyo ningependa Waziri aweze kunifafanulia eneo hili.

Mheshimiwa Spika, watu wamezungumzia kuhusu baraza la watu wenye ulemavu na wamezungumzia kuhusiana na idadi ya wajumbe na kadhalika, ni dhahiri kabisa

kwamba madhumuni ya kuwepo kwa baraza hili ni kuwa kama daraja kati ya watu wenye ulemavu na Serikali na hata ukisoma zile *function* za baraza katika *section* ya 11 ya Muswada huu inaonyesha kwamba ni kama *bridge* kati ya Serikali na watu wenye ulemavu, kwa hiyo, ni vizuri sana kama hili ni daraja kati ya watu wenye ulemavu na Serikali basi angalau kuwe na idadi ya kutosha ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nimeona katika sheria kipengele 1(e) wanazungumzia kwamba mtu mmoja kutoka *organisation* ya watu wenye ulemavu lakini tunafahamu watu wenye ulemavu wapo wa namna nyingi, kuna walemavu wa viungo, walemavu wa ngozi na walemavu wa vitu vingine kwa hiyo, nilikuwa nafikiri labda tuongeze na hapa tunaweza kusema kwamba *not less than four members from organisation* za watu wenye ulemavu ili kuweza kuhakikisha kwamba tuta-*accommodate* watu wengine na kuwa na watu wengi na tuzingatie baraza hili linafanya maamuzi kwa kura, kwa hiyo, ni vizuri sana kama litakuwa na watu wa kutosha wenye ulemavu hata hizi kura zinapokuwa zinapigwa ziweze kuzingatia vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kimoja tu ambacho ningependa kupata ufafanuzi kutoka Serikalini, katika Baraza Mwenyekiti anaonekana kwamba anateuliwa na Rais lakini wajumbe wa baraza haisemwi, kuna wajumbe ambao wanaingia kwa nafasi zao lakini kwa vyovyote vile ni lazima pawepo na *some sort of appointing authority* kwamba wajumbe wengine watateuliwa na Waziri anayehusika na watu wenye ulemavu, kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo nalo pia liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa ni ushiriki wa watu wenye ulemavu kwenye siasa, sehemu ya 51(3)(i) – (viii) ina-*guarantee* kabisa haki ya watu wenye ulemavu katika kupiga kura, lakini kifungu hicho haki-*guarantee* haki ya watu wenye ulemavu kwenye kuchaguliwa na ile *heading* ya *section* yenyewe inazungumzia kuchagua na kuchaguliwa, kwa hiyo, kuna taratibu ambazo zimewekwa, kuna taratibu ambazo vyama vya siasa vimeweka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kunakuwa kuna uwakilishi wa watu wenye ulemavu na kwa dhati kabisa bila kujali tofauti za kisiasa, chama kikongwe nchini kimetoa mwanga, kimeonyesha na kimeweza kuleta Wabunge wenye ulemavu ambayo ni changamoto kwa vyama vyetu vingine pia kuweze kufuata ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwakilishi, maana yake isiwe wawakilishi wa walemavu ni watu wa CCM tu, pia na vyama vingine viweze kuweka mazingira kama hayo ni hatua nzuri sana ambayo wenzetu wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hatua kama hii tunaweza tukaiweka ikawa ni ya nchi, ikawa ni ya Kikatiba. Kwa mfano, Sehemu ya 31 ya Muswada huu inasema kwamba katika maeneo ya kazi ambayo watu wameajiriwa zaidi ya watu 50 angalau asilimia tatu ya wale watu wawe ni watu wenye ulemavu, tunaweza kabisa, Bunge lina zaidi ya watu 300, kwa hiyo, ni 50 mara sita tunaweza tukasema kwamba na hata maeneo ya kisiasa kama Mabunge, Mabaraza ya Halmashauri na kadhalika yanaweza yakazingatia hiyo asilimia fulani na tukajenga mazingira ambayo vyama vya watu wenye ulemavu vyenyewe ndiyo vikaleta wawakilishi wao ndani ya Bunge badala ya wawakilishi kutokana na vyama vya siasa na hii inafanyika kwa nchi zingine kama Uganda na inasaidia sana kuondoa zile *ideological difference* miongoni mwa vyama vya watu wenye

ulemavu na hivyo kuhakikisha kwamba wawakilishi wanaokuja wazungumzia na kuzingatia zaidi mambo yale.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba akina Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, akina Mheshimiwa Mama Margreth Mkanga wanazungumzia zaidi mambo ya ulemavu bila kujali itikadi za vyama lakini ni hao kesho unaweza ukawapata wengine hawazingatii hayo, kwa hiyo tungeweza kuangalia tukawa na chombo ambacho ni cha Kitaifa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga hoja Muswada huu na kama nilivyosema hapo awali ni Muswada ambao ni *historical* lakini pia ni Muswada wa heshima sana kwa Bunge la Tisa ambalo umeliongoza na kuhakikisha kwamba Muswada huu umeweza kupita na ninawapongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba Muswada huu pia umeweza kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kabwe Zitto, tunaendelea na mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Margreth Mkanga atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, wakati huo Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ajiandae.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache kwenye Muswada huu muhimu ambao ni wa kihistoria, na ambao mchakato wake na mambo yake yote yameanza zamani, na ninamshukuru Mungu kwamba nimepata nafasi ya kuwa shahidi wa mchakato huo na hatimaye leo ninaamini Wabunge tutapitisha Muswada huu kwa sababu sote kwetu kwamba hata kama leo, kesho ndani ya familia yako hakuna mlemavu, lakini ni nani ajuaye hujafa hujaumbika, na sisi tuliopo katika nafasi hizi za maamuzi tusipoandaa mambo kama haya sawa sawa yatakapotusibu tusije tukalalamika mbona tulikuwa na nafasi ya kuyarekebisha, mbona tulikuwa na nafasi ya kuyaweka sawa sawa, hatutapaswa kumlaumu mtu lakini sana tutajilaumu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ameniwezesha kwa karama yake, kwa uwezo wake kuwepo hapa na kushuhudia haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Wizara iliyoandaa, Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi, Katibu Mkuu na wote kabisa kwa sababu ninafahamu Wizara imefanya jitihada za ziada kuhakikisha kwamba Muswada huu unajadiliwa leo Bungeni, hongereni sana na poleni sana, lakini huko ndiko kuwajibika na sisi tunawaombea muendelee kutujali namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kama mwenzangu alivyosema, kwa kweli tulikuwa tunamsumbua na vi-*note*, sasa akituambia tulieni tunasema ni yale yale, kwa kweli tunakushukuru sana Waziri Mkuu, ulitamka haya wakati wa chakula pale tulipokaribishwa na Mzee Reginald Mengi ukasema mambo yanakwenda vizuri hata na Mheshimiwa Dada Mkanga, anajua nikasema sasa kwa

sababu anaji-*commit* Dada Mkanga nitaendelea kuulizia, lakini hata kabla sijaulizia mambo yamekuwa tayari, nashukuru sana ahadi ile uliitoa mbele ya kadamnasi ya wenye ulemavu wenzangu zaidi ya 1,000, ikawa sasa wananiuliza, lakini leo wanashuhudia kwamba ahadi ile imetimia, kama wimbo wa Ahadi ya Baba Imetimia, kwa kweli tunakushukuru baba ahadi imetimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu, wanachama wa vyama vya watu wenye ulemavu na walemavu nchini kwa ujumla wao. Kwa mshikamano na ushikiriano mkubwa walionipa mpaka leo Muswada huu tunaujadili haya hayakuanza leo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeingia Bungeni mwaka 2000, nikawaendea wenzangu katika yote sisi tunachangamoto gani, wakasema tunazo changamoto nyingi, lakini hatuna sera na kadhalika. Nikasema basi tuanze na cha kwanza kwa sababu Kiserikali sasa hivi sheria hazitungwi mpaka sera, nashukuru Serikali tuliishauri kwa kelele zote sera ikawa tayari mwaka 2004 huu ni mwaka wa sita tangu ile sera imekuwa tayari. Tukaendelea kushauri Mungu bariki na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu ukaongeza *speed* na chumvi pale, sasa haya mawili ndiyo hatimaye leo yameunganishwa kupata Muswada mzuri kama huu kwa ujumla wake, nadhani sasa tutakuwa na mategemeo zaidi hasa yale yaliyomo humu yakitekelezwa.

Mheshimiwa Spika, mengi yamekwishaelezwa na hilo nilishukuru, nilikuwa nawasikiliza nikasema kumbe shule hii tuliyokuwa tunaitoa humu ndani maana yake siyo kuchangia tu lakini Waheshimiwa wengine nikiri kwamba walikuwa hawavijui. Haya mambo ya ulemavu kama huna mtu wako karibu, Mheshimiwa Zitto pale anaelewa na amesema vile kwa sababu mzazi wake ni mlemavu, kwa hiyo na yeye anakuwa ni sehemu yake.

Lakini kwa wengine kwa kweli mimi wenzangu nilikuwa nawaambia tusilaumu kwa sababu hawajui, *it is a wearer of the shoe who knows where it pinches*, kwa hiyo usilaumu kila mtu, tufanye jitihada ya kuelimisha sisi wenyewe ndiyo tuwe walimu taratibu umma na jamii utatuelewa, na tumefanya kazi hiyo kwa uaminifu kiasi kwamba jamii sehemu fulani wanaelewa sasa lakini sehemu kubwa ya jamii bado tunakazi kubwa kama Mheshimiwa Diana Chilolo alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, nimeona kama viongozi tunaelewa sana sasa hivi na yote wamesema, mimi leo hapa ni furaha tu ambayo hata haieleweki, ninafurahi mno na ninapaswa kupiga magoti kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu kazi ilikuwa ndefu tangu mwaka 2000 na siku za nyuma zaidi, leo inakamilika unahitaji nini tena, kwa hiyo, namshukuru Mungu katika kipindi changu alichonijalia kuwawakilisha wenzangu kwa pamoja tumefika mahali pa kusema sasa safari ni nyeupe. *(Makofi)*

Ninachoomba ni kwamba sheria hii itapita kwa vyovyote vile kwani ina matatizo gani na ndiyo tunajiandalia maisha mema huko na sisi tukifika kwenye kundi hili siombei, lakini nilisema hujafa hujaumbika, sheria hii itapita, Kanuni ziandaliwe haraka,

Muswada wa Gharama za Uchaguzi haraka kanuni tayari zimejadiliwa tayari, ili utekelezaji uanze hata kipindi hiki hakijaisha kwani hiyo Julai tunapomaliza tukiambiwa kanuni zipo tayari utekelezaji unakuja pana tatizo gani? Siyo tena kanuni inachukua miaka minne ndiyo utekelezaji uanze, itakuwa haina faida.

Mheshimiwa Spika, hivi wenzenu leo hapa tumefarijika huu ni ukombozi kwetu kama haya kweli yakitekelezwa kwa sababu ni mengi. Tafadhali sana ziandaliwe haraka kanuni za kutekelezea Muswada huu ambao naamini utakuwa sheria na Mheshimiwa Rais atasaini haraka sana kwa sababu nadhani anahitaji kabisa kuona haya mambo yananyooka, nimshukuru pia Rais nilimsikia anasisitiza kwa upande fulani kwamba hili lazima liwe, kule ulimwenguni alikosaini kule wakimuuliza sasa anaenda kifua mbele kwamba mimi nimemaliza kazi, na hiyo ni faida na heshima ya nchi yetu tunayoisema imejaa amani na utulivu, basi na maendeleo yawe ya wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi mmoja likiendelea na lingine mkaliacha nyuma hamjaendelea.

Mheshimiwa Spika, nikiri kufuta usemi kipindi kilichopita nilizungumza kwa uchungu nikasema sizungumzii tena mambo haya, nafumba mdomo wangu, *I was just desparate,* kiliniuma na ndiyo nikaendelea kughasi leo ninafuta usemi ule, nafuta kwa sababu inabidi nichangie haya, ile ilikuwa ni mfa maji haachi kutapatapa, siyo kwamba sikuwa na imani lakini *what to do* kama mwakilishi unafanyeje, wewe siyo mtendaji kwa hiyo ni kuhimiza tu. Kwa hiyo nafuta usemi ule kwamba leo nitachangia muswada huu kwa sababu upo hapa mbele yangu.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu ukurasa wa sita naomba pale tafsiri ya *civil society* tuweze kuongeza na vyama vya siasa, kwa sababu mpaka sasa ndani ya nchi yetu mambo ya uchaguzi na taratibu zake zinaenda kufuatana na vyama vya siasa, ni mpaka hapo tutakapobadili, kwa hiyo, hawa waliotajwa ndani ya *civil society* hata hawa kwa sababu watu wenye ulemavu tunashiriki humu na tunapaswa kushiriki humu, na ni kutokana sasa hivi na Chama cha Siasa ndipo unachaguliwa au unachagua. Pamoja na kwamba kijana wangu pale ameshapendekeza vinginevyo lakini hayo ni mpaka baadaye.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kifungu cha 11 ilivyoelezwa kwamba *NGO'S* na Taasisi zinazohusika na watu wenye ulemavu inabidi zipeleke ripoti angalau mara moja kwa mwaka kwa Baraza, hii mimi imenifurahisha kwa sababu itadhibiti taasisi ambazo ni za kitapeli, zingine zimeundwa kutumia changamoto za watu wenye ulemavu watu kujifaidisha, sasa hizo hazitakuwepo kwa sababu watakuwa wanakaguliwa kwenye taarifa hizo kwamba kwa nini mmedanganya haya na zitafahamika hizo *NGO'S* tapeli na zitafutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muundo wa Baraza wenzangu wamesema Serikali ongezeni walengwa wanaohusika halafu hawa watalaamu wawe tu washauri, kwa sababu anayejua hasa kinakuwa nini ni mlemavu kwa hiyo atatoa ushauri mzuri zaidi, kwa hiyo, hilo ni msisitizo lakini ndilo nilikuwa nalifurahia.

Mheshimiwa Spika, Kamishna wa Ustawi wa Jamii atahusika katika kuangalia idadi sahihi ya watu wenye ulemavu nchini, sijui ni kwa *register* au ni kutumia nini, lakini mimi nafurahi kwa sababu mipango mingi sasa hivi inashindikana. Hivi ni nani anajua kikamilifu kabisa watu wenye ulemavu wapo wangapi? Hata Bajeti ikitengwa inawezekana ikawa ndogo kuliko tulivyo na sasa tupo wengi tu, kwa hiyo, hapa nilikuwa nashauri kwamba huyo Kamishna ashirikiane na Mkurugenzi wa Mamlaka/Wakala wa Takwimu kwa sababu ile *National Bureau of Statistics* ndiyo ambao wanajua labda *through* sensa na vitu kama hivi, washirikiane pamoja na kwamba imesema itashirikiana na viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu ili kuweza kuona inakuwaje.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kwamba Baraza litatoa mapendekezo Serikalini kuhusu utoaji wa vifaa na nyenzo na pia itasaidia kutoa misamaha ya kodi kwa wanaoingiza *raw materials* za kutengenezea vifaa vya watu wenye ulemavu, wenzangu wamesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaumia sana na Serikali inasema sisi tunatoa *import duty* sijui, haitoshi vifaa hivi ni aghali.

Mheshimiwa Spika, nitakuletea bili hapa haya mavyuma niliyoyavaa juzi tu hapa nimekongolewa *it is true* wanasema vinatoka nje cha kuunganisha tu hapa ni laki mbili na kingine laki mbili na nusu laki tano kwa mguu mmoja, nani anaweza hayo?

Mheshimiwa Spika, tuone uwezekano wa kuhakikisha kabisa vinapungua ndiyo hivyo vinavyotusaidia kutembea, leo saa saba tulipoondoka hapa chuma cha mguu kilikatika, kule nimepima vipya ndiyo hivyo hivi vya zamani vimechoka, kilidondoka nimesaidiwa hapo *VETA* kuweka sijui wanaita sijui kitu gani, bila hivi Mkanga sitembei, sasa ni Mkanga, asiyeona je bila ile fimbo nyeupe, kiziwi je, bila kusikia, jamani hayo yamesemwa humu lakini tuone utekelezaji basi uwe bure kabisa.

Lakini kwa anayejiweza kama Mkanga *half*, *half* ile mnisaidie kulipa. Nimeumia, wazazi wameumia kunilea na kunifikisha hapa. Hapa natoa maendeleo kama binadamu mwingine yeyote. Kwa hiyo, hilo sijui ndiyo *positive discrimination* angalau mtu unampa moyo na unaipa familia moyo. Bila wao kunikongoja ningefika hapa? Kwa hiyo, naomba vifaa vya walemavu vipunguzwe bei kabisa na wasiojiweza iwe ni bure. Fedha ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa mambo ya ajira kwamba kutakuwa na marekebisho, kwa kweli kuna matatizo. Kuna wasomi wananipigia simu Mheshimiwa, mimi nimefaulu lakini *sociology* kila ninapoomba kazi nikienda kwenye *interview* naambiwa bado sifai. Labda kwa sheria hii sasa, hili likisisitizwa tutaweza kujitegemea katika mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 62 sehemu ya adhabu mimi nimesoma, nimeona tu kulipa faini. Mbona hakuna kifungu hapa? Sikuona kifungu, kwani ni kivipi mtu atakaye-*violate* Muswada huu na mambo yaliyomo ndani tangu familia mpaka nani, adhabu tena ya fedha sijui na kifungo; mimi nadhani hii inategemea na uzito wa kosa.

Faini na kifungo pia au faini yenyewe ifanye kuongezwa kwa sababu ndiyo hivyo mambo mengine unalazimisha watu wafanye pamoja na kwamba hayana ulazima, lakini ningeshukuru hayo.

Mheshimiwa Spika, muda umekwisha. Naunga mkono hoja. Lakini elimu kwa wote kuhusu masuala haya, ajira zaidi ya Maafisa Ustawi wa Jamii, katika maeneo yetu nakubaliana na wenzangu wote waliyoyasema. Mungu atubariki sote katika utekelezaji wa hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Margreth Mkanga, sote ndani ya Bunge na wenzetu nje ya Bunge wanatambua ushupavu wako katika kutetea haki za walemavu. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Asipotumia muda mrefu mno itakuwa vizuri ili tuweze kumsikia na Mheshimiwa Said S. Arfi, aliyeleta maombi yake hivi karibuni. Mheshimiwa Zambi kwanza. Nimemruka samani.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasikitika tu kwa sababu ulishanitaja kwamba ningefuata. Hata hivyo nashukuru kwa kukumbuka.

**SPIKA:** Hii ndiyo ukisikia inaitwa *positive discrimination*. *(Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze na mimi kuchangia Muswada ambao uko mbele yetu wa ndugu zetu walemavu. Ninaomba na mimi nitoe wasiwasi wangu kama Mwenyekiti wa Kamati alivyosema wakati anawasilisha taarifa yake, lakini pia na baadhi ya Wabunge wenzangu wamechangia. Naona sheria hii au Muswada huu unaongoza kwa kuwa na Wizara nyingi sana ambazo zinahusika moja kwa moja. Nikihesabu haraka haraka, naona Wizara kama saba, nane hivi zinahusika. Sasa utekelezaji wa sheria au Muswada ambao unahusu Wizara nyingi namna hiyo kuwekwa chini ya Wizara moja inanipa wasiwasi kwamba utekelezaji wake unaweza kuwa mgumu sana. Tunapomaliza kupitisha Muswada huu na baadaye Mheshimiwa Rais kuusani kuwa sheria, maana yake lazima kanuni zitungwe na zihusishe Wizara na taasisi ambazo zinaguswa na Muswada huu. Sasa ni vizuri ingeendelea kuangaliwa kama ni busara zaidi, basi Muswada uwekwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili angalau anapoagiza iwe rahisi kwa mambo yatakayoagizwa yaweze kufanyiwa kazi inapowezekana. Vinginevyo, tutakuwa na wasiwasi mkubwa sana. *(Makofi)*

Lakini kabla sijaendelea kuchangia Muswada wenyewe, naomba niwatoe wasiwasi wenzetu Waheshimiwa Wabunge wenye ulemavu, lakini pia na ndugu zetu Watanzania wengine wenye ulemavu. Mimi naomba niseme kwamba Muswada huu ni wetu wote, kwa maana ya kwamba, sisi ambao hatuna ulemavu hatujijui kama kesho itakucha salama au itakuwa namna gani. Lakini tuliingia na wenzetu wengine Bungeni humu wakiwa wazima kabisa, leo wamekuwa walemavu, wapo. Muswada huu tujue kwamba ni wetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi, sisi sote tumechaguliwa na wenzetu wengine ambao ni walemavu. Nina hakika wewe Urambo kule unakotoka kuna walemavu waliokupigia kura, kwangu Mbozi kuna walemavu walionipigia kura. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sisi kama Wabunge wote bila kujali maumbile yetu tuwasemee Watanzania wote tunapofanya hivi tunawasemea Watanzania wote wakiwepo walemavu na wasio walemavu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mama Mkanga asijikie mpweke sana na wenzetu walemavu wakajisikia wapweke sana. Sisi Wabunge tukiwa ndani ya Bunge tunawasemea Watanzania wote pamoja na wenzetu walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nipitie kwa haraka sana sehemu ya tano ya Muswada kuhusiana na wajibu wa Serikali za Mitaa au taasisi yoyote kumtunza mlemavu. Naomba tena niseme kwamba kumekuwa na tabia ya Watanzania wengi au jamii nyingi kukwepa wajibu wa kuwatunza watu wenye ulemavu. Kumekuwa na tabia hiyo, watu wengine wanaona kama ni wajibu wa Serikali peke yake au watu fulani fulani tu kuwatunza au kuwaangalia au kuwajali watu wenye ulemavu.

Kwa hiyo, ninaomba Wizara hii ambayo imepewa dhamana pamoja na kwamba nilifikiri ni vizuri kabisa jukumu hili lingepelekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini Wizara yenye dhamana ihakikishe kwamba kuna elimu ya kutosha kwa jamii, ione kwamba ni wajibu wa Watanzania wote, ni wajibu wa jamii yote kuwatunza, lakini pia na kulinda haki za wenzetu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nalisema kwa sababu kifungu hiki pia kinatoa kazi nyingi sana au wajibu mkubwa sana kwa Halmashauri zetu za Wilaya. Sasa wakati kinatoa wajibu huo kwa Halmashauri za Wilaya, hili pia liende sambamba na kuhakikisha kwamba kunatengwa fedha za kutosha kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutimiza wajibu huo ambao zinapewa za kuangalia au kuwatunza wenzetu walemavu. Kwa sababu bila kuhakikisha kwamba Halmashauri zinakuwa na bajeti nzuri kwa ajili ya kuwatunza wenzetu walemavu tutaishia pale pale kulaumiana kwamba tumetunga sheria, inaonekana nzuri, lakini utekelezaji wake ukawa hauwezekani. Kwa hiyo, naomba sana hili litiliwe maanani, liende sambamba na upatikanaji wa rasilimali kwenye Halmashauri zetu, kule Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba inazungumzia huduma mbalimbali kama afya na elimu na kadhalika kwa wenzetu walemavu. Wamezungumzia wenzangu suala la afya, mathalani suala la afya kuna walemavu wa aina mbalimbali, kuna wengine ambao ni walemavu, lakini uzalishaji mali kwao unawezekana na kwa maana hiyo hata kuongeza kipato wanaweza. Lakini kuna wengine ambao ni wategemezi kabisa hawawezi. Nilikuwa nafikiri ni vizuri sheria ingetamka wazi, badala ya kuweka mazingira mazuri tu, lakini sheria pia iweke matibabu kwa watu wa namna hii kwamba yawe bure, kwa sababu hawa hawana namna nyingine.

Mheshimiwa Spika, leo hata tukisema kwamba bima itashughulikia, lakini hata bima, mtu atakuwa anachangia kidogo, hicho kidogo atapata wapi pesa. Tungetamka bayana kama ambavyo kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imesema kwamba wazee wa umri fulani na watoto chini ya miaka mitano watapata matibabu bure,

tungetamka kwenye sheria hii kwamba matibabu kwa walemavu labda kama kanuni zitaainisha ni walemavu wa namna gani, basi matibabu yawe bure ili waweze kupata matibabu bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna unyanyasaji wa aina mbalimbali kwenye hospitali zetu mbalimbali. Mimi nimewahi kushuhudia mlemavu anapokwenda hospitali wakati mwingine haangaliwi haraka mpaka mwingine aingilie, msaidieni huyu. Tumesema Katiba imetoa haki kwa raia wote pamoja na walemavu. Kwa hiyo, kusiwe na kubaguliwa au kunyanyaswa kwa wenzetu wanapokwenda kwenye huduma kama hizo za matibabu.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la ajira. Muswada umesema vizuri sana na mimi naunga mkono. Suala la ajira kwamba panapokuwa na waajiriwa nadhani kumekuwa na marekebisho kwamba taasisi au kampuni iwe kiwanda kinapoajiri wafanyakazi zaidi ya 20 basi kuwe na kuhakikisha kwamba ninaogopa wenzetu walemavu wenye uwezo kwenye taasisi hizo wanaajiriwa. Lakini ninaogopa kwamba waajiri wengi kusipokuwa na kanuni ya kuwabana vizuri wengi watakuwa wanalikwepa hili. Hili wote tunalijua, unapokwenda kuomba kazi wanakwambia uzoefu wa miaka mitatu, uzoefu wa miaka mitano, leo huyu mlemavu anatoka chuoni amesoma vizuri hajafanya kazi hata mwaka mmoja unamwambia kazi ipo, lakini uzoefu miaka mitatu. Atapata wapi uzoefu? Labda sasa tufungue vyuo vya uzoefu. Unakwenda pale wanasema bwana kazi hii uzoefu miaka mitatu, mimi ndiyo natoka chuoni nitaupata wapi uzoefu? Lazima nianze mahali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nadhani kuwe na *deliberate move* za kuhakikisha kwamba waajiriwa hawa wanalazimishwa ili kuweza kuajiri hawa watu. Vinginevyo, wataendelea kusingizia na walemavu hawatapata kazi kwa kisingizio tu cha kwamba huyu hana uzoefu. Si wanataka wakwepe. Kwa hiyo, kanuni ziwe wazi kabisa za kuwabana waajiri ambao wanaweza wakalikwepa hili.

Suala lingine ambalo ningependa kulizungumza ni sehemu ya nane inayoweka masharti ya ujongeaji na huduma mbalimbali. Lakini hapa ninaomba nizungumzie suala la malalamiko yanayopelekwa na walemavu kwenye vyombo mbalimbali. Uzoefu unaonesha kwamba malalamiko ya Watanzania wengi acha walemavu, lakini Watanzania wengi kwa ujumla yanapopelekwa kwenye vyombo mbalimbali ziwe Mahakama, iwe Tume ya haki za binadamu au mahali pengine malalamiko haya yanachukua muda mrefu sana. Wakati mwingine watu wanakata tamaa. Sasa sheria hii ihakikishe malalamiko ya wenzetu walemavu yanayopelekwa kwenye vyombo mbalimbali yapewe msukumo.

Kwa hiyo, tutunge kanuni ambazo zitalazimisha malalamiko haya yashughulikiwe kwa kipindi gani, lakini tukiacha tu hivyo bila kusema kwamba malalamiko yanashughulikiwa kwa kipindi gani, utaratibu utakuwa ule ule. Malalamiko yanakwenda Tume ya Haki za Binadamu, yanakwenda mahali pengine yanachukua mwaka mmoja, miaka miwili, miaka mitatu. Mtu unaweza ukafa unaacha malalamiko yako hayajawahi kushughulikiwa. Kwa hiyo, ni vizuri tuwe na kanuni ambazo zitawabana au zitabana vyombo vile ambavyo vinatakiwa vitolee maamuzi kuhusu malalamiko ambayo yanapelekwa na wenzetu hawa walemavu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa nilizungumze, wenzagu wamelitaja, lakini nizungumze kwa namna nyingine, ni suala la ushiriki kwenye siasa. Hili linazungumzwa sehemu ya tisa ya Muswada. Hapa kuna mambo mawili, kushiriki kuchagua na kuchaguliwa. Hapa mimi naomba nizungumzie kuchaguliwa. Kuchagua siyo tatizo kwa sababu nina hakika wenzetu walemavu wamekuwa wanashiriki vizuri kuchagua viongozi wao. Lakini taabu inakuja wao wenyewe wanaposhiriki kutaka kuchaguliwa kwenye nafasi hizi.

Mheshimiwa Spika, bado jamii yetu haijaelimika vya kutosha na amezungumza vizuri mwenzangu Mheshimiwa Kabwe Zitto hapa kwamba watu wote wana haki ya kuchaguliwa *provided* ana sifa zinazostahili kuingia kwenye uongozi. Sasa jamii yetu haikubali moja kwa moja kwamba wanaweza kuongozwa na mtu ambaye ni mlemavu, achilia mbali wenzetu Wabunge ambao wameingia humu kwa kuchaguliwa na wenzao walemavu, lakini ukienda kule kijijini anasimama mtu mzima na mlemavu, inakuwa vigumu mlemavu kuaminiwa. Sasa Wizara ambayo imepewa dhamana hii, lazima ihakikishe elimu ya kutosha inakwenda kwa wananchi kuwaeleza kwamba wenzetu walemavu ambao wamesoma na wana sifa, kwa kuwa wana uwezo sawa sawa na watu ambao hawana ulemavu ili wenyewe waweze kushiriki vizuri kwenye shughuli hizi za siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nizungumze, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wengine. Lakini nitaka niliweke kwa namna hii. Suala la kuhakikisha kwamba sheria ikishapitishwa ianze kutumika, lakini na kanuni zitungwe. Ni kweli tumekuwa na tatizo, sheria inatungwa, unapita mwaka mmoja kanuni hazipo. Kuna sheria moja ambayo tulikuwa tunaipigia kelele, sikumbuki ni sheria gani tumeitunga sheria zaidi ya mwaka mmoja, kanuni hazipo! Sasa huu siyo utawala bora hata siku moja.

Ninaomba Waziri anayehusika ahakikishe kwamba tunapoipitisha na Mheshimiwa Rais akaisaini kuwa sheria, basi inachukua muda mfupi inavyowezekana ili kanuni zake zitungwe na ianze kutumika. Lakini ukisoma majedwali kwenye Muswada huu kuanzia jedwali la pili, la tatu na la nne, yanaunda Kamati mbalimbali kuanzia Taifa, Mkoa, Wilaya mpaka kule kijijini na kwenye Mtaa. Sasa sheria hii unaweza ukaona itatumika chini sana kama vile sheria zile nyingine za ardhi ambazo zinatumika sana kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sheria hii itafsiriwe mapema inavyowezekana kwa sababu wenzetu wanaoitumia kule chini hawajui Kiingereza kilichoandikwa humo, wapo wachache wanaweza wakasoma, lakini tafsiri yake iwepo. *(Makofi)*

Mimi nazungumza na bahati nzuri Waziri Mkuu yupo, *AG* yupo, sheria hii itafsiriwe na pengine kanuni zinapotungwa zitungwe moja kwa moja kwa Kiswahili ili kusiwe na muda mrefu zaidi wa kuanza kuhangaika na mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Godfrey Zambi. Waheshimiwa Wabunge, nimezingatia ushauri wa Katibu Mezani kwamba bado tuna muda wa kutosha kesho wa kuweza kupokea michango ya Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Said A. Arfi. Kwa hiyo, kuzingatia kwamba hata kama ningeruhusu mmoja wao aanze kuongea sasa muda uliobaki hautoshi na kwa msingi huo basi naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.42 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 14 Aprili, 2010 saa tatu asubuhi)*